ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	**-**	**SPIKA**
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais

20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo,

		Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
56. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy	-	Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 06 Juni, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe Katika kikao cha Baraza cha tarehe 1 Juni, 2017, Mhe. Abdalla Maulid Diwani aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na kuahidiwa kujibiwa kwa maandishi.

Katika kutimiza masharti ya Kanuni ya 40(4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016, Wizara hiyo imeleta majibu kama Waziri wa Wizara hiyo alivyoahidi.

Waheshimiwa Wajumbe sasa namuomba Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo asome jibu la swali la nyongeza alilouliza na Mhe. Mjumbe huyo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati ninajibu swali Namba 13, nililoulizwa kama swali la nyongeza na Mhe.Abdalla Maulid Diwani Mwakilishi aliyetaka kujua je ni wachezaji gani wa Zanzibar ambao wanacheza mpira huo Nje ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, orodha ya majina ya wachezaji hao ambao wanacheza nje ya Zanzibar ni kama ifuatavyo:-

1. Nadir Haroub
2. Haji Mwinyi
3. Said Juma
4. Mudathir Yahya
5. Agrey Morris
6. Abdalla Kheir
7. Mwadini Ali
8. Khamis Mcha
9. Suleiman Kassim
10. Adeyum Saleh
11. Abdul- azizi Makame
12. Moh'd Issa
13. Ibrahim Jeba
14. Omar Kheir
15. Nasoro Salum
16. Awadh Juma
17. Moh'd Faki
18. Abdalla Mundh-hir
19. Abrahman Othman
20. Nasoro Moh'd
21. Nasoro (Cholo)

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 90

Idadi ya Vitanda vya Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo Unguja na Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kamishna Mkuu wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar anastahiki pongezi kwa kazi kubwa aliyofanya ya kutengeneza vitanda kwa ajili ya wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo na hivi karibuni ameendelea na kazi hiyo kwa kutumia wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar.

Je, ni vitanda vingapi vinahitajika kwa ajili ya Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 90 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kabla ya kujibu nipokee pongezi kwa niaba ya Kamishna wa Chuo cha Mafunzo kwa hatua yake ya kuwapatia vitanda baadhi ya wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo. Aidha, kazi hiyo inaendelea kutekelezwa kadri uwezo wa kifedha unavyopatikana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla Chuo cha Mafunzo kinahitaji vitanda 300 vya chini na juu kwa ajili ya wanafunzi na Mahabusu wote wa Unguja na Pemba. Kwa hivi sasa vipo vitanda 10, kati ya hivyo vinane vinatumika kwa ajili ya wanafunzi watoto na viwili vinatumika kwa wanafunzi wa kike. Chuo cha Mafunzo kimo katika hatua za kumalizia vitanda vyengine 23 vinavyotengenezwa Chuoni hapo, vitakapokamilika vitanda 10 vitapelekwa kisiwani Pemba kwa ajili ya wanafunzi watoto.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na nilikuwa mzito kidogo hili swali nataka kuliuliza nilikuwa

nafikiria kwanza, lakini pamoja na majibu ya rafiki yangu kutojibu swali la msingi naomba kumuliza maswali madogo tu ya nyongeza kati (a) na (b).

(a) Mhe. Naibu Waziri hili jawabu sijui umelitoa wapi. Kwa upande wa Unguja tu wanahitaji karibu vitanda mia 400 wameshuka mpaka 350, sikwambii upande wa Pemba. Je, ni lini tutafanya ziara mimi na wewe mguu kwa mguu ukauone ukweli baada ya kuacha kuuziwa mbuzi kwenye gunia.

(b) Ni lini utaandika historia ya muda mrefu mimi kusimama hapa karibu mwaka hata mwaka kutetea kadhia hii ili kuondosha tatizo hili la kuandika historia. Je, juzi tumepitisha bajeti yenu kiasi gani cha fedha mlichotenga kwa kuwasaidia wanafunzi hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

a) Kwanza Mheshimiwa naomba nikupongeze sana kwa hatua mbali mbali na juhudi mbali mbali ambazo umezichukua, lakini niseme kwamba jibu ambalo tumelitayarisha ni jibu ambalo ndilo ambalo tumetegemea kwamba ndio lenye ukweli. Na taarifa hii ya vitanda mia 300 ndio mahitaji ambayo tumeyasema sisi kwa sasa hivi ambayo tunayoyahitaji. Lakini sambamba na hilo suala la kukubali kwamba labda twende tukaangalie mimi na wewe nadhani hilo jambo halina ugumu kwa upande wetu.

b) Naomba nimjibu Mheshimiwa kwamba kutokana na kadhia anayosema kwamba kila siku iliyokuwa ikijitokeza, sisi

wizara kwa mwaka huu kwa bajeti ambayo tumeipitisha juzi tunatarajia juhudi kubwa itafanyika ili kuona tatizo hili linaondoka na vitanda ni kwamba kama tumeeleza katika jibu la msingi, juhudi za kumaliza tatizo hili litafanikiwa na kwa utaratibu wa mwaka huu tunatarajia vitanda 100 vitatengenezwa kwa ajili ya kukubaliana na hali hiyo na nimesema kadri fedha itakavyokuwa imeruhusu tutaendelea kuongeza ili tuone ufanisi wa tatizo hili ili liondoke kabisa na ndio dhamira ya Serikali kuona jambo hili linafanikiwa.

Kwa hivyo naomba nikuambie Mhe. Mwakilishi kwamba kilio unachokitoa siku nyingi nadhani kitafika muda kitakwisha kwa utaratibu huu ambao tunakwenda nao.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kutoa majibu ya nyongeza kuhusu suala alilolisema Mhe. Jaku Hashim Ayoub hasa lile alilosema kwa Unguja tu tunahitaji vitanda 400.

Kwanza ninataka nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu fasaha na ya uhakika ambayo ameyasema, lakini nataka niseme kwamba kwa Unguja peke yake hatuhitaji vitanda 400, kwa sababu hivi sasa hivi mpaka leo asubuhi watu wote tulionao kwenye Vyuo vya Mafunzo, kwa maana ya wanafunzi na mahabusu ni 443. Kwa msingi wa vitanda tunavyovitengeneza ni vitanda ni vitanda vya *double deck.* Kwa hivyo wanafunzi waliopo ndani ya Vyuo vya Mafunzo kwa Unguja na Pemba ni 246 na mahabusi ni 197. Kwa hivyo ukifanya hesabu hiyo kwa Unguja hatuwezi kuhitaji vitanda 400 peke yake, inawezeka tukawa tunahitaji vitanda kama 300. Sisi tulipanga kutengeneza vitanda 300 kwa kuona wastani wa mahabusu na wale wanafunzi ambao wamo ndani ya Vyuo vyetu vya Mafunzo.

Kwa hivyo nimuhakikishie Mhe. Jaku Hashim kwamba vitanda ambavyo tayari kwa mwaka huu tumevitengeneza na vitanda ambavyo tutavitengeneza kwa mwaka wa bajeti ujao 2017/2018 vitanda 100, vitakuwa vinachukua idadi ya wanafunzi wasiopungua 250 mpaka 260.

Nam. 129

Utafiti wa Ufugaji Samaki Maeneo ya Jangwani

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Lakini kabla ya kujibiwa swali langu niliomba nifanye marekebisho kidogo kwenye swali. Kwa sababu kwenye Baraza letu tulisema tuliondoe neno, "vifaranga vya samaki". Kwa hivyo naomba kwamba pale kila linaposomeka neno "vifaranga vya samaki", liondoke na badala yake litamkwe, "kufuga samaki" au "samaki watakaofugwa".

Baaa ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba swali langu nambari 129 lijibiwe.

Kwa kuwa Wizara ya Kilimo ina wajibu wa kufanya utafiti ili kubaini aina mbali mbali za samaki watakaofugwa ambao wanaweza kufugwa. Na kwa kuwa maeneo mengi ambayo kwa Pemba yanaweza kufugia samaki kwa sasa ni sehemu za Majangwani ambayo kuna muungiliano wa maji ya chumvi na maji baridi hasa wakati wa mvua.

(a) Je, ni aina gani ya samaki watakaofugwa ambayo vinaweza kuishi vinapopatwa maji baridi na samaki hao wasiathirike kabla ya kuingiliwa na maji ya chumvi ambayo ndio hasa yanayokusudiwa kwa ufugaji huo.

(b) Je, vifaranga vya samaki Jodari, Nguru na Songoro ambao ni samaki wenye bei kubwa wameanza kuzalishwa na pia wanaweza kuishi kwenye mazingira kama hayo tunayoulizia.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wafugaji wa samaki kwa kuwapatia mafunzo ya ufugaji samaki na mitaji.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake namba 129 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo. Ninakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba maeneo mengi ambayo kwa Pemba yanafugwa samaki kwa hivi sasa ni sehemu za majangwani ambayo kuna muungiliano wa maji chumvi na maji ya baridi hasa wakati wa mvua.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Samaki wa aina ya mwatiko ndio aina ambayo vifaranga vya samaki hao vinaweza kuishi vinapopatwa na maji baridi na maji ya chumvi, yanayochanganyika na maji ya chumvi bila ya kuathirika kwa kiwango maalumu.

(b) Vifaranga vya samaki wa aina ya jodari, nguru na songoro ambao ni samaki wenye bei kubwa hawajaanza kuzalishwa na pia ni vigumu kuweza kuishi kwenye mazingira kama hayo ya majangwa katika maeneo ya

mikoko. Samaki wa aina hizi wanaweza kufugwa kwa ufanisi katika maeneo ya kina cha maji marefu hasa kutumia canjin.

(c) Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi katika mpango wake wa kawaida hutoa mafunzo kwa ajili ya wafugaji waliopo Unguja na Pemba. Aidha, mafunzo kama hayo yalitolewa mwaka 2016 na yanatarajiwa kutolewa tena hapa nchini mwaka huu wa 2017 kwa mashirikiano na wataalamu kutoka nchini China.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imeanza mazungumzo na taasisi za kifedha (benki) ili kupata mikopo ya kuwapatia mitaji wafugaji wa samaki. Benki ya Kilimo tayari imekwishawasilisha orodha ya masharti yao na kukamilisha mazungumzo ya awali na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Biashara, taasisi ya kifedha pamoja na kutembelea baadhi ya miradi hapa Zanzibar. Hivyo Waheshimiwa Wawakilishi wawe karibu na jamii na watayarishe vikundi vilivyomo kwenye majimbo yao waweze kupata mikopo hiyo.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri pamoja na kwamba umeniambia kwamba samaki aina ya mwatiko ni samaki ambao kwamba wanaweza kuishi kwenye muingiliano wa maji baridi na maji chumvi bila ya kuathirika. Samaki hawa ni katika jamii ya mikizi, lakini kwa kuwa samaki wa aina hiyo.

a) Je, kuna utaratibu gani wa kupata vifaranga vyengine au samaki wengine wadogo wa kufuga ambao wataweza kuishi kwenye maeneo hayo tuliyoyataja, ukitilia maanani kwamba tukifuga samaki wa aina hiyo tu watu wataweza kutumia samaki

wa aina moja jambo ambalo litakuwa si zuri, kwanza tukitilia maanani kwamba chakula watu wengi siye tunakula samaki.

b) Lakini pia kuhusu habari ya uwezekano wa kupata hiyo mikopo. Je, hizo taasisi ambazo zimeshakubali kutoa mikopo kwa hao wafugaji wa samaki. Je, wapo tayari kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa lengo la kuwasaidia hao wafugaji wa samaki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe utulivu ni mdogo sauti zimekuwa kubwa, majibu ni kwa sisi sote, majibu yanapotokea pamoja na kuwa anajibiwa Mjumbe lakini ni kwa sisi sote. Kwa hivyo tuwe watulivu katika kusikiliza majibu ya hoja zinazotolewa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Omar Sief Abeid kwa maswali yake mawili na ninapenda kumjibu kama ifuatavyo:-

a) Ni kweli kwa sasa tunafuga sana samaki wa mwatiko lakini vile vile wako perege wanafugwa na aina kama ya changu wako wanafugwa na aina nyengine za samaki mbali mbali wanafugwa, lakini sasa hivi taasisi yetu ya utafiti wa samaki pamoja na *hatchery* tuliyojenga, kazi yake kubwa ni kufanya utafiti zaidi kuona aina gani za samaki tunaweza tukazifuga mbali na hili tunazozifuga. Kwa mfano sasa hivi tuna majongoo yataanza kufugwa, kaa, pweza tunafuga na kadhalika. Kwa hivyo nasema zipo aina nyingi za samaki tunafuga lakini hivi kituo chetu cha-*hatchery* utulichokijenga Kizimbani ambao mwezi wa nane kitaanza kufanya kazi rasmi kitakuwa na aina nyingi za samaki ambazo tunaweza kuzalisha na vifaranga kuweza kupeleka kwa wafugaji wetu.

Kwa hiyo nasema nakubaliana na kwamba kunahitaji kufanya utafiti zaidi, kujua aina nyingi za samaki lakini zaidi si aina za

samaki, ni samaki ambao watakwenda kwenye soko watauzwa na watapata bei na watu watawapenda. Hilo ni jambo la msingi ambalo la kuzingatia.

b) Kuhusu suala la mikopo ya fedha kwanza nasema niwashukuru sana Benki yetu Kilimo ya Tanzania Bara ambayo jana wamesaini fedha bilioni 209 walizopata kutoka *ADB* ambazo wamekubali katika fedha hizo kupitia taasisi zetu za Benki zilizoko Zanzibar hapa kuziingiza pale na kuweza kupata mikopo bei nafuu.

Nafuu ya kwanza wao wanatoa *grace period* wanatoa muda wa kutokulipa kwa mfano mwaka mmoja, miwili kabla ya kuanza kulipa.

Nafuu ya pili riba yao ni ndogo ni asilimia 8 mpaka 12. Kwa hivyo kuna manufaa makubwa ambayo wakulima watayapata. Jambo la msingi ni watu kuamua kufanya biashara kwa sababu ukikopa unatakiwa kulipa, si pesa ya sadaka. Hilo la kwanza. Lakini la pili ni sisi Wajumbe Wawakilishi ku-*organise* vikundi maalum ambavyo vitasimamia na kuweza kufanya kazi hizi kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri umesema katika ufugaji wa samaki mpaka samaki wa changu, tasi. Samaki wa Changu mara nyingi hupendelea kuishi katika miamba.

Je, kuna utaratibu gani wa kuweza kufuga samaki hawa kupitia kwenye mabwawa na ukizingatia mle hamna miamba.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali kama ifuatavyo.

Kwanza taaluma za kufuga samaki zimepanuka sana. Hata wale samaki wanaokuwa kwenye maji makubwa sasa hivi tunaweza kuwafuga kwa kutumia utaratibu wa *caging* ambao ninaousema. Mhe. Mwenyekiti, unakwenda kwenye bahari, unaweka *cage* yako halafu samaki unawafuga mle ndani. Hizi taaluma zimepanuka sana sasa hivi, sio kwamba tunategemea kufuga samaki katika mabwawa tu kama tunavyofanya sasa hivi,

Kwa hivyo ninasema hizo taaluma zipo na sasa hivi tunaanza utaratibu wa kuangalia namna gani kupata angalau *cage* kumi au kumi na tano tuanze kufuga samaki wa tuna kwa mfano katika bahari kuu ili waweze kusafirishwa nje. Kwa hivyo aina ya kufuga samaki siyo ile ya kuchimba bwawa tu peke yake, kuna aina nyingi na utaalamu upo mkubwa sana na tukiutumia utaalamu huo naamini kabisa tunaweza kufuga aina nyingi za samaki.

Mhe. Makame Said Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri anayoyajibu katika jibu mama, kwa kusema ukweli kama samaki wanaotajwa katika hili hawawezi kuwa katika maji ya mchanganyiko. Hili ni sahihi lakini tu nimuulize swali moja la nyongeza ambalo linahusu katika majibu ya swali la pili amesema kwamba kama wanaongeza ufugaji wa kubadilisha aina ya baadhi

ya samaki mpaka kamtaja na pweza kama na wao pia wako tayari kuanzisha kufuga.

Lakini ninavyofahamu mimi pweza wapo wa aina mbili. Sasa sijui ni pweza wa aina gani ambaye ataweza kuhimili maji haya mchanganyiko, nataka anibagulie ni pweza wa aina gani ambaye anaweza kuishi, maana kuna pweza wa nyuri nane, kuna wengine nyuri mpaka zaidi au upungufu wa hapo.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na naomba kumjibu swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwamba kuna aina nyingi ya ufugaji, kuna ufugaji wa kuchimba bwawa. Kwa mfano Kisiwa Panza pale tumetenga eneo maalum ambalo ambalo tunalifunga kwa muda wa miezi mitatu, kabla ya kufunga unakuta pweza ana ukubwa wa kilo tatu, baada ya miezi mitatu ukifungua ana kilo sita. Kwa hivyo tunafuga vile vile. Tatizo tulilonalo ni kwamba watu wanavamia na sasa hivi tunataka kufungua maeneo mengine kama vile Tumbatu na kadhalika kama maeneo saba.

Kwa hivyo aina zote za pweza unazozitaja kwa sababu tunawafuga katika mazingira yao yale yale basi inakuwa sio tatizo hata kidogo kuweza kupata aina ya pweza tunaowahitaji.

Nam. 95

Kero ya Wafanyabishara Kulipishwa *VAT* Mara Mbili Haijatatuka

Mhe. Jaku Hashm Ayou - Aliuliza

Mhe. Mwenyekiti, kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko wafanyabishara kulipishwa VAT mara mbili wakiwa Dar es Salaam na mzigo unapofika Zanzibar nako wanalipishwa VAT. Suala hili limekuwapo muda mrefu licha ya kudaiwa kushughulikiwa mara kwa mara lakini hakuna mabadiliko yoyote.

(a) Mhe. Mwenyekiti, serikali haioni kuwa mtindo huu ni sawa na kuwaonea au kuwakandamiza wafanyabishara.

(b) Mhe. Mwenyekiti, serikali haioni sasa wakati umefika kuafikiana na Upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano jambo hili linalokera sana likamalizwa.

(c) Ni lini hasa jambo hili litafikiwa mwisho.

Mhe. Waziri wa Fedha wa Mipango - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali Nam. 95 la Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, mfumo wa kodi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unahusisha kodi za muungano na zisizo za muungano. Kodi hizo za muungano ni ushuru wa forodha, kodi ya mapato na ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini. Kodi nyengine zote ikiwemo kodi ya ongezeko la thamani si kodi za muungano. Hivyo kwa mujibu wa Katiba kila upande wa Jamhuri ya Muungao wa Tanzania unaruhusika kuwa na sheria yake pale inapohitajika. Kwa kutambua kuwa kodi hizo za biashara zina athari kubwa katika biashara baina ya pande mbili za Jamhuri ya Muungano, kwa muda mrefu zimekuwa zikizingatiwa na kila upande na aghalabu huwa na utaratibu na viwango vinavyofanana.

Mhe. Mwenyekiti, si sahihi kuwa tatizo la kodi ya *VAT* baina ya pande mbili za Jamhuri ni la muda mrefu bali limetokana na

mabadiliko yaliyofanywa kwenye Sheria ya *VAT* ya Tanzania Bara kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 ambayo yaliondoa utaratibu wa muda mrefu uliokuwa ukitumika wa uwakala wa Hazina za pande mbili, kukusanyia upande mwengine pale bidhaa zilizohusika zinapohaulishwa kwenda upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utaratibu huu uliambatana na marejesho ya kodi kwa bidhaa hizo zilizohaulishwa. Ni takriban mwaka sasa tokea mabadiliko hayo kufanyika.

Mhe. Mwenyekiti, chini ya utaratibu mpya, bidhaa zinazotengenezwa Tanzania Bara zinaponunuliwa kutoka kiwandani na mfanyabiashara aliyesajiliwa chini ya Sheria ya *VAT* ya Zanzibar na kuhaulishiwa na kutumika Zanzibar, kiwango cha kodi ya *VAT* kwa Tanzania Bara kitakuwa ni sifuri na hivyo *VAT* italipwa Zanzibar wakati wa kuingizwa bidhaa hizo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba sasa kujibu swali la Mhe. Mwakilishi la msingi kama ifuatavyo:-

(a) Pamoja na kasoro za utaratibu wa sasa bado Serikali haioni kwamba inawakandamiza wafanyabiashara wadogo ambao wanatozwa kodi kwa Sheria zilizopo.

(b) Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa huu ni wakati muafaka wa kuafikiana baina ya pande zetu mbili na kulimaliza suala hili. Kwa upande wetu, SMZ imechukua jitihada kubwa kuzungumza na wenzetu wa Tanzania Bara juu ya athari ya mabadiliko ya Sheria yake ya *VAT* kwa biashara baina ya pande mbili hizi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tunaziendeleza jitihada hizi za kuzungumza na wenzetu.

(c) Mhe. Mwenyekiti, suala hili linahitaji ridhaa na niliwahi kulijibu katika Baraza hili kwamba kwa sababu siyo suala

la Muungano, kila upande una sheria yake ni suala ambalo linahitaji ridhaa ya pande mbili ili liweze kumalizika. Kwa hivyo jitihada ya Wizara ni kuendelea kuzungumza na wenzetu ili kutafuta njia bora zaidi ya kufanikisha biashara katika pande zetu mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na darsa niliyoipata kwa Mhe. Waziri hivi asubuhi niombe kumuuliza maswali mawili madogo tu ya nyongeza.

Alipokuwa anajibu swali (a)

a) Pamoja na kasoro za huo utaratibu wa sasa bado serikali haionei wala kukandamiza wafanyabiashara, hili nitamwambia Mhe. Waziri itakuwa kateleza kibinadamu lakini *ZRB* wamepiga kambi bandarini hawajui chochote wala hawasikiii chochote kinachozalishwa kutoka Tanzania Bara ikiwa nondo, ikiwa *gypsum powder* wanakwambia lete tu wewe.

Kwa hivyo naomba ukae na *ZRB* uwape darsa kama uliyonipa mimi, wao hawajali chochote wanakwambia lete tu, imekuwa kama maandishi ya Kiarabu wanavutia kwao tu. Nakuomba ukae nao, ushahidi upo na ukiuhitaji sina mashaka nao na hasa kwa utendaji wako.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa uliza swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ndiyo swali lenyewe namwambia Mheshimiwa ungenisikiliza ninachokizungumza Mhe. Mwenyekiti kwanza.

b) Katika mapato unaweza kutwambia tumepokea kiasi gani kutoka kwa ndugu zetu wa damu kuhusu *payee* kwa mwezi tumepokea shilingi ngapi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Nimesema kwamba wafanyabiashara hawaonewi na msingi wa kusema hivyo ni kwamba wanatozwa kodi hiyo kwa mujibu wa sheria zilizopo. Nilisema kwamba suala hili siyo suala la Muungano. Bara wana Sheria ya *VAT* Nam. 11 mwaka 2014 na Zanzibar tuna Sheria yetu ya mwaka 1998 na kila upande ina haki ya kutoza kodi ya *VAT* vile inavyoona yenyewe inafaa.

Sasa mazungumzo ya pande mbili ni muafaka kwa ajili ya kuweka mustakbali mzuri wa biashara katika nchi yetu, lakini hapo hakuna maonevu. Wakati wenzetu walipobadilisha sheria hii, sisi Wizara ya Fedha tulikaa na wafanyabiashara na tukawafahamisha juu ya mabadiliko haya na tukawaelekeza jinsi gani ya kufanya kuepuka hili. Kwa sababu kama biashara bidhaa iliyozalishwa Tanzania Bara inahaulishwa upande wa Zanzibar, kwa maana kule ni lazima iwe *zero rated,* kwa maana *VAT* iwe katika kiwango cha sifuri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ili hilo liweze kufanyika ni lazima kwanza huyo mnunuzi mwenyewe awe amesajiliwa kama mlipa kodi ya *VAT* hapa Zanzibar. Lakini pia bidhaa hiyo ainunue kutoka kwa mzalishaji ili kule asitozwe kodi hiyo na bidhaa hiyo lazima ihaulishwe kuja upande wa Zanzibar. Sasa kodi hiyo itakuja kulipwa kwa upande wa Zanzibar. Sasa akinunua nje ya utaratibu huu, itabidi kule akatwe alipe *VAT* na hapa kwa sababu

ZRB haiwezi kutambua hivyo kutokana na sheria zilizopo na hapa ndiyo wanakumbana na kulipa kodi hiyo mara mbili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo sio suala la maonevu ni suala la sheria zilizopo. Lakini zinakubaliana kwamba wafanyabiashara wetu wadogo wadogo wanapata matatizo na usumbufu huo na ndio maana nikasema wizara zetu mbili zitaendelea kuzungumza juu ya suala hili ili kusaidia wafanyabiashara wetu wadogo wadogo. Hilo ningeomba Mhe. Jaku Hashim akubaliane kwamba mambo yote yanayofanywa hivi sasa yanafanywa kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mhe. Mwenyekiti, aliulizia kiwango. Kulikuwa na kodi ambayo sisi tulikuwa tunaidai kwa maana ya marudisho kwa mwaka ule wa 2015/2016 ambayo ilikuwa inakaribia bilioni 9. Lakini tokea kupitishwa Sheria hii, hakuna *VAT* ambayo sasa tunaidai kutoka kwa upande wenzetu. Na hizo za nyuma zinaendelea kulipwa kwa mujibu wa makubaliano baina ya pande mbili au baina ya Wizara zetu mbili, Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungao na Wizara ya Fedha ya Zanzibar ambapo hakuna tatizo mpaka hadi sasa hivi katika masuala haya. Tunaelewana katika marudisho ya zile *VAT* ambazo ni halali kurudishwa upande wa Zanzibar. Lakini kwa sasa hivi kwa sababu utaratibu huo haupo, kwa hivyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzirar haidai *VAT* kwa mwaka huu wa 2016/2017 tokea kpindi kile ambacho sheria imepitishwa rasmi ya *VAT* kwa upande wa Tanzania Bara.

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Soma utaratibu, kifungu gani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante, Kifungu cha 63 kuhusu utaratibu na 37 kwa Mhe. Waziri nafikiri hakunisikia swali langu la pili, naamini kuwa hakunifahamu, bora uniruhusu nimwambie tena ili aweze kusikia.

Nilichomwambia kuhusu *payee* yaani *BOT*, Jeshi, Polisi, mapato yetu kwa mwezi yanafika shilingi ngapi kutoka kwa ndugu zetu wa Tanzania Bara. Na la mwanzo vile vile halikukaa sawa. Kule unanunua mali kiwandani kama nondo na mtu ana usajili hapa bado analipishwa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti,

a. Kama Mhe. Mwakilishi ana ushahidi wa kwamba huyo mtu kafuata utaratibu wote na bado hapa kalipishwa naomba tuonane na anipe ushahidi. Lakini kiutaratibu hakuna suala hilo lakini kama upo ushahidi huo nitamuomba baadae anisaidie na tutalifuatilia.

b. Kama *payee* kutokana na wafanyakazi wa SMT waliyokuwepo hapa, *payee* ambayo imepangwa kulipwa kwa mwaka ni bilioni 21. Sasa sijafanya hesabu za haraka haraka, gawa kwa 12 tutaweza kupata *average* ya *payee* kwa mwezi.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kama ifuatavyo.

Mhe. Waziri najua kwamba ulikuwa una-*propose* ya kuwapunguzia bei wafanyabiashara wanaoingiza chakula nchini hasa kwa mwezi huu wa Ramadhani ili chakula kipungue bei.

a) Je, kodi hiyo umewapunguzia.

b) Je, chakula hicho unafanya *monitoring* gani kujua kama kodi hiyo umewapunguzia na kimepungua bei kwa wananchi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kama ulivyo utaratibu kwa kila mwaka, serikali hutoa unafuu wa bei katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Kipindi hichi pia kwa mwezi Mtukufu huu tunaoendelea nao serikali imefanya hivyo na tumetoa unafuu huo tokea tarehe 10 Mei, 2017 na utaendelea unafuu huo mpaka tarehe 25 Juni, 2017. Na unafuu ambao tunautoa ni kwa bidhaa nne (4), sukari, mchele, unga wa ngano na tende.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kawaida kabisa na naomba niwaeleze Waheshimiwa Wajumbe kwamba sukari ilipaswa ilipwe kwa *rate* za Jumuiya ya Afrika Mashariki asilimia 60 ya CIF. Lakini kwa Zanzibar huwa tunatoza kwa miezi ya kawaida asilimia 12.5. Lakini kwa mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni asilimia sifuri, hamna lakini kwa bidhaa ya mchele kikawaida kwa jumula ya *rate* ni asilimia 75. Miezi ya kawaida ni asilimia 10. Mwezi wa Mtukufu wa Ramadhani sifuri kabisa hamna kitu. Mhe. Mwenyekiti, unga wa ngano *rate* ni asilimia 25, kwa miezi ya kawaida ni asilimia 10 lakini Mwenzi Mtukufu wa Ramadhani sifuri. Tende kwa miezi ya kawaida ni asilimia 25 lakini kwa mwezi Mkutufu wa Ramadhani sifuri.

Mhe. Mwenyekiti, hili Mhe. Rais mwenyewe amewahimiza wafanyabiashara watoe unafuu huo. Sasa kama kuna wafanyabiashara ambao wanaitumia vibaya fursa hii na

Mheshimiwa unawajua twambie, hatua tutazichukua kwa wafanyabiashara hao. Kwa sababu huo unafuu umetolewa na Serikali kwa kuwasaidia wananchi katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani na ufuatiliaji unafanywa. Lakini kuna Wizara ya Biashara, kuna kitengo maalum ambacho kinafuatilia suala hili, lakini na wananchi na wao wanapokuwa na taarifa hizo waiambie serikali ili tuweze kuwajua wafanyabiashara wa namna hiyo ambao wanapata unafuu huo lakini hawaupeleke unafuu huo kwa wananchi.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ametupatia na yenye kufahamika. Mimi naomba nimuulize swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Waziri ni kweli kwamba umesema ndani ya mwezi Mtuku wa Ramadhani mmeweka asilimia ziro kwa ajili ya wanaofanya biashara waweze kufanya biashara vizuri. Lakini je, huoni kwamba kuweka asilimia hii kwamba wasilipe chochote wanaweza kuleta vitu kwa njia ya udanganyifu kwa kupitia ndani ya mwezi huu wa Ramadhani.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Suala kubwa ambalo tunalihimiza kwa wafanyabiashara wetu ni suala la uadilifu na uaminifu. Serikali inatoa hii kwa nia ya dhati kuwasaidia wananchi wake lakini pia na wafanyabiashara na wao kupata unafuu. Kama nilivyosema mwanzo *rate* tunazozitumia hapa sio *rate* za Jumuia ya Afrika Mashariki, huwo pia ni unafuu peke yake. Sasa na wao wachukuwe ubinaadamu huo huo, kwa

wale ambao hawachukui ubinaadamu huo wa kuondosha udanganyifu huo, sisi wale ambao wanadanganya tutawafatilia na nimesema watu wanaowajua watwambiye. Wizara zipo zinazohusika na suala hilo ili hatua zichukuliwe. Lakini serikali inafanya hivyo kwa niya ya kuwasaidia wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti, ninachosema ni kweli anaweza akatokezea kwa yule ambaye siyo muaminifu kuitumia fursa hiyo kuleta kiwango kikubwa ambacho pengine kitatumika nje ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Tunawaomba tunawaomba wasifanye hivyo kwasababu kodi ni pamoja na wao, kodi ikiongezeka tukikusanya kodi katika nchi hii tukiongeza huduma za kijamii lakini na uwekezaji ukiimarika katika nchi hii biashara zao pia zitakuwa kwa hiyo ni suala la taaluma na tutandelea kutoa taaluma hiyo kwa wafanyabiashara wetu ili waweze ku-*comply* na sheria za kodi ziliyopo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti jina kamili rasmi ni Suleiman Sarahan Said na mimi naomba swali langu namba 157 Wizara ya Ardhi lijibiwe.

Nam. 157

Migogoro ya Ardhi

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejitahidi sana kupunguza migogoro ya ardhi mpaka kufikia kuanzisha Mahakama ya Ardhi. Hata hivyo bado suala hilo linaonesha ndio kwanza linakua kuliko kupunguwa, inaonekana labda baadhi ya Sheria zimepitwa na wakati.

a) Je Serikali inalijua hilo.

b) Je, Serikali iko tayari kuzifanyia marekebisho baadhi ya Sheria za Ardhi ili kupunguza migogoro hiyo.

c) Je, Serikali imejipanga vipi kupunguza au kumaliza kabisa migogoro ya Ardhi inayoshamiri siku hadi siku.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi Maji Nishati na Mazingira naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said wa Chakechake swali lake namba 157 lenye vipengele (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

a) Sekta ya ardhi inaongozwa na Sheria tisa ambazo bado zinafanya kazi na wakati na kupitia sheria hizo ndizo zinazoifanya sekta ya ardhi kupata ufanisi mkubwa katika utekelezaji wa kazi zake za kila siku. Tatizo kuu la kuendelea kuwepo migogoro ya ardhi ni kutokana na sababu nyengine kama zifuatazo:

- Kuwepo kwa utapeli na udandanyifu kwa baadhi ya wananchi ambapo huuza maeneo zaidi ya mara moja

- Lakini pia wananchi kutofuata taratibu za kupatiwa hati za haki ya matumizi ya maeneo
- Kuwepo kwa uvamizi wa maeneo ya Serikali

b) Utaratibu wa Serikali kuzifanyia marekebisho sheria mbalimbali upo pale ambapo itaona ipo haja ya kufanya hivyo. Aidha, kwa vile Serikali hivi sasa ipo katika hatua za mwisho za kukamilika kwa Sera ya Ardhi, Serikali itaweza kufanya marekebisho ili kuweza kuendana na Sera ya Ardhi.

c) Miongoni mwa sababu kubwa ya kuwepo migogoro ya ardhi ni kutokana na kukukuwa kwa uchumi na kuongezeka kwa thamani ya ardhi. Serikali imeweza kuweka njia mbalimbali za kuhakikisha inaondosha kabisa migogoro ya ardhi. Baadhi ya njia hizo ni kama:

1. Kuendelea na zoezi la utambuzi na usajili wa ardhi katika maeneo yote ya Zanzibar.

2. Kuimarisha shughuli za Uhaulishaji wa Ardhi, Taasisi za Serikali zinashirikiana katika hatua za Uhaulishaji ambapo hatua huanzia katika ngazi ya Sheha na Wilaya na baadaye kufanywa uhakiki wa eneo kwa kupitia wataalamu lengo la utaratibu huu ukiwa kuhakikisha Taasisi zote hizo zinafahamu na kutoa taarifa juu ya uhaulishaji husika.

3. Utatuzi wa migogoro unaofanywa na Kamisheni ya Ardhi kwa kushirikiana na Taasisi mbali mbali hususan Ofisi za Mikoa na Wilaya hupelekea kutatuliwa migogoro kwa ufanisi na wananchi huridhika na maamuzi yanayotolewa bila ya kufikishwa mahakamani baadhi ya migogoro.

4. Kuendelea na utaratibu wa kuyapanga maeneo mbali mbali kwa kuipatia *Master Plan*.

5. Kutolewa kwa Elimu, Serikali kupitia Taasisi zake za Ardhi ikiwemo Kamisheni ya Ardhi, Bodi ya Uhaulishaji Ardhi na Mahakama ya Ardhi zimefanya jitihada kubwa ya kutoa elimu kupitia vyombo vya habari na katika ngazi mbalimbali kuhusiana na masuala ya ardhi kwa lengo la kuondoa migogoro.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti na mimi nimsifu Naibu wangu Waziri kwa majibu yake mazuri sana lakini nimpe maswala moja lakini lenye (a) na (b) la nyongeza.

a) Kwa kuwa una mpango wa kupunguza au kumaliza kabisa migogoro ya ardhi hapa Zanzibar swali jee ni lini utadhibiti na kumaliza kabisa utapeli wa kuuziana ardhi Zanzibar. Lakini swali la pili

b) Bado una mpango wa kuimarisha Mahakama za Ardhi ambazo ni pesa nyingi sana na wewe unamaliza migogoro huoni kwamba utatumia pesa nyingi zilizokuwa hazina haja baadaye.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said Mwakilishi wa Chakechake swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Kuhusina na namna ya kuweza kuzuwiya utapeli hili ni suala letu sote viongozi na wananchi kwa jumla kwa sababu hasa baadhi ya wananchi ambao si waaminifu ndio wanaosababisha hili sasa kwa pamoja wetu tutaweza kulizuwia.

b) Haja ya kuwepo kwa Mahkama ya Ardhi ipo kwa sababu migogoro haijamalizika kwa hiyo ni sawa kwamba makosa yako duniani ndio maana kukawa sheria na adhabu kungekuwa hakuna makosa kungekuwa hakuna haja ya sheria na adhabu sasa ikimalizika migororo

mojamoja basi kutakuwa hakuna haja hiyo, lakini madamu migogoro bado ipo ingawa kwa kiasi kidogo kulinganisha na huko tunapotoka utaona ipo haja ya kuwepo Mahkama ya Ardhi na nyenginevyo si kupoteza pesa. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a)

Mhe. Waziri migogoro ya ardhi mara nyingi husabishwa na baadhi ya Masheha pamoja na baadhi ya Watendaji wa Wizara yako jee unalijua hili na kama unalijua ni hatua gani za kisheria unawachukulia Watendaji hao pamoja na Masheha wanosabisha hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa idhini yako kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira naomba kumjibu Mhe. Suleiman Makame wa Ziwani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Taarifa hii sina ya kwamba baadhi ya Masheha na Watendaji wanaohusika katika hii habari lakini nikuombe tuu kama una taarifa zilizosahihi tuletee na sisi tuzifanyie kazi na hatua zichukuliwe. Ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali kwa makusudi imeweka Ardhi ya Mahkama ili kuondoa kero na matatizo yanayowakabili wananchi wetu hasa wale wanyonge ambao hawana pa kukimbilia lakini matatizo ya ardhi mara nyingi yanaanzia kwa Masheha wetu baadhi yao kwa sababu utamsikia mwananchi kiwanja hiki kaniuzia Sheha jee naomba Wizara itowe kauli rasmi mwananchi anapotaka ardhi hasa aende wapi, aanzie wapi ili matatizo haya yasiwakute wananchi wetu ambao yanawazonga bila ya kujitambuwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Ni kwamba mwananchi anayetaka ardhi aende Kamisheni ya Ardhi na hata wanapokuwa wanauziana ni vyema anayenunua kabla ya kununua basi aende pale kwa sababu tuna utamaduni wananchi kwamba tunauziana kwa mfano nyumba na tunamalizana huko kwa huko sasa ni vyema katika kupunguza hiyo migogoro kabla ya kununua uwende Kamisheni ya Ardhi, Bodi ya Uhaulishaji kwa ajili ya usalama na kupunguza migogoro nchini. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kupata jawabu la swala 168.

Nam. 168

Changamoto ya Ubora wa Huduma Za Zantel

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Kampuni ya Zantel imekuwa ni kielelezo cha huduma za mawasiliano kwa upande wa Zanzibar kwa miaka mingi sasa. Hata hivyo, kadiri siku zinavyokwenda huduma za Kampuni hiyo zimekuwa zikizorota mara kwa mara. Mara kadhaa mtandao huo hukatisha mawasiliano bila taarifa, wakati mwengine mteja hukatwa fedha kwa huduma ambayo haifahamu, au makato yanatangulia kabla ya huduma haijaanza.

Je, nini tatizo kampuni hiyo kuzorota huduma zake mara kwa mara na kusababisha usumbufu kwa wananchi.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Mhe. Jaku Hashim Ayoub wa Jimbo la Paje suala lake Nam. 168 kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni faraja kubwa kwa Zantel kuwa kielelezo kwa miaka mingi katika kuwahudumia wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Mmiliki mpya aliyenunua hisa za Zantel mwezi Oktoba 2015, aliliona suala la uchakavu mkubwa wa mitambo iliyokuwa ikitoa huduma hizo ambazo kwa kiasi fulani imeshapitiwa na wakati. Uchakavu wa mitambo hiyo, ndio changamoto kubwa iliyokuwa ikizikuta Zantel pamoja na wateja wake.

Mhe. Mwenyekiti, kipindi kizima cha mwaka 2016, Zantel ilijijengea mpango mkakati wa kuimarisha huduma zake ambao ulihusisha kuinua viwango vya wafanyakazi wake pamoja na kubadilisha mitambo chakavu na kuweka mitambo mipya ya mawasiliano ya sauti na taarifa *(internet)* kwa visiwa vya Unguja na Pemba. Zoezi hilo la uwekaji wa mitambo mipya lilianza tarehe 31 Januari 2017 na kutegemewa kumalizika mwisho wa mwezi wa June 2017. Aidha, tayari wateja wa Zantel katika

maeneo mengine wameshaanza kupata huduma bora hasa katika yale maeneo ambayo mitambo mipya imeshafungwa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwanza nimpe salamu zake kutoka kwa wananchi wakati wa bajeti yake alipoipitisha hivi juzi na hasa katika yale maeneo ya skuli nimpongeze sana Mhe. Waziri salamu hizo nikuulize tuu maswala madogo ya nyongeza.

1) Ni maeneo gani ambayo wameshaanza kupata huduma bora kwa upande wa Unguja na Pemba wakati ulijibu hapa swala hivi sasa kuna huduma bora hasa katika maeneo ambayo mitambo mipya imeshafungwa ni eneo leo gani limeshafungwa mitambo mipya na wapi linapata huduma bora.

2) Zanzibar ninavyokumbuka ilikuwa na *share* yake katika Kampuni ya Zantel jee *share* ile ingalipo mpaka muda huu na Zanzibar imenufaika na kiasi gani kutoka kwenye Kampuni hiyo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala la kwanza kuhusu huduma bora ningependa kumuhakikishia Mwakilishi pamoja na Baraza lako Tukufu kwamba huduma za Zantel zimeboreshwa kwa kutumia mitambo mipya na pia wamekwisha anzisha utaratibu wa mawasiliano wa 4G yaani *Fourth Generation* kwa Unguja na Pemba kwa hivyo hapo naweza nikasema wazi kwamba huduma hizo zimeboroshwa na bado wamo katika mkakati wa kuweza kuzifanya huduma zao ziwe bora zaidi kwa kubadilisha mitambo na kutumia mitambo ya kisasa.

Kwenye swala hili la Hisa za Serikali ya Zanzibar kwenye Kampuni ya Zantel kwanza kabisa Mhe. Mwenyekiti ningependa kusema wazi kwamba Shirika la Zantel ni Shirika lilokuwa ni *private* yaani ni Shirika lenye wenyewe wenye hisa huko ni Kampuni ya Milcom ambao walinunua hisa hizo kutoka Kampuni iliyokuwa inamiliki Zantel hapo zamani na Serikali yetu bado ina hisa asilimia kumi na tano kwenye Zantel.

Lakini hisa hizo kumi na tano kwa mia hazituwezeshi sisi kubadilisha Sera na Usimamizi yaani *Management* wa Kampuni ya Zantel, ingawaje tunashiriki kwa kuwa tuna watu wawili katika Bodi ya Zantel moja akiwa Katibu Mkuu wizara yetu ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na pili ni Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Bodi inapokaa ya Zantel huwa hao wanashirikishwa katika kufanya maamuzi, kwa hivyo kimsingi ninachotaka kusema ni kwamba hisa zetu bado ni kumi na tano kwa mia. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Soma utaratibu Mhe. Jaku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwanza nikupongeze katika Wenyeviti wanaokubali utaratibu moja wewe nikupongeze kwa dhati kabisa tofauti na wengine wanaokalia kiti hicho.

Mhe. Mwenyekiti: Soma kifungu kieleweke.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Muda unakwenda Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Soma maelekezo kusudio.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: 63 taarifa kuhusu utaratibu mjumbe anaweza kusimama wakati wowote kusema maneno kuhusu utaratibu lakini mjumbe anapofanya hivyo itabidi ataje Kanuni ya Baraza iliyokiukwa ya mjumbe yoyote nafupisha hapo maana ni kubwa nakuja kunako 37 Waziri au mjumbe yoyote aulizwe swali ambalo ana madaraka nalo anakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kwa usahihi kwa ufupi isipokuwa kwamba swali alouliza Waziri mmoja linaweza kujibiwa na Waziri mwengine au Mwanasheria Mkuu ndio hapo ninapokuja.

Mheshimiwa rafiki yangu hakunisikia.

Mhe. Mwenyekiti: Lete hoja yako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hoja yangu ni maeneo gani kwa upande wa Pemba waliopata huduma bora na Unguja ni maeneo gani yalopata huduma bora hilo la kwanza. La pili ni nchi ya Zanzibar *share* yake ni *amount* gani iliyopata tokea muda huo kujiunga.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa swali lako ambalo ulikuwa unaliuliza tayari jawabu lake limeshatoka. *(Makofi)*

Kaa kitako Mhe. Jaku, Mhe. Omar nimekuona katika swali la nyongeza.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuza swali dogo kwa kuwa kupata huduma ni haki ya mteja anapoomba huduma na anapolipia huduma kwa kumtoa huduma lakini ni ukweli usiofichika kwamba Kampuni ya Zantel kwa sasa huduma zake zimekuwa si za kuridhisha kama tulivyoambiwa kwamba na unaweza kuzungumza eko imezidi unajisikia mwenyewe maeneo mengi hupati mfano toka juzi tu na kwenye jibu lake alojibu mwaka jana wakati anafanya

majumuisho alisema Zantel watafunga mitambo mipya watakamilisha mwezi wa nane mwaka jana. Jee vipi mitambo aliyoahidi mwaka jana Zantel kwamba wamefunga wamemaliza kuifunga na kama hawajamaliza lini wanategemea kumaliza ili wale wateja waweze kupata huduma kama wanavyoilipia. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti kwanza niseme kwamba Kampuni hii ya Zantel ni Kampuni Binafsi haiendeshwi na Wizara wala haiendeshwi na Serikali na sisi tuna hisa kumi na tano kwa mia kama nilivyosema na kwa kuwa hii ni kampuni binafsi kama kuna mtu hapa anataka kwenda kununua hisa kwenye kampuni hiyo aende akanunuwe.

Ninachotaka kusema ni kwamba tunazungumzia maeneo gani yanayoshughulikiwa na Kampuni ya Zantel ni karibuni Zanzibar nzima wamejenga minara yao kila pahala na wametuhakikishia Wizarani kwamba kwa Unguja na Pemba unaweza ukatumia huduma zao katika maeneo yao yote kama kuna maeneo yana matatizo haya yanatokana na kwamba hivi sasa hivi wanabadilisha mitambo yao kutoka mitambo ile ya zamani ya *third generation* kwenda *fourth generation* na hiyo bado haijakamilika nchi nzima.

Swala hilo jengine nafikiri itabidi na sisi pia kiwizara tukawaulize hawa watu wa Zantel watupatie hasa majibu kamilifu ya kwamba lini watamaliza kufungu hiyo mitambo na tukilipata hilo jibu tutakuleteeni kwa maandishi. Ahsante Mwenyekiti *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti kutokana na hali ya swali hili lilivyo na jawabu yake ilivyo naona kama nitapoteza muda halitokidhi hoja ya swali la msingi naomba kuliondoa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea mbele kuna tangazo wanatangaziwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti wanaombwa wakutane katika ukumbi wa mkutano mara tu baada ya kipindi cha maswali na majibu ambayo yanayofanywa hivi sasa kwa hivyo wajumbe hao wanaruhusiwa kwenda katika kikao cha Kamati ya Bajeti.

Naomba niwatambulishe wageni wetu wa leo.

Waheshimiwa Wajumbe leo hapa ukumbini tuna wageni wa Mhe. Abdalla Ali Kombo, Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe, ni watendaji wa Chama cha Mapinduzi kutoka jimbo hilo. Wageni wenyewe ni kama wafuatao.

1. Ndg. Bakari Iddi Siwamoja - Mwenyekiti wa Tawi la Mwenge
2. Ndg. Kalathami - Magogoni
3. Ndg. Maulid Abdalla Mwinyi - Diwani
4. Ndg. Hassan Abdalla Jaku - Katibu wa Jimbo la Mwanakwerekwe
5. Ndg. Maulid Haji - Mwenyekiti wa Tawi la Mwanakwerekwe C
6. Ndg. Ali Iddi Mbaraka
7. Ndg. Safia Yahya
8. Ndg. Said Khamis na
9. Ndg. Muhammad Hassan Simai

Nasema nyote karibuni katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi. Ahsanteni sana.(*Makofi*).

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2017/2018 – Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea na michangio ya hotuba ya Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira akifuatiwa na Mhe. Masoud Abrahman Masoud ambaye ameomba dakika tano, halafu atafatiwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) ajitayarishe.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii asubuhi hii. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutupa afya njema na kukutana kwenye kikao hiki cha Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira pamoja na watendaji wake wote kuanzia Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Maafisa Wadhamini kutoka Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze moja kwa moja na suala la upatikanaji maji safi na salama hasa katika eneo la Shehia ya Kizimbani. Mhe. Mwenyekiti, Kizimbani ni eneo ambalo sasa hivi limechimbwa visima karibu 10, tumshukuru Mwenyezi Mungu maji yanatoka vizuri na wenzetu maeneo ya Mjini wanafaidika na maji haya safi na salama. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana wananchi wa Shehia ya Kizimbani hawafaidiki na maji haya, sasa nimekuwa na wasi wasi inawezekana isije ikawa kama ule umeme ulipokuja Zanzibar, umeme kwanza ulifikia Fumba lakini kwa bahati mbaya umeme ulichelewa sana kufika Fumba. Sasa na mimi niseme wananchi wangu wa Shehia ya Kizimbani hawafaidiki na haya maji safi na salama. Kwa vile kuna mradi mkubwa sasa hivi *ZAWA* wanao nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja hapa atwambie kati ya vile visima vingi ambavyo vimechimbwa katika Shehia ya Kizimbani

atuhakikishie angalau kisima kimoja kiwe kinafanya kazi kuwapatia maji wananchi wa Shehia ya Kizimbani.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende kwenye uchimbaji wa visima vya Ras-al-Khaimah kwenye Shehia ya Dole. Bahati nzuri niwapongeze *ZAWA* kwa kufikiria kama wananchi wa Shehia ya Dole wana tatizo la maji safi na salama hasa miundombinu imekuwa chakavu na ni ya muda mrefu, sasa hivi maji muda wote mashine inafanya kazi lakini maji kwa wananchi hayafiki.

Mhe. Mwenyekiti, *ZAWA* baada ya kuliona hilo walifikiria kutuchimbia visima viwili vya Ras-al-Khaimah vipo Dole na bahati nzuri wamekuja kujenga tenki zuri sana na mwaka juzi likazinduliwa kwenye Mwenge wa Uhuru. Lakini bahati mbaya mpaka leo utekelezaji bado haujaanza. Mhe. Waziri katika kikao cha bajeti kilichopita alisema hapa kuwa visima 11 vya Ras-al-Khaimah tayari wameshaanza kuvifanyia kazi. Lakini nikamuomba sana kisima cha 12 na 13 vipatiwe mabomba na mashine vile visima vilivyopo Dole ili wananchi wale na wao wapate kufaidika kwa maji safi na salama. Nimuombe sana Mhe. Waziri kwa sababu waziri huyu anatoka kwenye jimbo lile, basi awafikirie sana wananchi wa jimbo lile ili na wao wapate kutatuka na tatizo hili la ambalo sasa hivi limewakabili la muda mrefu sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende kwenye Shirika hili la Umeme. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mkurugenzi pamoja na watendaji wake wote wa Shirika la Umeme kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, maana yake ukitembea sasa hivi Unguja na Pemba maeneo yote utayakuta maguzo ya umeme na mawaya kila pahali unapatikana, ni kazi nzuri ambayo wenzetu wanajitahidi kuifanya. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwenye hili kuna deni kubwa la serikali ambalo linadaiwa, jana hapa lilizungumzwa bilioni 61 na bahati nzuri serikali wamelipa bilioni 1,

tuwapongeze wizara kwa kufanya kazi hiyo nzuri. Mhe. Mwenyekiti, lakini deni hili zaidi tunakuwa nalo sisi wenyewe kama serikali, mawizara ya serikali ndio yanadaiwa pesa nyingi sana na hasa Mamlaka ya Maji (*ZAWA)* ndio inadaiwa pesa nyingi sana. Kwa hiyo, nimuombe tu Mhe. Waziri atakapokuja hapa atwambia ikiwezekana taasisi moja moja ya serikali atuwekee yale madeni ambayo yapo, pengine nusu na robo ya deni hili lililopo la bilioni 61 ni madeni ya serikali wananchi pengine wao wana asilimia ndogo ambayo inaonekana wanadaiwa. Kwa hiyo, nimuombe sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie hilo ili tusiwabebeshe mzigo mkubwa sana hawa Shirika la umeme tukaona hawafanyi kazi vizuri kumbe wanajitahidi isipokuwa hawaonekani jinsi wanavyo…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako ulioniomba umemaliza na ushapata nyongeza.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, kwa haraka haraka nimalizie kwa kusema tu watu wa Mamlaka ya Maji *ZAWA* niliondoka nao nikenda nao katika Shehia ya Mbuzini. Shehia ya Mbuzini kuna tatizo kubwa la maji kwa muda mrefu bahati nzuri nilitembea nao katika eneo la Kwanyanya, pale eneo la Kwanyanya kuna wakulima wanalima kama *irrigation* wanatumia maji ya kisima kile. Niliawomba sana wawafatilie wale wakulima wajue ili yale maji yafungwe katika maeneo haya wananchi wetu wapate maji safi na salama. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa aniambie hatua gani toka kipindi hicho zimechukuliwa mpaka leo kuwa bado wananchi wa eneo la Mbuzini hawapati maji safi na salama.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho niseme kuna hii kadhia ya muda mrefu la hati za wananchi wa Dole ambao walitakiwa wapatiwe hatimiliki za wakulima, nusu wakapata hizo hati na nusu mpaka leo hawajapata. Inasemekana watu wa Idara ya Ardhi hawajapima

yale maeneo ambayo tayari serikali ilitoa ruhusa wapimiwe na wapatiwe hati kwa ajili ya ukulima. Kwa hiyo, na Mhe. Waziri atakapokuja aniambie ni lini atawamalizia wananchi wale waliobakia kupatiwa hatimiliki katika eneo la elimu…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda umemaliza.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, niunge mkono hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa asilimia 99 na asilimia 1 mpaka pale atakaponiahidi kama wananchi wangu wa Kizimbani pamoja na hatimiliki za Dole zitatolewa.

Mhe. Mwenyekiti: Anayefuata ni Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) ajitayarishe.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya wizara hii ambayo imesomwa. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kujaalia uzima leo kusimama katika Baraza lako hili kuweza kuchangia. Bila ya kupoteza muda niende moja kwa moja katika uchangiaji wangu naanza katika ukurasa wa 23, nafikiri ni Idara ya Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, kama unavyofahamu kwa upande wa ardhi imekuwa kilio cha muda mrefu sana, nashukuru Rais wa mwanzo wa nchi hii kwa adhma kabisa ya kuwasaidia Wazanzibari wakwezi na wakulima alithutubu kutoa eka tatu tatu kwa watu kwa ajili ya kilimo na eneo dogo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zao za kuishi. Na sheria bahati nzuri katika mwaka 1992 imekuja kutungwa sheria Nam. 12 ya ardhi, lakini kifungu 24(3) kinasema kila Mzanzibari atamiliki eka tatu kwa ajili ya kilimo na eneo dogo la ujenzi wa kudumu.

Mhe. Mwenyekiti, inakuwaje leo hii imesomwa ripoti hapa kuna watu wana zaidi ya eka 28 wanamiliki, wao nani, kwa sababu gani? Ikumbukwe kama ile ardhi ni ya Wazanzibari sote tuna haki yakumiliki ardhi ile, lakini hata ile sheria haiwaruhusu hawa watu wamiliki ardhi ile. Je, taratibu gani serikali imeweza kuridhia mpaka kuwamilikisha watu wale idadi hii kubwa ya eka hizi 28 na kuendelea au kumi na zaidi.

Ningeomba sana Mhe. Waziri katika suala hilo basi tupate majibu ya kina kwa sababu upande wa ardhi imekuwa kilio, kilio kisichokuwa na msikilizaji. Inasumbua sana baadhi ya watu wakawa juu ya sheria kwamba hizi ambazo tunatunga wenyewe wanazipinda kwa ajili ya maslahi kujikumbizia mali ambazo hawastahiki kuzimiliki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu mali ya ardhi Wazanzibari sote tuna haki kumiliki ardhi, lakini baadhi ya watu wanajifanya wao ma-*hero* kwamba wamemiliki ardhi ile yote hata sasa hivi unashinda hata kupatiwa ardhi au chakusikitisha hata hivyo viwanja basi imekuwa shida waheshimiwa kupatiwa kwa sababu hiyo ardhi inamilikiwa na mapapa wa nchi hii. Ningeomba nizungumze hilo kwa upande wa ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda mbele nizungumzie suala la Mahakama ya Ardhi. Kweli pale Majestic katika jengo letu ipo Mahakama ya Ardhi, kwa kweli lile eneo sio rafiki. Nimeona hapa kuna mpango wa kujenga, ningekuhimiza sana Mhe. Waziri ulifanye haraka iwezekanavyo yaani wale watu pale watoke kwenye lile jumba bovu wahamie kwenye jumba ambalo lina hadhi na ile Mahakama yenyewe, pamoja na kazi kubwa wanayofanya kusimamia unyanganyi usiendelee watu kunyanganywa ardhi zao. Lakini eneo wanalofanyia kazi sio rafiki mwisho hata choo katika jengo lile ni kibovu wanatumia choo cha majirani. Kwa kweli hatuwatendei haki watu wale ambao

wanaofanya kazi katika Mahakama ile ya Ardhi. Ningekuomba sana Mhe. Waziri kwa hilo ulifumbie macho uwaone wale watu haraka waweze kuhama na kuhamia jengo ambalo lenye kulingana na hadhi na heshima ya wale wanaofanya kazi kwenye Mahakama ile ya Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda mbele katika hiyo kifungu 49 Mamlaka ya Maji. Mhe. Mwenyekiti, bado upande wa maji ni changamoto tumeambiwa kwamba asilimia 87 upatikanji wa maji Mjini, bado mimi nasimama pale pale kwenye imani yangu ninachokiamini kwamba bado asilimia 67 iliyozungumzwa upatikanaji wa maji Mjini haiingii kwenye akili yangu kwamba ni sawa. Haiko sawa na nina sababu zangu za kusema.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji imeshindwa kutoa maji kiasi hicho ambacho walichokiandika, pamoja na miradi mingi sana ya nchi hii ya maji kuna *JAICA*, kuna *KONOICA* kuna chungu nzima sijui Ras-al-Khaimah mmetuandikia sasa hivi kuna China. Bado tatizo la maji katika maeneo yetu ni donda ndugu, bila ya viongozi wa majimbo Mbunge na Mwakilishi kuchimba hivi vishimo vidogo vidogo watu wakapata maji nafikiri wananchi wetu wa Zanzibar wangenuka kwa sababu hawana maji.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ipo na kongwe na siku nyingi tu lakini upatikanaji wake au ufanisi wake haupo. Kwa hiyo, mheshimiwa tatizo ni nini? Ukweli usiofichika kama tulivyozungumza katika Wizara ya Afya tunazungumza tena katika wizara yako hii pana matatizo katika Idara yako ya Maji. Haiwezekani Idara ya Maji ile kuna siku mkubwa kenda katika sehemu husika yale maji yanakuwa yanatoka, vyereje baadae akiondoka tu siku ya pili maji yale hayatoki na kuna manung'uniko baadhi ya watendaji wako wanafanya makusudi kuyafunga maji yale ili kuwachonganisha wananchi na serikali yao. Hilo suala lipo, uhakika upo na hata juzi paliulizwa swali

pale na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele kama anajuulikana hasa mtu huyu anafanya kadhia hii, bado mnasema mnasubiri hekima, busara, mheshimiwa hivyo hatuwezi kufika.

Kwa hiyo, ningeomba sana katika hizo hekima zetu na busara zenu mziondowe tuchukue hatua isiwe mtu mmoja akawaudhi watu mia moja wa nchi hii. Mhe. Waziri kwa hilo ningeomba nakuamini dada yangu unaweza kazi, shujaa, shupavu uchukue maamuzi magumu katika hilo, tuachane kila kitu siasa tu. Tuchukue maamuzi magumu ya kuweza kufanya kazi kuwatatulia wananchi wetu matatizo walioyokuwa nayo hususan suala la maji, sio kila wakati mtu atafute chajio, atafute na maji wapi na wapi? Huo muda wa kufanya kazi utakuwepo wapi, ningekuomba sana katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika hilo nitauliza kidogo tu, nataka kujua visima vingapi ambavyo Ras-al-Khaimah wamevichimba na tayari vinafanya kazi. Baada ya hapo kuna visima vya China, je Wachina hawa wamechimba visima vingapi ambavyo tayari vinafanya kazi?

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele katika mchango wangu naingia hapo kwenye jakamoyo la roho, Shirika la Umeme. Mhe. Waziri dada yangu Salama Aboud Talib nimekwambia hivyo kwa sababu unajua namna gani ninavyoumia juu ya maslahi ya wananchi wetu katika nchi hii. Shirika la Umeme kuna mchwa, Shirika la Umeme kuna ubaguzi, Shirika la Umeme kuna uoza na mheshimiwa hilo unalijua, lakini inashangaza mpaka leo hii bado hujachukua hatua. Na imefikwa wakati sasa hivi baadhi ya watendaji wa Shirika la Umeme kupata kichwa kwamba wao hakuna wa kumfanya kitu katika nchi hii, wao ni nani?

Mhe. Mwenyekiti, pale tuna kikundi cha watu tu wanajifanya kama lile shirika ni la kwao, lile shirika ni la serikali sio shirika la

mtu. Kuna baadhi ya watu katika shirika lile wakajiona wao ndio *superior, super power,* ndio wenye maamuzi ya mwisho kundi kubwa la watu wengine hawana thamani wala mchango katika shirika lile. Kwa kweli hatuwatendei haki watu wetu wa Shirika la Umeme. Nilitaka niseme hayo kusudi na nasema kwa uchungu kabisa kwa sababu najua yanayofanyika pale.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuja hapo mwanzo kukwambia kadhia mbali mbali lakini moja kwa moja nakwambia kama Shirika la Umeme linafanya kazi vizuri pamoja na hayo wale watendaji wa chini bado hawapati fursa, stahiki zinazohitajika tofauti na wakubwa wa pale. Juzi tu baadhi ya watendaji Maafisa wamekwenda Pemba watendaji zaidi ya 7, wamekwenda kulipana posho ya 600,000 kwa siku tatu, wa chini unawakata hawalipwi hata posho maana yake nini, wale nani? Mheshimiwa inasikitisha sana kwa sababu hawa wa chini ndio wanaobeba nguzo, ndio ambao wanaokwenda kuvuta mawaya, wanafanya shughuli zote hawa kutwa wanapishana kwenye mara ndege, mara boti kwa kusafiri na kupeana maposho.

Kwa kweli huwatendei haki hivyo ningekuomba sana katika hili uchukulie hatua na si hilo tu kuna suala kadhia nzima wewe mwenyewe ni shahidi nilitoa tangazo la kuuza mafuta ya kuendeshea mashine Pemba yalifika kuuzwa shilingi milioni 600 ikakataliwa hii bei mtu wa chini akazunguka wakakubaliana wauziane milioni 200 na mpaka *voice mail* unayo, lakini chakusitisha mpaka leo umeshindwa kuchukua hatua. Watu wanapatana ili wakubaliane wana mpango wa rushwa wapewe milioni 50 ili waweze kuwaachia. Mheshimiwa hatuitendei Zanzibar tuone sisi leo mko mbele mnaisimamia serikali lakini ikawa mnashindwa kuchukua hatua katika serikali na hamuwatendei haki wa Zanzibari wa nchi hii walio wengi.

Mhe. Mwenyekiti, si hilo tu katika shirika lile juzi tu hapa walikaa bila ya kufata taratibu za *procurement* wamenunua gari kwa zaidi ya shilingi milioni 140 bila ya *tender board*, bila ya chochote. Na bahati nzuri Mwenyezi Mungu ile gari kailani imeshapata ajali juzi, gari ya milioni 140 wameamua tu wao wenyewe na hawaulizwi *untouchable*. Nasikitika sana na sana zaidi ya sana hili shirika la serikali kwamba kama kuna watu basi wana mikono yao wakubwa mtuachie ili lile shirika lifanye kazi kwa ufanisi. Mnatwambia habari ya deni…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Maulid Diwani zungumza na kiti usizungumze na waziri.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Nashukuru kwa uchungu kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna watu wako juu ya sheria wanajiamulia wanavyotaka, leo hii unamuondoa mtu ukumbini unamuweka chumbani hatuwezi kufika. Mhe. Mwenyekiti, si hilo kuna deni la *ZECO* ambalo linapigiwa kelele mara unaambiwa bilioni 21, mara bilioni 65 na jana tunaambiwa milioni sitini na moja na laki nane. Kwa kweli ni kizungumkuti nitakuomba sana mheshimiwa utakapokuja unaambie deni halisi la Zanzibar linalodaiwa na *ZECO* ni kiasi gani, na hili deni linalipwa vipi, na hili deni limeanza lini kwa sababu nina taarifa za kutosha kabisa, deni hili limeanza baada ya 2006 kuanzia mwezi wa 8. Kwa sababu bili iliyoletwa pale 2006 mwezi wa saba ni zero *balance* kutoka *TANESCO* badala ya Tanzania kusamehewa madeni na wakati huo Waziri wa Fedha alikuwa Mhe. Zakiya Meghji, kipindi kilichofatia imekuja deni *zero balance*. Lakini humu tunaambiwa deni hilo limeanza zamani, inasikitisha sana sijui kulikoni hapa na hata kwamba inalipwa zaidi ya shilingi bilioni tano ina maana miezi 13 ingekuwa lishakwisha hili deni lakini mpaka leo bado hamna linaloendelea.

Mhe. Mwenyekiti, na si hilo tu shirika lile linapondwa juu ya kadhia nzima ya matumizi mabaya ya fedha za nchi hii. Mhe. Mwenyekiti, shirika lile karibuni limenunua *transformer* zaidi ya 12 kwa kila transfoma moja ni milioni 25, hizo *transformer* ziko ndani hazitumiki, kwa sababu baadhi ya watu wa *procurement* na baadhi ya watendaji wa pale kutegemea *ten percent* wamezinunua *transformer* ambazo hazina

matumizi yake. Na isitoshe wameshatoa zabuni nyengine kununua transfoma 74. Jamani wapi tunakwenda halafu huku mnasema kuna deni, huku mnanunua magari, huku kuna hivi inasikitisha sana. Na si hilo Shirika la Umeme hilo hilo wamenunua waya wa *neutral* wa kufungia mita zao ambao waya ule ni wa *3 phase* ambapo waya unaofungiwa mita za TUKUZA ni *single phase* ambao ni waya maalum mtu hawezi kuiba. Katika kudhibiti maibaji yale leo hii maroli mwa maroli yako katika Shirika la Umeme yamewekwa hayatumiki, pesa kiasi gani zimetumika.

Kama tulivyozungumza mwazo Mnazo Mmoja kubovu huku ndio kumeoza kwa sababu baadhi ya wakubwa hukubeba ukweli usiofichika. Shirika la Umeme kuna baadhi ya wakubwa inavyosemekana kwamba wana mikono yao. Sasa sijui nani Mhe. Waziri utakuja kunambia au vipi imebidi mimi niseme huo ndio ukweli uliokuwepo. Lakini si hivyo, tu Shirika hilo hilo la Umeme pamoja na yote hayo imeweza kutengeneza kikundi hicho cha hao watu wa *procurement* hao kama bwana hujawaahidi wao *ten per cent* yao wewe huwezi kupata kazi katika shirika lile tumeona tumegundua tenda mbali mbali zinapatiwa watu na hawakidhi vigezo vigezo, wanapatiwa mapesa watu wanapiga pesa zao juu kwa juu huduma pale mbovu. Inapelekwa *rope hole* pale hata *cape* ya juu haina mtu unafungiwa, *rope hole* nyengine unaambiwa ukanunue mwenyewe mjini ili uweze kukamilisha kazi yao.

Na si hivyo, tu kuna watu wa Tunguu wanaojenga nyumba zao wanaotaka kulipa umeme kule wanaambiwa lazima walipe laki tano *ZECO Fees* Mhe. Waziri tutafika. *ZECO Fees* hii una taarifa nayo hii kwamba lazima watu walipe shilingi laki tano ndio wavutiwe umeme wakati nguzo pale ipo. Sasa sijui taratibu gani mpya zilizokuwepo hizo wa kuunganishwa umeme mpaka zifikie hizo.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana zaidi ya sana kwa uoza ulioko pale Shirika la Umeme bila ya kufanya maamuzi magumu hili deni litakuwa kelele tu halishi siku zote pale pana ubadhirifu tunaokwenda chungu nzima kuwaonewa wafanyakazi wetu wa chini, wao wafanyakazi wakubwa wakajilimbikizia mamali ambapo kitu ambacho sio halali.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuja hapa katika kipindi kilichopita nilizungumzia juu ya kadhia nzima ya wafanyakazi 67 ambao waliokuwa nje ya mkataba na malipo ya mafanyakazi ambaye kastaafu kafanya kazi zaidi ya miaka 25 kalipwa milioni mbili Shirika la Umeme hili karatasi hii hapa ninayo ya malipo, Mhe. Mwenyekiti, ushahidi huu hapa upo naomba sijui atakuja kunipa jibu gani ni hawa ambao alinambia kwamba watakapostaafu pesa zao zile zitaingizwa katika Mfuko wa Kustaafu, huyu bwana kastaafu mnyonge wa Mungu kafanya kazi zaidi ya miaka 25 pale kalipwa milioni mbili Shirika la Umeme hilo hilo. Sasa kwa kweli kuna manyago ya kutosha.

Kuna suala la *bonus* lilianza 2014 Shirika hilo la Umeme kila mfanyakazi alikuwa anapokea si chini ya shilingi laki moja naa hivi juzi tu imesimamishwa hapa kwa sababu nasikia kwamba mna mzigo mkubwa wa deni mnasaidia namna gani. Lakini nataka kujua *bonus* ile yote ni kiasi gani ambayo iliyokuwa inatoka kwa wafanyakazi wale wa Shirika la Umeme. Ningeomba sana Mhe. Waziri katika hicho Shirika la Umeme panahitaji uangalizi wa hali ya juu kwa sababu si pahali pazuri kwetu sie. Najua nikisema hivyo, nitachukiwa lakini ukweli utabaki ukweli tunajenga nchi lazima tuseme ukweli.

Shirika la Umeme lina Mwanasheria Mkuu kesi ngapi kasimamia Shirika lile limeweza kushinda. Limewakatia mita au limewangolea mita zaidi ya mita 300 ambao wananchi waliokuwa wanaiba umeme. Kazi yao ni kupeleka Mahakamani aisamamie

ende mahakamani ashitakiwe ili alipe pesa shirika lipate. Lakini hamna liwalo imekuwa unatoka kwenye Mwanasheria Mkuu unakwenda kufanya kazi za *procurement* na masuala mengine ambayo siyo ya kwako, imefika hatua hata kuwapeleka mafundi wetu wahusika mnawapeleka Maafisa Habari mnawapeleka Korea kwenda kutafuta waya, *engineer* hakuna. Nilitaka niseme hayo kwa moyo safi kwa kweli Mhe. Waziri uka kazi kubwa sana na lakini kama hilo utalifumbia macho hilo suala la Shirika la Umeme basi mtakusikitikia sana kwa sababu pengine hata hiyo nafasi pengine uliokuwa nayo wewe watakuwa hawakutendei haki.

Ningekuomba sana Mhe. Waziri unatakiwa ujikaze kiume tupambane kuona ile kadhia pale iliyokuwepo Shirika la Umeme inaondoka. Shirika la Umeme ni sehemu moja mbovu afadhali haya hiyo Mnazi Mmoja....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika nne.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mheshimiwa kwa hizo dakika zangu nne ulizonipa nafikiri kwa kweli nasema kwa uchungu kabisa tuendee, siwezi kuendelea. Ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako hili tukufu kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa bajeti yake ya mwaka 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa wizara hii kwa kazi kubwa wanayofanya hasa tukizingatia kwamba ina sekta muhimu juu maisha ya binaadamu. Suala kubwa la kuangalia hapa Maji, Nishati ya Umeme, Mazingira yetu, Ardhi mambo manne yote

Mheshimiwa ni uhai wa nchi hii na usalama kwa wananchi wetu. Bila ya kuwa na mambo hayo maendeleo ya nchi na kuishi kwake kunakuwa mashaka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazangumzia mamlaka ya maji *ZAWA*. Mamlaka ya Maji ina jukumu zito katika nchi hii kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata maji na wanaondokana na usumbufu ambao unawakabili siku hadi siku. Lakini kwa bahati nzuri au mbaya Mamlaka ya Maji inajitahidi kufanya kazi zake lakini naona inafikia pahala wakati mwengine wanakwama sijui kwa kitu gani. Mamlaka ya maji katika taasisi ambayo inapata misaada mikubwa katika nchi hii nafikiri ndio peke yake mabilioni kwa mabilioni yanapatikana kutafuta maji katika maeneo mbali mbali. Lakini maji hayo bado ni shida na hata kipindu pindu katika Mkoa wetu wa Mji Magharabi hasa Wilaya zetu za Magharibi A na B ndio kunako kadhia kubwa sana ya kukosa maji na kunywa maji machafu na kupata kipindu pindu. Naiomba sana wizara kupitia Mamlaka ya Maji ijitahidi kufanya kazi zake kwa ufasaha na kwa uangalifu ili kujua kwamba maji ni uhai na bila ya maji hatuwezi kuishi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mradi wa Ras al Khaimah, mimi niipongeze serikali kwa juhudi zake. Lakini pia nasikitika kwamba kuna visima 150 hadi leo Mhe. Mwenyekiti, tuna visima vichache ambavyo vinafanyakazi. Visima vimechimbwa lakini havina kazi yoyote vinavyofanya. Kwa Unguja tuna visima 10 kwa Pemba kuna visima 9 hiyo ni changamoto nzuri lakini kwa visima 150 hatukufikia pahala.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa upande wangu wa Jimbo la Kijito Upele nazungumzia kwanza visima vya Ras el haimah ninavyo viwili kwa vitatu, ninacho kisima Tomondo ninacho kisima Kijito Upele hivi vimekaa, vimekosa *pump* tu na kwa bahati nzuri Mamlaka ya Maji hao hao kwani wakifanya vizuri mimi

napongeza tu wamechimba kisima kikubwa hapa Taveta Magirisi lakini mpaka leo kimekaa kimetulia. Niwaambie au nawaomba sana visima vitatu hivi cha Magirisi, Tomondo Uzi na Kijito Upele pamoja na Kwarara kisima tulochimba Mbunge na Mwakilishi kama vitatiwa *pump* na kusambaza maji tatizo la maji katika Jimbo langu la Kijito Upele itakuwa historia katika maisha yetu, hayo mabilioni sijui ya India sijui ya wapi wala yasifike. Huu mradi tunaogaiwa gaiwa tu wangevipatia *pump* visima hivi wakatoa kila kitu na mabomba na kila kitu tatizo la maji litabakia historia katika eneo langu.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, katika mradi huu wa Ras al Khaimah Mwanakwerekwe C pana kisima kikubwa kimechimbwa na tuliona kwamba kisima hichi kingepata mashine nzuri kubwa inayokidhi haja basi tatizo la maji pia lingekuwa historia. Lakini hadi leo Mhe. Mwenyekiti, la kushangaza imewekwa *pump* ndogo maji baada ya nyumba sita au nane hakizidi. Mimi naona wizara ilifatilie na kikaangaliwe kisima kile kwamba kipo kimekaa lakini *pump* iliyowekwa pale haistahili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika Jimbo langu la Kijito Upele maana kwanza mtu analilia kwao nina kisima kile pale cha Kijito Upele kisima kile naipongeza wizara namupongeza Mbunge aliepita Mhe. Shereweji na pia nampongeza Mhe. Shamsi Vuai Nahodha wakati huo Mwakilishi sasa hivi Mbunge kilifanyiwa ukarabati mkubwa halikadhalika na mambo mengine yalitokea maji yakawa yanapatikana lakini yalikuwa yanachukuliwa kwa magari.

Nimpongeze sana Mhe. Waziri Mamlaka ya Maji kisima kile ilikuwa kwa maeneo ya Taveta, Meli nne Uzi yalikuwa hayapatikani kabisa kwa muda wote. Lakini baada ya kusema kwamba kisima kile kiachwe maji yakachukuliwe Msikiti Mabuluu huko ndiko kulikoelekezwa magari ya maji

wakachukuwe kule wauze maji kwa asilimia kubwa yanapatikana saa 24 na wananchi wameridhika. Mimi ombi langu tu kwamba tuzidishe bidii katika visima hivi nilivyovitaja na visima vinne hivi kama tutaviunganisha *pump* leo tatizo la maji litaondoka kwa muda mrefu na kipindu pindu kitatuondoka katika maeneo yetu.

Nashangaa Mheshimiwa hadi leo visima hivi vimekaa hatujui hatima yake vipi. Naiomba serikali kupitia wizara haya masuala ya visima kuchimba papo kwa papo ni hatari katika mji wetu. Lakini kama vinapatikana visima vikubwa vya kudumu basi tatizo hili la usalama pia litakuwepo.

Baadhi ya visima vinavyochimbwa vinachimbwa katika maeneo hatarishi siku za mafuriko zinaingia maji ndani visima na wananchi hawana la kufanya. Niiombe sana wizara kupitia Mamlaka ya Maji hili lisimamiwe vizuri juu ya kunusuru wananchi wetu na maradhi ya kipindu pindu la mlipuko yanayokea mwaka hadi mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza tena Mamlaka ya Maji kwa juhudi yake hiyo, lakini nawapongeza kwa kufatilia mambo mbali mbali. Lakini niwaombe tu naomba tena leo katika Baraza hili mimi katika Wilaya yetu ya Magharibi "B" tuna majimbo 7. Majimbo 7 haya kama tunakwenda kwenye mgao basi ningeomba kama ifuatavyo:

Tupatiwe mfanyakazi wa kudumu katika majimbo haya, jimbo moja baada ya jengine litakuwa ngumu, lakini Kijito Upele, Mwanakwerekwe, Pangawe tuambiwe nyie likitokezea tatizo lolote saa 24 mtafuteni fulani, halafu na wengine vile vile waliobakia huko Dimani, Chukwani yaani majimbo ya karibu karibu yaani tukenda hivyo Mheshimiwa mafanikio yatapatikana, Kiembesamaki. Chukwani pamoja na Dimani, tuweke *zone* zetu tunajua linatokea tatizo tunamkamata fundi fulani. Niwaombe

tunawaambia Mamlaka ya Maji tunapokwenda wasiwe na hasira sisi tunakaa na wananchi shida tunazijua sisi kuliko wao.

Lakini pia Mheshimiwa nakuja Shirika la Umeme. Mhe. Mwenyekiti, mimi kawaida yangu Mheshimiwa nitasema kweli daima uongo kwangu mwiko. Nawapongeza kwa asilimia moja au hata zaidi kama ipo. Shirika la Umeme wanafanyakazi nzuri wanafanya kazi kwa bidii wanafanyakazi ya jihadi, maana kama mimi niliepitia mwanajeshi najiona kama niko katika lindo nalinda na silaha yangu na yeye anakwenda pahala pamekatika umeme anakwenda kusambaza umeme hatari anayo yeye mikononi mwake hajali mvua hajali jua. Shirika la Umeme Mheshimiwa nalisemea mimi nawapongeza kwa asilimia mia moja wanafanyakazi nzuri.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2016/17 kuna vijiji 47 jamani hii sijui niseme nini vijiji 47 Unguja viko 20 na Pemba viko 27 tuwaambie nini kama ingelikuwa Mamlaka ya Maji visima hivyo 57 tuko mbali sasa hivi katika majimbo mbali mbali. Lakini tunakwenda hatua baada ya hatua. Nimuombe sana Mhe. Waziri awasaidie, awaelekeze, awasimamie lakini Shirika la Umeme ndio roho bila ya umeme hatupati maji, bila ya umeme hatuna raha. Kwa hivyo mimi nawapongeza kwa asilimia mia moja na nawaomba tu wenzangu tuangalie tu huku huku wenzetu hawa wanafanyakazi nzito na wanafanyakazi ngumu wakati mwengine wanakwenda katika mazingira hayastahiki wewe mwenyewe unakimbia. Mimi nasema nawapongeza, nawapongeza kwa asilimia zangu hizo.(*Makofi*).

Jengine zuri tu nilisema siku moja hapa watu hawakunielewa. Lakini nasema ndivyo ilivyo, Mhe. Mwenyekiti, umeme umefika kwa Mhe. Haji Omer Kheir Tumbatu katika kisiwa, umefika Kisiwa Panza, umefika sijui Mtambwe kwetu kwa wakwe zangu. Leo kwa nini hapa Kwarara Madina hakuna umeme na sikusema

kwa nia mbaya nimesema hali halisi kwa sababu Sera ya Chama cha Afro Shirazi na CCM Zanzibar nzima ipate umeme katika nchi na katika visiwa vidogo vidogo. Kwa hivyo naipongeza sana serikali na nalipongeza Shirika la Umeme kwa kutekeleza adhma hiyo. Lakini nawapongeza zaidi Madina leo Mhe. Mwenyekiti, wanang'ara wanafanyakazi zao vizuri televisheni wanaona na mambo mengineyo huo ndio ulimwengu wa leo.

Nampongeza Waziri baada ya kumwambia tu tukafuatilia lakini nampongeza Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme na watendaji wake umeme umefika kwa wakati, watu hawana maneno washindwe wenyewe kuunga. Lakini naomba tu kuna baadhi ya wadanganyifu katika Shirika la Umeme, kuna baadhi ya watendaji wadanganyifu wanaosema mimi afisa fulani nakwenda pale sijui Meneja Mkuu baada ya yeye ndie mimi unataka umeme pesa zako nipe mimi, hili linaathiri shirika na linapata jina baya. Niwaombe watu wanaohusika kama wale hatua za kisheria zichukuliwe ili lisiendee shirika letu kusemwa kwa vibaya.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ardhi jana katika hotuba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati alitoa kauli nzito, mimi naiunga mkono Kamati suala la ardhi kwa asilimia mia moja. Lakini nitaiunga mkono hotuba hii yote lakini maamuzi ya Kamati na maelekezo yake naiunga mkono kamati. Nafikiri kiswahili changu kimeeleweka sina tatizo yote naunga mkono.

Mhe. Mwenyekiti, suala la *ZURA* niipongeze serikali kwa kuona kwamba pana haja sasa hivi ya kuweka *ZURA* twende katika suala letu bei za umeme, bei za maji, petroli na mambo mengineyo. Bahati nzuri au mbaya *ZURA* nasema inafanyakazi zake vizuri. Lakini mamlaka zile zinazohusika kidogo huwa hazifatilii au hazihusiki kuangalia pana kitu gani au pana kosa gani. *ZURA* toka kuwekwa tunashukuru Mheshimiwa mafuta kwa kipindi kirefu

hatuombi itokee hayajapungua nchini kwetu wanasimamia vizuri na wanakwenda vizuri.

Lakini pia na wenye masheli wamewekewa mikakati kwamba lazima sheli iwe *standard* hiyo ndio inavyotakiwa kimataifa bidhaa ile kubwa wafanyakazi bila ya kipaa kile cha juu wanaumia afya zao zinaathirika jua na mvua. Kwa hivyo, hiyo naipongeza *ZURA* kwa kuelekeza hilo ili kwenda vizuri na katika hali ya ulimwengu ilivyo. Lakini bahati katika upangaji wa bei hilo pia sina matatizo nalo. Nawaomba tu *ZURA* wawe wakali wakati wa kupanda bei ya mafuta siku hiyo hiyo itabadilishwa, utaambiwa baada ya dakika tano mafuta hamna watu wanafanya marekebisho. Lakini wakati wa kushuka sasa panakuwa na matatizo, ndio ule watu wanasema "Mchongoma kupanda rahisi kuushuka una kazi". Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri kupitia *ZURA* yetu ambayo ni nzuri mafuta yanaposhuka bei wawe haraka haraka wayashushe ili wananchi wapate faida.

Mhe. Mwenyekiti, suala langu la mwisho katika wizara hii nitalisemea kwa ufupi kabisa. Mamlaka ya Maji wameweka mpango mzuri wa mita zetu. Narudia tena ndio la mwisho hili na mita hizi walizoziweka zina manufaa kwa wananchi wetu kujielewa, lakini bahati mbaya sasa hivi wananchi wengi wanalalamika hasa upande wa Makadara, wanatumia *zone* ya Makadara wanasema kwamba bili wanazopelekewa zinakuwa kubwa sana. Ilikuwa wanategemea shilingi 4,000, shilingi 6,000 mpaka shilingi 8,000 inategemea matumizi ya mtu. Lakini mtu anaweza kupelekewa shilingi 25,000, shilingi 30,000 au shilingi 18,000 na maji yenyewe yanaeleweka yanaweza kukaa kutwa ukapata mara moja hupati tena. Kwa hivyo, naiomba Mamlaka ya Maji ikaangalie labda kuna kitu gani katika mita zao ili wananchi wetu wasiwe na kasoro ya kuilalamikia Mamlaka ya Maji.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naiomba Mamlaka ya Maji Visima vya Tomondo, Kwarara, Taveta Magirisi pamoja na Kijitoupele twende tukaangalie tupate mashine wawafungie wananchi wetu wapate maji waondokane na usumbufu huu.

Baada ya hayo machache mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Lile agizo la kamati walilolitoa na mimi nikiwa chini ya Mwenyekiti wa Wenyeviti nitasikiliza taarifa ile pale itakapotolewa sina pingamizi na wao. Lakini kwa jumla naunga mkono kwa asilimia mia moja ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata kwa mchango wako. Naomba nimwite Mhe. Machano Othman Said kwa dharura kama nilivyosema aendelee na baadae Mhe. Mussa ajitayarishe.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuwa mchangiaji wa Wizara hii ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Pia naomba nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba viumbe kwa kutuwezesha kuja hapa leo siku ya Jumanne kuchangia bajeti hii. Aidha, niwashukuru sana watendaji na viongozi wa wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wamekabidhiwa wananchi na watendaji kazi wao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitozuwia kifungu chochote katika wizara hii na naiunga mkono bajeti hii, mchango wangu mkubwa utakuwa katika kuuliza na mashauri. Mchango wa kwanza. Kwanza tutambuwe kwamba wizara hii inajenga au inabeba mahitaji na matumaini ya watu wa Zanzibar. Sehemu zake zote hata hili jina lake Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Haya

mambo manne yote ni muhimu katika ustawi wa wananchi wa Zanzibar. Kwa hivyo, ni wajibu wa Waheshimiwa Wawakilishi kutoa maoni yao, kukosoa lakini pia kuielekeza serikali jambo gani lifanyike katika kuhudumia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niende kwenye maji. Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi walizungumza sana tatizo la maji na kwa bahati nzuri katika hotuba hii ya Mhe. Waziri kazungumzia juhudi za serikali katika upatikanaji wa maji safi na salama. Lakini na mimi kama nilivyouliza juzi suala la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri kwamba ningependa sana Mhe. Waziri akija kesho atuarifu kuanzia mwaka 2000 mpaka mwaka 2017 ni fedha kiasi gani au miradi ya aina gani ambayo serikali kwa fedha zake na fedha za wafadhili ikiwemo mikopo na misaada kama *JICA*, China, Japan na ule Ras Al Khaimah na sasa wa India imepatikana na kutumika na hali ya maji ikoje.

Mhe. Mwenyekiti, sisi ambao tuna majimbo tunawawakilisha wananchi tunahisi kwamba bado asilimia ambayo inazungumzwa kwamba maji yanapatikana hayapatikani. Kwa hivyo, nafikiri ni wakati sahihi tuelezwe kiwango cha fedha na hali halisi ya maji. Lakini pia Mhe. Waziri naomba nikueleze kwamba kwa kupitia kwa Mhe. Mwenyekiti, kwamba sisi wananchi wa Jimbo la Mfenesini bado tuna tatizo la maji na ni matumaini yetu kwamba kutokana na serikali ilivyotuambia kwamba mradi ukija wa China sisi tutakuwemo basi tunatarajia kwamba Jimbo la Mfenesini litafaidika sana na mradi wa India.

Lakini kuna jambo moja naomba tu nikueleze Mhe. Waziri kwa kupitia Mhe. Mwenyekiti, kwamba kama miezi minne au mitano nyuma mamlaka baada ya kilio chetu ilikwenda kuangalia uhalisia wa matangi ya maji ya Kama. Yapo matangi mawili kule, kuna tangi jipya na la zamani, lakini yote hayafanyikazi vizuri, na

mamlaka ilianza kuyafanyia ukarabati lakini kazi ile imesita na kuleta kero kubwa kwa wananchi wa Shehia kama ya Kama, Mfenesini, Chuini na baadhi ya Shehia kwa sababu hakuna matangi ya kusaidia maji.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri tunaomba hili nalo na ningependa sana Mhe. Waziri ama Naibu Waziri baada ya kumalizika kikao cha Baraza la Wawakilishi cha msimu huu basi tufanye ziara ya kutembelea jimbo langu lote kuangalia matatizo ya maji na ikiwezekana na umeme.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kuhusu maji pia tunavyo visima vya Ras Al Khaimah katika jimbo letu ambavyo vimechimbwa, lakini ufanisi wake bado ni mdogo na vyengine vimechimbwa katikati ya maziwa ya maji ambavyo baada ya masika haya nafikiri hata alama ya visima itakuwa haipo tena. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ni matarajio yangu kwamba utatusaidia ili tuweze kufanikiwa katika suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoka katika suala la maji nije katika suala la umeme. Mimi kwanza niwapongeze Shirika la Umeme pamoja na kasoro zilizokuwepo katika shirika. Nafikiri serikali itatumia mkono wake kuzirekebisha kasoro hizi. Lakini mimi nitoe ushauri kwamba pengine muda au wakati umefika kwa serikali kuangalia uwezekano wa kuwa na mamlaka au taasisi ya kushughulikia umeme vijijini. Wenzetu Tanzania Bara wanao *REA* na inasaidia sana kwa kweli kupeleka umeme vijijini. Sasa hivi hapa kwetu Zanzibar Shirika la Umeme kwa jumla ni la kuuza umeme na kupokea umeme, lakini tunapolipa na kazi ya kuweka miundombinu ya umeme, kwa kweli kazi inakuwa kubwa na hatimae tunakua hatutambui. Hii kazi ya kuweka miundombinu ya umeme ni ya Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge au ya Shirika la Umeme maana yake kazi zimezongana.

Mhe. Mwenyekiti, tunajua kwamba ipo asilimia 2 inaitwa ya miundombinu katika kila mnunuzi wa umeme, kila ukinunua umeme na pengine tungeambiwa pengine kwa miaka miwili hii iliyopita tumepata kiasi gani kutokana na asilimia 2 ile ya kununulia umeme. Kwa hivyo, ushauri wangu ni kwamba serikali ifikirie kuanzisha taasisi ambayo itashughulika na uwekaji wa miundombinu ya umeme zaidi kwenye maeneo yetu ya vijijini, kwa sababu hili litasaidia sana kupunguza mzigo kwa Shirika la Umeme na wao kufanyakazi halisi ya usambazaji na uuzaji wa umeme badala ya kuwa wao pia ni wawekaji wa miundombinu katika maeneo mbali mbali ya vijiji.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, katika Shirika la Umeme pia niombe kwamba kwa bahati nzuri serikali imeugawa Mkoa wa Mjini/Magharibi katika Wilaya sasa hivi ziko wilaya tatu. Kuna Wilaya ya Mjini, kuna Wilaya ya Magharibi A na B. Ukiangalia Wilaya ya Mjini wana vituo vya kununulia umeme visivyopungua vitatu. Kuna Michenzani, kuna Malindi na kuna Gulioni. Wilaya ya Magharibi B wana vituo viwili Mazizini na Mwanakwerekwe pale. Lakini Magharibi A hakuna kituo cha kununulia umeme.

Kwa hivyo, mimi nashauri na kuwaomba waangalie sana pale kwenye eneo la Chuini Kwa Nyanya waweke kituo cha kununulia umeme hata kama kontena la kisasa la kileo, na kwa bahati nzuri eneo lile tayari, kwa habari nilizonazo tayari wanataka kuwapa Halmashauri ya Magharibi A Manispaa ya Magharibi A. Kwa hivyo, wao watangulie Shirika la Umeme kuweka kituo kwa ajili ya wanunuzi wa umeme wa Wilaya mpya ya Magharibi A itatusaidia sana msongamano wa kuja mjini kununua umeme. Wakati mwengine mtu anataka kununua umeme wa shilingi 5,000 anatakiwa aende mjini akanunuwe umeme arudi tena Mwakaje, Mwachealale au Bubwisudi hii inakuwa kidogo shida Mhe. Waziri. Kwa hivyo, tunaomba utufikirie sana na uwashauri Shirika la Umeme waangalie hata kwa muda kwanza kwa

kontena, baadae Manispaa ikijenga pale wawe na eneo la kudumu la kununulia umeme.

Mhe. Mwenyekiti, niishukuru serikali nataka kumalizia kwa mambo mawili ya mwisho. Kwanza kuishukuru serikali kwa kuamua kwamba eneo lile la Chuini kwa kupitia Mipango Miji kulipima na kuwakabishi Manispaa A ili liweze kuliendeleza na shughuli zake za maendeleo.

Lakini la mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, nirejee kwenye maji. Mhe. Mwenyekiti, maji, elimu, afya na kilimo ni vitu ambavyo kila wakati vipo kwa wananchi. Pengine Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yupo hili angelichukua kidogo akatusaidia elimu tayari imegatuliwa kwenda kwa wananchi, afya tayari imegatuliwa kwenda kwa wananchi na kilimo nacho kinagatuliwa kwenda kwa wananchi, inabakia maji. Mimi nafikiria haya matumizi makubwa ya fedha kwenye maji na ikawa sote tunalalamika nafikiri kwa tatizo hilo. Hebu na sisi Zanzibar tuangalie uwezekano wa kugatua shughuli za maji ziende katika halmashauri zetu, ili kila wilaya au kila manispaa au kila halmashauri waweze kujua kama wamepata bilioni 10 za maji zinatumika vipi, maji yanapatikana wapi na wapi kutakuwa na kasoro za maji. Suala hili linaweza kutusaidia kupunguza tatizo la maji Zanzibar. Kwa hivyo, mimi nashauri pengine mwaka huu haimo katika ugatuzi, lakini serikali nzima ione kwamba na maji nayo yanastahiki kwenda kwenye ugatuzi ili kupunguza matatizo na malalamiko ya maji ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana baada ya kunipa dakika zao hizo na mimi naunga mkono bajeti hii ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Machano Othman. Sasa naomba nimwite Mhe. Mussa Foum Mussa, na baadae atafuatiwa na Mhe. Simai Mohammed Said ajitayarishe.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuchangia. Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake wote kwa kazi zao nzuri wanazozifanya katika serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo na mimi vile vile nizungumzie habari ya Shirika la Umeme. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuwa na azma ya udhabiti kwa visiwa vyote vya Unguja na Pemba kuvipatia umeme. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, na mimi vile vile katika jimbo langu ninacho kisiwa kimoja kinaitwa Kisiwa cha Shamiani, hiki nadhani nacho kimeshapatiwa umeme kwa sababu katika kipindi cha sherehe za Mapinduzi za mwaka huu ulikwenda kuzinduliwa. Kwa hivyo, naipongeza serikali kwa jitihada yake hiyo kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo vile vile na mimi nielezee kwamba katika jimbo langu shehia zote zimefika umeme. Lakini kuna baadhi ya vijiji bado havijafikishiwa umeme. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Afisa Mdhamini wa Wizara Pemba. Mhe. Mwenyekiti, hawa wamefika katika jimbo langu na tukatembea sehemu ambazo kuwa bado hazijapata umeme.

Mhe. Waziri aliniahidi kwamba vijiji hivyo navyo vitafikishiwa umeme. Kwa hivyo, nampongeza kwa maelezo yake, isipokuwa nimesema tu kwamba suala hili nilielezee kwa sababu Mhe. Waziri katika maelezo yake alieleza kwamba katika kazi

zitakazofanywa na shirika hili ni kusambaza umeme katika sehemu mbali mbali, lakini hakuzitaja tu zile sehemu ambazo zitapelekewa umeme. Lakini nimesema kwamba na mimi nizungumzie zaidi ili kuweka katika *Hansard* vizuri.

Vile vile nataka nimkumbushe Mhe. Waziri katika swali langu nililopeleka katika kikao kilichopita, naomba ninukuu majibu yake. Majibu yake yalikuj hivi;

"Napenda ifahamike kwamba ahadi zote anazozitoa Mhe. Rais ni utekelezaji wa ilani ya uchaguzi katika kipindi husika, miongoni mwa sera kuu za serikali ni kuwapatia huduma za kijamii wananchi wa Zanzibar popote walipo, ikiwemo huduma hii ya umeme. Utekelezaji wa ahadi za sera hizo hufuata mipango ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu hutegemea na aina ya mradi husika. Aidha, vijiji alivyoviainisha

Mhe. Mwakilishi katika swali lake. Napenda kumfahamisha kuwa vijiji hivyo vimo katika mpango wa wizara yangu wa usambazaji umeme vijijini, kwa m waka ujao wa fedha 2017/2018. Vijiji vyenyewe hivyo ni kama hivi ifuatavyo.

Kijiji cha Kitondooni, Mtamba, Mtakafu, Mchakwe Kaskazini na Mchakwe Kusini".

Nadhani Mhe. Waziri vijiji hivi tumevitembelea mimi na wewe. Kwa hivyo, bado nakueleza kwamba katika jitihada zako zote naomba hivi vijiji visije kusahauliwa kwa sababu vimo katika ahadi ya Mhe. Rais wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo vile vile nasema kwama Shirika la Umeme linajitahidi kufanya kazi. Lakini katika sifa wakati mwengine na hila zipo. Mhe. Mwenyekiti, mimi naishauri serikali kwa kupitia Shirika la Umeme, kwanza wafanye

utafiti juu ya umeme wanaoungiwa umeme huko vijijini kuna mashaka. Kwanza kuna wafanyakazi wengine wa Shirika la Umeme wanafanyakazi zao kibinafsi ndani ya Shirika la Umeme.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile huko vijijini kuna mambo wakati mwengine ni mazito. Inawezekana wakati mwengine ukakuta nyumba ina umeme ilihali bado haijaungiwa umeme. Sasa naliomba shirika lifanye utafiti kwa hali ya juu ili kuondosha hizi kasoro, kwa sababu kuna mtu anatumia umeme lakini halipi na kuna mwenziwe analipa. Hapa pana matatizo kidogo. Hili suala la kuwa mfanyakazi anafanyakazi zake yaani kazi za Shirika la Umeme ilihali ziko nje na mapato yanakwenda mikononi mwake. Sasa na haya tunayoyazungumza yafanyiwe utafiti vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo sasa nizungumzie suala la maji. Niipongeze serikali kwa jitihada ya kuwaletea wananchi huduma ya maji. Nataka niseme Mhe. Mwenyekiti, lakini kwanza nimpongeze tena Mhe. Waziri, kwa sababu tuna matatizo pale Kendwa kulikuwa kuna matatizo ya kisima, kisima chetu kilizidiwa na Mhe. Waziri alipokuja tulikitembelea kisima hicho. Mhe. Rais alipofanya uzinduzi wa barabara ya Kiwani, Mgagadu, wananchi wa kule walimuomba kwamba kile kisima kiunganishwe na kisima cha pili ili ile nguvu iwe kubwa zaidi, kwa hivyo Mhe. Rais alikubali na Mhe. Waziri kalisimamia hili na kazi ya pale imeendelea vizuri iko katika hatua za kumalizia. Kwa hivyo nampongeza Mhe. Waziri kwa jitihada yake hii kubwa.

Lakini vile vile nasema kwamba bado katika Shehia yangu ya Chole tuna matatizo ya maji bado maji hayajafika yaliwahi kufika mabomba lakini maji hayapatikani, na hapa tulipokwenda na Mhe. Waziri aliniahidi kwamba kuna kisima Kengeja kitapeleka maji Chole lakini hili suala bado halijaanza, namueleza tu Mhe. Waziri

na hili alisimamie kwa sababu tatizo la maji Chole ni kubwa mno watu hawapati maji kwa muda mrefu sana.

Vile vile Shehia ya Mtangani nayo kuna tatizo la maji lakini kule kuna mfuko wa Mbunge nadhani kuna utaratibu wa kuchimba kisima ili kuhakikisha kwamba na Shehiya ya Mtangani inapata maji kikamilifu, yakitendeka hayo yote niliyoyaeleza basi na sisi wana jimbo la Kiwani tutakuwa tumefaidika vizuri na suala la maji.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo vile vile nichangie katika ukurasa wa tisa hapa Program ndogo ya Uratibu na Uendeshaji wa Shughuli za Wizara Pemba. Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017 Wizara Pemba ilikuwa na mambo ya kuyafuatilia na mambo mengine ya kuyatekeleza, katika mambo waliyoyapanga hapa ni jumla ya mambo 8 lakini mimi nataka nizungumzia hili jambo la mwisho la nane, nambari ya kirumi hii inazungumza kufanya ziara ya ukaguzi wa maeneo ya uwekezaji, Micheweni na maeneo ya utalii Makangale, Kiweni, Muambe na Vitongoji.

Kwanza nataka niseme kwamba naipongeza Wizara kupitia Pemba lakini nataka niseme kwamba sijui ziara hii kule Kiweni Mwambe imefanyika au laa, kwa sababu mimi kama Muwakilishi sikuwa na taarifa sijui Masheha hili suala wanalijua. Sasa naomba tu kwa mara nyengine ikifanyika basi na sisi kama wahusika wakuu wa majimbo tupewe taarifa kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, huko chini kuna mambo makubwa, tatizo la ardhi limekuwa kubwa na watu wanapata malalamiko sana, na mimi tatizo la ardhi katika Jimbo letu la Kiwani limenikumba sana. Kwa hivyo nataka niseme kwamba Mhe. Waziri mtakapokuwa mnafanya ziara kutembelea katika majimbo yetu, katika shehiya zetu na sisi kama Wajumbe wa Baraa la Wawakilishi mutuelekezee kwa sababu mimi binafsi nimeambiwa nimeuza ardhi sasa wananchi wanataka waambiwe ukweli kwamba je hili suala ni kweli au laa.

Mhe. Mwenyekiti, nimezungumzwa kwamba nimeuza ardhi Kuji, nimeuza ardhi Kiweni, nimeuza ardhi Kachunge sasa mngelinishirikisha wakati ule mnapokuja basi wananchi wangefahamu je hili suala ni kweli au laa, sasa nakuombeni Mhe. Waziri hii ziara ikiwa ilifanyia wakati huo au haikufanyika basi ufanye kwa makusudi ili uje tupite hayo maeneo niliyoyazungumza na wananchi siku hiyo basi angalau wale masheha na viongozi wao wajumbe wao kumi kumi wale basi wawepo ili waelezwe. Ikiwa kuuza nani aliyeuza ajulikane hapa ndio tutajua ukweli upi na uwongo ni upi, lakini hii kujipandisha huku tu juu viongozi wetu hamteremki chini likajulikana suala la ukweli ni upi hii ijtajenge fahamu mbaya wananchi wetu kwa sababu kuna wananchi waliamini kwamba mimi nimeuza ardhi. Ilihali sina habari nalo hilo suala wala hio sehemu nyengine zinazozungumzwa mimi uhai wangu wote sijawahi hata kufika, sasa sijui mtu huuza kitu ambachokuwa sio chake sijui atauza vipi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niendelee kuipongeza Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwanza na mimi nataka niseme kwamba suala la ardhi limekuwa zito, mapendekezo waliyoyatoa Kamati basi tunaomba hilo suala lishughulikiwe na iundwe hiyo Kamati teule kwa sababu itakapoundwa hii kamati sisi wawakilishi tunapoishauri Serikali tunakuwa na nia safi ya kuisaidia, baadae kusaidia wananchi wetu suala la ardhi limekuwa zito. (*Makofi*).

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi ni hayo tu niliyoyazungumza, mimi sina nia ya kuwa nizuie kifungu lakini namuomba tu Mhe. Waziri atakapokuja basi anipe maelezo mazuri ili nijenge matumaini zaidi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kiwani, baada ya maelezo hayo mimi naunga mkono kwa asilimia mia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mussa sasa nimuite Mhe. Simai Mohammed Said na Mhe. Jaku Hashim Ayoub ajitayarishe.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutupa uhai leo kuweza kufika hapa lakini pia nikushukuru wewe pia kwa kuweza kuniona na kupata nafasi. Pia nianze kwa kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Serikali yake yote kwa kazi nzuri wanayoifanya, lakini pia nimpongeze Mhe. Wziri kwa hotuba yake aliyoisoma kwa haraka, lakini pia tumeweza kumsikia vizuri kwa *speed* nzuri kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii mimi leo nitaanza kwa kuzungumza maeneo mawili la kwanza nimekwenda kwenye *Hansard* yangu kuiangalia ya mwaka jana naona kama nitakuwa najirudia rudia mambo mengi ambayo nimezungumza mwaka huu. Lakini nianze juu ya suala la kwanza la Ramani ya Zanzibar mwaka jana nilizungumzia suala la ramani ya Zanzibar juu ya mabadiliko ya tabia nchi lakini pia juu ya *land reclamation* inayofanyika Mtoni kwamba kisiwa cha Zanzibar sasa ramani yake haitakuwa ipo kama Zamani, nataka kujua ramani ya Zanzibar sasa hivi ukiingalia katika mitandao na katika *Google* haipo sawa na hali halisi. Sasa je ramani yetu lini tutaipata kama ilivyo hata maskulini waweze kutambua ramani ya Zanzibar sasa hivi ni hii hilo la kwanza.

Lakini suala la pili masikitiko yangu ambayo nilikuwa nasoma gazeti la Zanzibar leo la jana wakati nasoma gazeti la Zanzibar leo ambalo ni gazeti la Serikali Waziri apiga *stop* mpango wa utoaji ardhi ndani ya hifadhi ya taifa, Mhe. Mwenyekiti, Ngezi ni eneo la hifadhi lakini urithi wa Wazanzibari Watanzania na Dunia, lakini pia ni urithi unaotambulika maeneo mengi. Lakini

ukiangalia humu ndani inasemekana kutokana na hii taarifa iliyoandikwa kwenye magazeti watu kutoka Wizara ya Ardhi wanataka kwenda kupima eneo la hifadhi ya Ngezi na wanataka kupima ekari 400, lakini mbali ya ekari 400 baya zaidi wamekwenda usiku kuweka *beacon* hili gazeti la Serikali sio mimi na naomba ninukuu hapa inasema hivi.

Inasema "Kutokana na kuwa walinzi wetu kuwa kidogo watu wa Idara ya Ardhi walivizia siku ambayo walinzi walikuwa hawapo tena katika hii sehemu maana walikuwa jioni na kuweka *beacon* zao usiku ili kufuata walikuja mapema kukamilisha kazi yao" alieleza Salim mimi simjui Salim nani.

Lakini sambamba na hilo juu ukirudi inasema, "amri ya kuondolewa kwa *beacon* hizo ilitolewa na Waziri wa Wizara hiyo Hamad Rashid Mohammed wakati alipofanya ziara kutembelea eneo hilo, lakini zaidi inasema ndani naye mtaalam wa Misitu Pemba Salim Mohammed Said alisema eneo lote la msitu wa Ngezi ni ekari 2900, lakini Idara ya Ardhi tayari walikuwa wameshapima ekari zisizopungua 400 kwa ajili ya kupewa muwekezaji". Hili ni gazeti la Serikali au la Zanzibar la SMZ.

Hivi ndani ya Serikali Mawaziri wetu huyu mmoja anayekaa hapa mbele yangu na yule kule Waziri wetu anayekaa kule wa Serikali wanagongana kiasi kama hicho mpaka tunaishia kama hapa, Waziri mmoja anatoa agizo la kuzuia mwengine anasema twende tukapime eneo tena la *Reserve* hii kwa kweli ni aibu tunamtia Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tukisema tutaambiwa wabaya lakini leo huu mtego ni wakwenu wenyewe kwa sababu hili gazeti ni la Serikali.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nitoe taarifa kuhusu msitu wa Ngezi, kwanza katika eneo la Ngezi kuna eneo pia la mrithi la Mjaja Mpwani ambae kwa wakati huo Mhe. Waziri wa Kilimo alikuwa

Mhe. Mohammed Aboud Mohammed alitoa agizo juu ya malalamiko yao wapatiwe eneo lao na karatasi ninazo hizi hapa, moja ambao warithi hii ni katika nakala ambazo wamekwenda anaema hii imeandikwa na Mohammed Aboud Mohammed Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, inasema Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais sasa inakuwasilishia rasmi suala hilo kuwa wananchi hao wapimiwe shamba lao na kupewa hati yao ili wapate haki yao kama uamuzi wa Mahakama ulivyoelekeza. Isipokuwa tu tuhakikishe kuwa upimaji huo usihusishe eneo la Kambi ya Jeshi la Kujenga Uchumi na eneo la Hifadhi ya Msitu iliyopimwa na Serikali.

Sasa inakuwaje Wizara ya Ardhi inataka kuwapatia eneo la hifadhi muwekezaji mimi naomba sana Kamati ya Mhe. Hamza iingilie mara moja ifuatilie suala hili juu ya hifadhi na tupate wala hatuhitaji kamati teule, mimi naamini Kamati ya Mhe. Hamza ni watu makini watupatie taarifa kama kuna migongano juu ya Mawaziri wawili hilo ni la kwao, lakini suala la kulinda hifadhi ni yetu sisi sote na Baraza la Wawakilishi ambayo ni urithi wa Wazanzibari na Watanzania na watu wote duniani.(*Makofi*).

Mhe. Mweyekiti, baada ya hapo sasa naomba nitoe ushauri juu ya suala jengine suala la *Land Transfer Board.* Mheshimiwa unapotaka kwenda kukopa pesa benki huwa wanahitaji nyaraka tofauti, sasa napenda kujua Mhe. Waziri ni watu wangapi wamepatiwa hati kutoka *Land Transfer Board hapa* Zanzibar, lakini pia kuhusu sheria ya *Condominium Act* mwaka 2010 hii sheria kwa kweli ilikuwa ilete neema kwa Zanzibar lakini bado inaelekea haieleweki iko watu wengi na wawekezaji. Mimi nilikuwa nataka kufahamu ni utaratibu upi unaotumika baina ya Serikali yetu na Wizara husika kuweza kuitangaza sheria hii ili Wazanzibar na wawekezaji na pia Shirika letu hili la *ZIPA* waweze kuonesha kwamba tayari watu wanaijua ili tuweze kuona

neema kwamba hii Sheria inafanya kazi ili iweze kuingiza mapato kwa ajili ya Serikali na wananchi wetu.

Lakini pia Mhe.Mwenyekiti, nataka niende suala la *ZURA* kwanza natoa pongezi zangu naungana na Mhe. Shihata mambo yamekuwa mazuri, mafuta na Gesi hayaadimiki bei tunaona wanakwenda vizuri na hata katika mambo yao (CSR)*Corporate social responsibility* wamekuwa ni wamekuwa ni wazuri, lakini katika suala la mafuta na gesi kwa mujibu wa sheria, nilikuwa naangalia jana sheria ya mafuta na gesi ya *Petroleum Agreement* inasema kwamba *Petroleum Agreement Means Between the Government National Oil Company Contractor Related the Petroleum Licenses Area*. Sasa Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia sasa hivi kwa utaratibu tunaokwenda tunaanza sasa kujipanga sisi wenyewe katika masuala mbali mbali juu ya utaalam hasa katika mafuta na gesi, mimi naomba sana katika maeneo ambayo utaalam tunahitaji kusoma hizi *Seismic waves* wanazozifanya kusoma data, na ukenda katika kifungu cha 43(i) kinasema hivi "*Not With Standing the Right of a Permit Holder, Company and the Authority or Petroleum data Generated Under this act shall be owned by the Government, the Authority may in a prescribed manner authorized the permit holder and company to use the data referred to a subsection one of this section after the agreement.*

Mhe. Mwenyekiti, *technology* inabadilika kila siku mimi naomba sana Mhe. Waziri hawa watu ambao sasa hivi Mkurugenzi wetu ambae ameshateuliwa na nitoe pongezi kwa Mhe. Rais juu ya *Zanzibar Petroleum Development Corporation* panapotokea mikutano ya kimataifa ili kuweza kutambua na kuweza kuzisoma hizi data hasa za *Seismic waves* tusione tabu kugharimu pesa kuwapeleka kwenda kusoma na kushiriki mikutano wape pesa waende kila mkutano na kila elimu wanapohitaji tuweze kujua na *data* zetu tuweze kuzifahamu. Mhe. Waziri pale unapoona pana

faida basi usione tabu kutoka kuwaambia Wazanzibari na uwe *transparent* kuwaambia suala la mafuta na Gesi tumefikia wapi, kuna matumaini makubwa sana katika Serikali ya awamu iliyopita wapo wengine humu ndani Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliongea utafikiria mafuta na gesi yanakwenda kuchimbwa kesho, kutokana na hilo tuliwachanganya wananchi wetu wengi sana.

Mimi naomba sana elimu izidi kutolewa na ikiwezekana katika skuli za Serikali na vyuo vyetu wazidi kueleweshwa kwamba huu ni mpango tunaaza juu ya *Oil and Gas Industry* na tutachukua muda, haitakuwa leo au kesho kwa hivyo ni muhimu suala hili likafahamika vizuri Mhe. Mwenyekiti, na watu wakajipanga vizuri na watu wetu wazidi kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mhe. Waziri Ukurasa wa 21 kifungu cha 40 (iv) anasema hivi. "Mpango mkuu wa matumizi ya ardhi unaelekea kuifanya Tunguu kuwa eneo la makaazi, biashara na huduma ikiwemo Gereji, magari ya mawe, yadi ya magari na nyenginezo kwa kufanikisha lengo hilo Idara imejipanga upya eneo hilo na kulifanyia malengo hayo". Mimi nataka kuuliza Serikali hivi mimi wanataka waning'oe hawa 2020 kwa makusudi, mbona nafanyiwa mambo ya maajabu ajabu, maana yake naletewa watu viwanja vinatolewa lakini barabara hazitengenezwi, umeme haupelekwi, maji hayatandikwi mimi nabakia kutandikwa kwenye vyombo vya habari na mawio kila siku, mimi sina uwezo wa kupeleka bomba za maji na umeme hii ni kazi ya Serikali, mimi kazi yangu ni kufika hapa kuwasemeya.(*Makofi*).

Leo nimetandikwa na watu wa Kikungwi kwenye mawio hawana umeme, mwaka jana kwenye *Hansard* nimezungumza hapa na Serikali ikasema inafuatilia na *Hansard* yangu ninayo hapa nimezungumza nikasema juu ya kijiji cha Kikungwi pamoja na

Unguja Ukuu masuala ya maji, lakini leo narudia haya haya Serikali imeniahidi hapa itasimamia masuala ya kupeleka umeme Unguja Kikungwi Uwandani pamoja na Tunguu upande wa Kibele na kwenye kitabu imetajwa, lakini viwanja vinapimwa Tunguu wananchi wanapewa maji hakuna, ardhi iliyokuwepo wanasogezwa watu sasa mimi nifanye nini. Mimi naomba hata hii ardhi kama mna mpango wa kuwapa Waheshimiwa mimi sitaki chukueni nyinyi lakini mimi nataka wananchi wangu wapate maji na umeme, sasa isifike pahala nikamwambia Waziri labda yeye hana uchungu pengine hana jimbo sisi wenye majimbo tuna uchungu kwa sababu tunalalamikiwa wananchi wetu kila siku maji maji maji, umeme umeme umeme kila siku kwa wiki unatandikwa simu.

Sasa mimi naomba neno moja suala la maji kama ni *Priority* basi Waziri ajipange vizuri katika sehemu zote na maeneo yote, ukiangalia kwenye kitabu huwezi kujua maeneo gani mwaka huu Serikali itaniunga mkono ili na mimi nijipange, tunaambiwa Serikali imejipanga mikakati mizuri tangi la Unguja Ukuu linavuja utafikiria mfereji wa mvua sasa hivi pampu inapigwa kupeleka maji Unguja Ukuu, Uzi kisiwa kizima hawapati maji utafanyaje, tangi lile lina gharama yake zaidi ya paundi laki mbili na limeanza kuvuja. Sasa Serikali lazima ijipange kununua tangi jipya na sisi kama kuna sehemu ya kuchangia tuko tayari, Unguja Ukuu maji hayafiki, Kikungwi maji hayafiki, Tindini maji hayafiki sasa maeneo yote haya watu walioipigia kura Chama cha Mapinduzi na wao ndio walioahidiwa.(*Makofi*).

Ng'ambwa ukichimba kisima chini unapata maji ya chunvi kwa hivyo wanategemea bomba la maji lifike kule, maeneo ya Dunga, Binguni, Tunguu watu hawajawahi kuona maji kwenye bomba yakitoka la mfereji, lakini maji Tunguu hiyo hiyo ardhi zinapimwa lakini maji hayatoki. Sasa mimi Mheshimiwa naomba sana katika hizi wadi zote na maeneo yote Serikali ijipange ili

tuhakikishe haya mambo yanakua na mimi naomba sana Mhe. Waziri tulifanya ziara pamoja samahani kidogo Mhe. Waziri Gavu ananisumbua tu huyu!

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli katika suala la umeme na suala la maji wadi ya Ubago pamoja na eneo la Dunga hasa sehemu ya Dunga Kinyongo Mhe. Mwenyekiti yapo maeneo tunaweza kufanya mpango mzuri kwasababu visima vipo vile vya Ras el Khaimah na vilivyochimbwa nyuma, tunaweza tukajipanga tukawapelekea maji wananchi wetu tatizo moja maafisa ambao waliokuwepo wa maji a mkakati pamoja na ofisi moja kwa moja na *ZAWA* hakuna mpango maalum wa kutushirikisha sisi. Mimi naomba moja kwa moja Mhe. Waziri uingilie kati Naibu Waziri amefanya ziara anaelewa lakini lakini suala la maji hadi leo jimboni kwangu hakuna *improvement* yoyote. Na haya ndio masikitiko yangu na taasisi za Serikali na vyuo na maeneo yote Ofisi za Chama, Mkoa lakini jimboni kwangu maji hayatoki maeneo mengi.

Sasa maji mnayachukua mjini vijijini mnayapeleka mjini lakini huko yanapotoka kwenye vyanzo vyenyewe wenyewe hawapati, hasa hili ni tatizo mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti kwa huruma kabisa mwaka jana niliwasema naendelea hapa naomba sasa mwaka huu maeneo yangu Tunguu pamoja na Kikungwi na Dunga haya maeneo ambayo watu wamekipigia kura wanakipenda Chama cha Mapinduzi, basi katika utaratibu huu na paipu za maji tuweke mpango maalum tuhakikishe maji yanakuwa.

Mhe. Mwenyekiti baada ya kuongea suala hilo la maji, nataka nizungumze kuhusu umeme. Mhe. Mwenyekiti umeme wa Zanzibar mahitaji yetu yanazidi kuongezeka kila siku, *cheba* iliyokuwepo 100KV tunashukuru katika ile *missile challenge corporation* Wamarekani wametusaidia lakini matumizi yetu

yanazidi kuongezeka. Mimi naamini katika saa 12:00 jioni mpaka saa 4:00 za usiku sasa tutakuwa tushafikia karibu ya 65 ambayo ni 65 *megawatts*, ambayo waja wetu huu uwezo wake ni *megawatts* 100, sasa mimi nataka nizungumze katika suala hili mpango mkuu wa Serikali tunapoenda na jinsi uwekezaji unapofanyika wa haraka haraka tutafikaje sisi huko mbele je, tukifika mwaka 2020 na mahitaji yanaongezeka kuna *project* ya nyumba za *real state* kuna Mbweni kuna upande wa Fumba na upande wa Kaskazini hasa *demand* ikiongezeka na lazima tuhakikishe na *supply* inakuwa ya kutosha mimi nashauri Mhe. Mwenyekiti mahoteli ambayo yanatumia tutafute njia ya kuhakikisha kama wao wanatumia upande wa *solar*.

Hizi *garden light* tutafute njia utaratibu tuwalete watu kutoka China kampuni za binafsi tutoe *test exemption* tuwaunganishe ili angalau kwenye masuala ya taa wao wanatumia *teknolojia* ya *solar* kwa muda maalum tusiwalazimishe. Lakini tuwa-*encourage* tukifanya hivyo angalau waya wetu huu tutaweza ku-sustain kutokana na *demand* tunayokwenda nayo kwa miaka ya mbele, Lakini pia ule waya wa zamani ambao ulikuwa ukitumia 45 *megawatts* ambao kwa sasa unafika *capacity* ya 40 nataka kujua je, unafanyiwa *services* ya kutosha pamoja na majenereta ambayo ni *becar power 25 megawatts* yaliyokuwepo mtoni sijui nikipita pale naona sasa yanaanza kama kuota ota kutu kwa nje. Lakini je yanawashwa na kuzima yanafanyiwa *service* ya kutosha na endapo panapotokezea fault yoyote tunaweza kuhakikisha tutapata kuweza kutumia yale majenereta bila ya tatizo lolote.

Mhe. Mwenyekiti nataka niongelee sasa katika huu mpango mzima wa Serikali kwenye mambo ya maji na ardhi na maeneo tofauti. Mhe. Mwenyekiti mimi kwa kweli nikirudi huko nyuma kama nilivyosema mwanzo majimbo ambayo yanaotoka kutoka nje ya mji hasa katika masuala ya maji, tuna ahadi nyingi tumezitoa na mimi muda wangu huu ninaoutumia sasa hivi nataka

nimwambie Mhe. Waziri suala la maji ni mtihani mtihani mtihani, mimi namuomba sana Mhe. Mwenyekiti Waziri atakapokuja katika maeneo ambayo nimeyazungumza ambapo Naibu Waziri wake tumefanya ziara pamoja na akanambia tutashirikiana kwa pamoja na Serikali.

Hakuna mpango hadi leo, ulofanywa nikaletewa naomba nipatiwe taarifa kamili na hapa nitapokwenda kwa sababu sitaki kufika pahala kwenye mabuti tutabana banana huko huko, mimi nataka nielewe suala la umeme pamoja na namuomba sana upande wa Kikungwi Uwandani, Kikungwi Uwandani ambao hawa ndio wanaonishughulikia kwenye redio kwenye mawiyo, sasa ahadi ambazo tayari Serikali wao wamezitowa lakini dandana na mateke napigwa mimi hasa tujue tunawataka wapi tuunganishe nguvu huko Kikungwi Uwandani ili tuweze kutimiza.

Mhe. Mwenyekiti baada ya muda wako kutumia kwa uzuri kabisa nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kunipa niseme kwamba naunga hoja asilimia 50 nikasubiri maelezo ya kina kutoka kwa Mhe. Waziri juu ya suala la maji na umeme katika jimboni kwangu ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Simai Mohammed, Mhe. Jaku, Mhe. Mohamed Said (Dimwa) ajitayarishe pamoja na Mhe. Ali Khamis Bakari.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti mimi nianze na maneno ya Katibu Mkuu wangu wa Chama Mhe. Abrahman Kinana. Siku ya tarehe 12 Machi alisema *"*dhulma tuiseme ili wananchi wasionewe", vile vile *"*mazuri tuyaseme nayo tusisite kuyasimamia maovu wakati huu na hatimae tutahukumiwa kusema kweli ni mpenzi wa Mwenyezi Mungu", haya maneno alizungumza saa 6.40 katika Mkutano Maalum. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitakuwa sijamfanyia haki Mhe. Waziri

kama katika kuna waziri ukampigia simu akipokea mmoja ni huyu, “mnyonge mnyongeni haki yake mpeni” na “msema kweli mpenzi wa Mwenye ezi Mungu” tofauti na Mawaziri wengine na kama yuko kwenye kikao basi simu yake anakurudishia. *(Makofi)*

Mhe. Salama nakupongeza kwa dhati kwa hilo na Mawaziri wengine na Manaibu Waziri wengine na Makatibu Wakuu na Wakurugenzi fuateni nyayo za Bibi huyu dada yangu, ‘‘msema kweli mpenzi wa Mwenyezi Mungu” hapa hatukuja kumkomoa mtu wala hatuna nia ya kutaka kumkomowa mtu mimi ilipokuwa hoja ya umeme kipindi kile walifikiri labda nataka kumuonea, lakini hoja ilikuwa sahihi na iko wazi na wala hakitaki tochi lakini ni ukweli Mheshimiwa hilo nikupongeze nitakuwa sijakufanyia haki, yuko kwenye kikao akatoka anakwambia kwamba sema shida yako na huu ndio uungwana na nitakuwa sijakufanyia haki Katibu Mkuu wako vile vile, Mhe. Al Khalil Mirzan kwa umaki wake nimpongoze kwa hilo.*(Makofi)*

Lakini yote haya kama sikumshukuru Mhe. Hamza Mwenyekiti wa Kamati hii kwa umakini wake wa hali ya juu, jemedari Hamza Hassan Juma na kuna msemo “mtama mkukuu dawa” “mtama mkukuu dawa” imekuwa tunapata darasa kutoka kwake Mhe. Hamza mtu mzima huyu na uzowefu wake unasaidia, hotuba yake imejaa kila kitu maana yake Mhe. Hamza nikupongeze kwa hilo lakini mimi nitaanza na ilani ya Chama cha Mapinduzi ndo mchango wangu. Nitaanza na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuhusu maji, hebu Mhe. Waziri miye nataka nifahamu watu wa Michamvi wamekosa nini kwenye Serikali hii, narudia tena tena na tena tokea dunia kuanzwa mpaka leo hii maji hayo hayajafika nini tatizo, sababu gani Mheshimiwa kila mwakilishi Waziri hapa utapata shida sana kunako sekta ya maji ndo kile nilichosema Mhe. Balozi tusaidie wewe ndie boss wetu humu ndani.

Hii wizara inataka Katibu mwengine Al Khalil peke yake hatoiweza au mtuweke Waziri wa Maji tu peke yake hoja yote humu Muakilishi atakaposimama atagusa maji nankubaliane na kitabu cha Mwenye ezi Mungu, *"waja aina minal mai kulla syai'in hayyin"* na tumejaalia kila kitu kinapata uhai kutokana na maji mimi nisingezaliwa bila ya maji, leo watu wa Michamvi wanafikiria nini wakifanye usiku watoto skuli, wengine wanaweza kukosa kwa suala la maji kwa sababu ya milioni 300 au 250. Kuna wawekezaji kule mimi siwalaumu watu wa Mamlaka ya Maji nitawaonea lakini kama kule ile shilingi mia ilokwenda katika Mfuko wa Barabara sasa iyondoke, yende kwenye Mamlaka ya Maji (ZAWA) hizo barabara zinaweza zikapitika lakini kama hawa wananchi barabara ya kazi gani nchi hii. *(Makofi)*

Kila mwakilishi hapa mwenye jimbo nna hakika suala la maji limemgusa, na hii Mhe. Mwenyekiti, Mheshimiwa ninukuu Mheshimiwa Maneno ya Nape "Mhe. Naibu Spika, ilani ya Uchaguzi inatengenezwa na Chama cha Mapinduzi na ndio mkataba wetu kati ya CCM na wananchi, tusipotekeleza wananchi hawataturudisha na huu ndio ukweli kwa sababu tuliwaahidi katika kampeni zetu. Tanzania nzima kilio chetu cha maji si maneno yangu hayo Mhe. Mwenyekiti, suala la maji ni uhai wa kila mtu leo Kibonde Mzungu wanakosa maji nawao. Kila mmoja atainuka lakini nataka kusema sababu gani watu wa Michamvi mpaka leo mwaka jana hata gari moja la maji halikupelekwa.

Hivi sasa huko Michamvi najua mie shida niliyokuwa nayo, leo ramadhani ya kumi na moja wamepelekea vigari viwili baada ya kumuomba Mhe. Waziri juzi vigapelekwa vigari viwili, watu wale vigari viwili vitawafanya nini, vigari viwili vitafanya nini. Hebu nambieni yahe ni yale maneno nilikuwa nilonukuu Mhe. Katibu wa Mkuu wa Chama tutahukumiwa na tuliahidi katika ilani kule na baya zaidi sijui kama wamenitia hasara watu wa Mamlaka ya

Maji (ZAWA) walinambia nichimbe msingi kule nikauchimba kwa gharama chungu nzima, mradi wa maji ya chumvi nikaambiwa angalau watapata wananchi, niliambiwa miezi mitatu sita mwaka wa pili na unakwenda zake. *(Makofi)*

Si milioni 1,000,000 sio 2,000,000 sio 3,000,000 gari moja shilingi elfu 60,000 napeleka mie kule Mhe. Waziri, kisima kimechimbwa na Ras al Khaimah hebu tuwafikirie hawa watu Ilani ya Chama cha Mapinduzi itafika lini kwa vitendo kule baada ya kuisikia kwenye vitabu tu, wamekosa nini watu wa Michamvi katika Serikali hii jamaa. Mpeni heshima, Waziri aliyekuweko Ikulu na Rais aliahidi na agizo la Rais litekelezwe alipokuwa akimnadi Mhe. Issa Ussi Gavu Chwaka nakumbuka vizuri mie akaahidi kiasi kikubwa cha maji, Ras al Khaimah watu wa Michamvi wanaumia hasa wakina mama suala la maji linawasumbua sana, na maji sio biashara hapa Mhe. Waziri nafikiri kila bajeti, kila mwakilishi atagusa suala la maji huu mradi tuliambiwa pesa za India umefikia wapi, mtihani mkubwa huu maji ni msingi wa binaadamu, maji ni haki ya binaadamu, hawa watoto wa Michamvi baada ya *time* ya kwenda skuli wanashindwa wakati mwengine kwenda kutafuta maji kwenda kuyasaka maji muda wote unapotea kwa maji.

Gari moja 60,000 miye Mwakilishi nitafanya mangapi. Juzi pampu ya Bwejuu Waziri nilikwambia kahangaika nani, pesa zimetoka mfukoni na mimi mfuko wa jimbo mpaka leo sijapewa mpaka leo mfuko wa jimbo sijapewa, nitafanya mangapi mimi wananchi wamenichaguwa kuja kusema matatizo yao ndo maana chombo cha Wawakilishi, sio mtatuzi maji, dawa, barabara suala hili tutawaonea Mamlaka ya Maji (ZAWA). Kuna mtoto anaitwa Zahor huyo jawabu hakosi za kukupa, wala siwezi kumlaumu ndio siasa lakini kweli Mamlaka ya Maji imekuwa na matatizo sio matatizo uwezo wao ni mdogo. Lleo pampu moja iungue, hapa sijui kama kuna hakiba kule. Suala la maji Mhe. Waziri hili

litatusumbua sana na litakwenda kutufunga kama nilivyosema tuliahidi hii Ilani Mheshimiwa ukurasa wa 77 kuendelea kuimarisha usambazaji wa huduma za maji safi na salama kwa wananchi kutoka asilimia 87 kwa mwaka 2015 hadi asilimia 97 kwa mwaka 2020, mjini kutoka asilimia 70 na mwaka 2015 hadi asilimia 85 kamati ya vijijini, vijijini ikiwemo Michamvi kijiji, leo mpaka leo wanasikia tu Ilani tu kwenye vitabu kwa vitendo haijafika.

Mheshimiwa nije kunako sekta ya ardhi, Kamisheni ya Ardhi. Mhe. Waziri mimi hapa kidogo nikuombe sana hati za ardhi muda mrefu. Mhe. Mohammed Aboud hayupo hapa naye Mohammed Aboud aanze kuandika nimwambia suala tumepitisha Kamisheni Ardhi leo zaidi ya miaka mitatu, toka kupitisha Kamisheni ya Ardhi miaka mitatu hati ile Mhe. Waziri mnyonge anamsomesha mwanawe anakwenda kukopea Benki hati ile ile, hati ile ni biashara ndiyo inayomkombowa mwananchi, hebu tueleze sababu gani hati hizo zinachapishwa *spelling* moja moja a, b, c, d hazijesha, si uungwana huu, hii ndiyo mkombozi hati ya ardhi Mhe. Waziri hili la muda mrefu tumepitisha Kamisheni ya Ardhi humu miaka mitatu karibu hakuna chochote kinachoendelea.

Sasa wananchi watatuelewa vipi, kila siku kesho tuko mbioni hizo mbio sijui zinaanzia wapi zinamalizia wapi, kipindi kile alikuwa Mhe. Ramadhan Shaaban nilimuuliza suala mimi hapa hati kutoka hapa chini mpaka juu ya meza pamefunika nilimuliza kama huna kalamu nikuletee ya kusaini hati. Ndio baadae zikatoka kipindi kile hati ziko juu ya meza wananchi wanaumia, hati ile unaweza ukafanya biashara kuuzia mandaazi, chapati kwa hati ile kwenda kukopa ni mkombozi wa mnyonge hati ile suala la hati Mhe. Waziri wanyonge hawafanyiwi haki, lakini kuna suala *lease.* Mheshimiwa mtu ananunua shamba kama Makunduchi milioni mia moja leo *lease* unam-*charge dollar 650,* aah hii ni haramu

dhambi kubwa shamba kainunua ingawa mnasema ardhi ni mali ya Serikali lakini shamba kanunua milioni mia moja halafu huwezi kumkamua *lease ZRB* aah hili kalifikirie Mhe. Waziri sana. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Waziri mie nataka unifahamishe kuna Serikali gapi hapa Zanzibar, kuna Serikali ngapi Mhe. Waziri. Kuna mtu mfano keshapita hatua zote nilimwambia Mwanasheria Mkuu hizi kesi nyengine ziangalie Serikali itakuja kula hasara hapa, mimi nimshukuru sana Mhe. Balozi kwa umakini wake kwa kufuatilia na akauliza ilikuaje tukafika hatua kama hii. Mtu kishapewa hati keshapewa vibali keshafika pahali kasha *invest* anatoka mtu tu *somewhere,* Mkurugenzi hapa hapaelekei kitu kiko wazi hakitaki hata tochi leo utakuja kula hasara Serikali kuambiwa yasoelekea vibali kila kitu *ZIPA*, Halmashauri, Mazingira yashafanyika kila kitu, tena muekezaji mzalendo tulia tu Mwanasheria Mkuu haya yanakuhusu vile vile, tulia tu Mwanasheria Mkuu haya ndo niliyokwambia Serikali ishauri vizuri tulia tu Mwanasheria Mkuu tulia tu utakuja kujibu atakuja kujibu mimi nauliza kuna Serikali ngapi humu ndani. *(Makofi)*

Serikali mtaitia hasara halafu mtakuja kusema mahakamani ati tunaonewa, kumbe uwezo wenu mdogo. Nilichosema hapa nilikuu maneno ya Katibu Mkuu tutafika wapi, kama Serikali ndo ilotowa sehemu leo unataka kumdhulumu sijui tunachokifanya kitu cha ajabu kitu gani. Au mzalendo hana haki nchi hii semeni kama mzalendo hana haki nchi hii, hii hapa hebu njoo uchukue umpelekee Mhe. Waziri aone vielelezo pale, maana utahoji ujenge hoja akaangalie nini kimekosewa humo uje unihukumu mimi Mhe. Waziri, tufanya mambo si ajabu Mhe. mimi niombe nikuombe ni-*declare interest* kwa suala hili, anatoka mtu tu, hii kusoma sana Mhe. Mwenyekiti ukaitwa daktari hata mimi siku moja nilipewa hospitali mie, daktari alikuwepo mmoja Muyuni kazidiwa na kazi akanambia Jaku wafunge dawa wenziwe hawa,

nikapewa kituo, mimi nikawapiga buluu wote wale, kuna dawa inatiwa kwenye chupa ukatia buluu mmoja mmoja nikawa natia lile gozi, nikaitwa daktari siku ya pili yake, mimi nikaitwa daktari Jaku. *(Makofi).*

Sasa kusoma kwako kwingi ukaitwa daktari usifikiri ndo elimu kubwa, hata mfunga kidonda anaitwa daktari. Haya maneno niliyafanya mimi Muyuni, daktari alikuwa mmoja siku hiyo hakuja wengine wawili nataka kufunga dawa akaniambia bwana nisaidie nikawatia buluu wengine wenye vidonda vikubwa nikawatia ule unga wa shindano nikawapaka juu nikaitwa daktari, hasa huu udaktari wakati una madhara yake kusoma kwingi kuna matatizo, tufike mahali tuangalie haki ya mtu iko wapi, ubinadamu uko wapi tusifike Serikali kuja kuitia hasara Mwanasheria Mkuu usiwaonee haya, kaa na migogoro yote inatoka kunako ardhi nyiye mnasema mnataka kutatua huku Serikali inazidisha migogoro.

Waheshimiwa hii ndio hali ilivyo Kamisheni imeundwa, hati hazipo migogoro mnasema mnataka kuitatua kule Serikali mnazidisha migogoro, Mheshimiwa kuhusu *transformer* zilizokuwepo kwenye visima vya maji nataka maelezo yake. Ukenda Shirika la Umeme wanakwambia wenyewe ZAWA, ukenda ZAWA wanakwambia sisi hatuna mamlaka ya umeme. Hapa uje uniwekee kiswahili ambacho kina ufasaha, mimi ni muathirika mkubwa wa suala hili. Tatizo hili ni la muda mrefu na siku ile kama hukuingilia kati Mhe. Waziri ukatoa amri basi watu wa Jambiani wangeumia. Ndiyo yale nikasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, umefanya kazi nikupongeze kwa hilo. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kuna mashamba haya yanahitaji hati muda mrefu eneo la Paje, Umbuji wamo katika ule mradi wa kupima mashamba na wanadai hati zao muda mrefu. Hilo nikuombe

ulitafutie ufumbuzi. Kunako hati tayari limekaa sawa hili nafikiri hakuna tatizo kiasi kwamba kutachukua muda mkubwa.

Baada ya miaka mitatu tokea kuundwa Kamisheni hiyo nafikiri litafika pahali limalizike. Kero kubwa ilikuwa ni suala la watu wa Michamvi ambaye mimi ndiye ninayeumia kupeleka magari kwa wiki shilingi laki nne. Ukitaka kuhakikisha nenda kwa Sheha ya Michanvi kamuuliza maneno hayo, Jaku kweli analeta pesa hapa au anakuja kutudanganya Barazani tu. Nenda kapate ushahidi wa suala la Michamvi, siyo kwamba mimi napiga gumzo tu hapa natafuta siasa. Toka ukajiridhishe kwa Sheha wa Michamvi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo na ile kadhia niliyokupa suala la Bwana Ahmed Shehe pale Malindi naomba ulifatilie.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub una dakika mbili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nafikiri baada ya maelezo hayo namalizia juu ya suala la Mahakama ya Ardhi nimesahau. Wajumbe mara nyingi wanapiga kelele hii ni kama hadithi iliyokuwepo Mnazimmoja. Watu wanakwenda kupata haki zao wanarowa, hapana mahali pa kukaa, jengo halikidhi.

Mhe. Mwenyekiti, hii Mahakama bora ifungwe sasa hivi bora tutafute pahali kwenye mdodo au mboribo tukakae tuhukumu kesi. Jengo lile liko hatarini, halikidhi Mahakama ya Ardhi, mtu anatoka Shamba, hajui pa kukaa, akifika pale pana mvua pa kujistiri hamna, choo hukijui kiko wapi. Mahakama ya Ardhi haikidhi hata kidogo. Tumesema pale *child building* lilikuwa linahatarisha usalama likafanyiwa marekebisho, basi hili halikuwacha hata kidogo na Mahakama ya Ardhi. Kaipande ile

ngazi uisikie inalia twii!, unategesha kwanza mguu mmoja mmoja huwezi kupanga miguu miwili kwa pamoja. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, Mahakama ya Ardhi hairidhishi. Mhe. Hamza Hassan Juma yeye kama ni Mwenyekiti, wa Kamati aliangalie ukweli wake, linahatarisha usalama jengo lile litafutwe jengo jengine. Kila mwaka tunapiga kelele kwa suala hili, lakini hakuna jawabu linalopatikana. Kwa hapa nitahitaji maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo wala sina mashaka na utendaji wa Mhe. Bi. Salama lakini Mhe. Balozi naomba utupelekee salamu kwa Mhe. Rais atutengenezee Katibu mwengine kama itawezekana wa Wizara ya Maji ili akakae pembeni tu kuhusiana na suala la matatizo ya maji. Lakini Katibu Mkuu peke yake Ndg. Al Khalil atayafanya mangapi, hii Wizara ni kubwa kuna ripoti ya Mazingira, kuna Wizara tatu zimeingia hapa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nitasubiri jawabu la Mhe. Waziri lakini kama nilivyosema jana hakuna matatizo makubwa kama hayo akishakuniridhisha nitaachia tu.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakupongeza Mhe. Jaku Hashim na sasa hivi namwita Mhe. Mohamed Said Dimwa na baadaye atafuatiwa Mhe. Ali Khamis Bakari kwa dakika tano na Mhe. Panya ajitayarishe.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kukushukuru sana kwa imani ya nafsi yangu. Lakini kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu sana aliyenifikisha hapa nikiwaona nyote katika hali ya uzima na mimi niko sawa kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake bora kabisa. Lakini vile vile nimpongeze Naibu Waziri na yeye kwa kutujibu masuala bora yenye umuhimu na usahihi mkubwa. Nimpongeze sana ndugu yangu Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wote Wakurugenzi mpaka na yule mtu wa chini sana wa ufagiaji nawapongeza sana kwa kuwasaidia ndio maana Waziri akaonekana leo amewasilisha hotuba nzuri sana. Mhe. Salama hongera sana kwa uwasilishaji wako mzuri.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo nataka nianze kwenye programu ndogo ya Utawala wa Ardhi. Kwanza nataka niseme kwenye kitabu kikubwa hichi kwenye programu ndogo au programu zote zimetajwa programu na pesa zao, lakini bado sijaona ukurasa ambao unaonyesha pesa za maendeleo ziko wapi. Lakini kwenye kitabu chako hichi wametaja pesa za maendeleo zipo. Ningeiomba serikali kabla hatujaingia kwenye vifungu watuletee hii programu ya maendeleo iko wapi, la si hivyo hapa pengine patakuwa hatuwezi kupitisha vifungu hivi tunaomba sana watuletee maana tumesoma vya kutosha sisi hatuvioni.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee mbele, nikienda kwenye programu hiyo hiyo ndogo niliwahi kusema mwanzo na nikatoa hoja binafsi ya Sekta ya Uwekezaji maeneo hatarishi kwa sekta ya uwekezaji. Sekta ya uwekezaji hiyo niligusia katika sekta ya viwanda pekee. Lakini vile vile sasa kunakuja kitu chengine kuna sekta hii ya uwekezaji katika ardhi nayo kumbe inakadhia kubwa sana. Cha kushangaza tumekuwa tuna *list* nyingi sana na ndiyo wamenipa Kamati ya Bajeti nitafute pesa wapi. Nilihangaika vya kutosha nikaona pesa wapi zipo, nimezigundua pesa na sasa nataka mkae kimya mnisikilize jinsi nitakavyoelekeza pesa zilipo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais iliundwa Kamati ya Mhe. Mshimba ambazo *documents* zake ninazo hapa,

imempelekea mapendekezo lakini kumbe Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ni mtu mwema sana, ni mtu hodari sana, anajibu barua hiyo anampelekea Waziri aliyekuwepo wa Ardhi. Naomba niinukuu,

"Tafadhali rudia nakala yenye kumbukumu Namba Baraza la Wawakilishi K10/3/108 ya tarehe 17 Septemba, 2012 iliyoandikwa kwangu na Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi wa Baraza la Wawakilishi na kunakuliwa kwako na suala la hapo juu linavyojieleza.

Natumai umeyapata mapendekezo hayo na nakala nimeambatanisha kwa rejea yako na mara moja kwa kina kutafakari hatua za kuchukua kutokana na mapendekezo hayo. Kwa kweli Wizara yako ikiendelea na mtindo huu ni wazi kabisa kuwa tutaweza kuwavunja moyo na kuwapoteza wawekezaji hao ambao wamekuwa na hamu ya kuwekeza katika nchi yetu. Baada ya kuwahamasisha waje nchini kwetu kuwekeza hasa katika sekta ya utalii".

Nimshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais anasema, mimi nakubaliana na mapendekezo hayo na nakuomba uchukuwe hatua inayostahiki kuwarejeshea *Spice Islander limited* eneo lao waweze kuendeleza ujenzi wa mradi wao madamu tayari kibali cha *ZIPA* wanacho siku nyingi nashukuru sana na nakala zikapelekwe huko.

Nimshukuru sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, nataka nianze na hapa.

Mhe. Mwenyekiti, *lease* hii ilikuwa inalipwa dola laki moja na ishirini elfu (120,000), nimepiga kwa hesabu zangu za haraka haraka ni miaka tisa (9) ilikuwa tupate kama dola milioni moja na thamanini elfu (1,080,000) kwa pesa za Tanzania nimezihesabu

kwa kiwango cha chini ni elfu mbili mia mbili na thalathini (2,230) tumepata bilioni mbili, milioni mia nne na nane na laki nne (2,408,400,000). Hii ni *lease* moja. Sasa nna *lease* hapa 99 tukipiga hesabu hii hata bajeti ya Zanzibar ya Serikali yote tunaweza kutumia leo. Sasa nataka nijiulize na nilikuwa nakijiuliza kwa nia njema tu, hivi jana tulikuwa tukibabaishana na Waziri wa Afya pesa ndogo za Mnazimmoja, hivi hapa pesa hizi tungezipata tusingewasaidia wenzetu wanyonge, tusingewasaidia kuweza kupeleka bajeti hii serikali ikaweza kwenda vizuri. Nilikuwa nasikitika sana kuona jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile ajabu yangu inayonionesha naomba nisome Katiba hii na Mhe. Mwenyekiti, naomba ninukuu baadhi ya vifungu,

Kifungu cha 43(5) "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Mamlaka ya Rais ndiyo itakayokuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera za serikali kwa ujumla na Mawaziri chini ya uwongozi wa Makamo wa Pili wa Rais watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar".

Mhe. Mwenyekiti, najiuliza kwa mnasaba na barua ambayo nimei-*quote* serikali inafanya kazi vipi, najiuliza tu, sijui kama nilikuwa naota au vipi. Kuwa Waziri anapelekewa barua atoe, Waziri anakaa kimya. Pole sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais tunajua kazi zako unazozifanya kwa nia njema. Lakini vile vile Baraza hili la Wawakilishi liliunda Tume Teule ya Ardhi na hii ndiyo ripoti yenyewe. Cha kushangaza sana serikali hakuna jibu lolote, wamekaa *silence*. Mimi ningeomba sana nitumie kifungu cha 111 kuunda Kamati Teule ili tujadili jambo hili kwa kina na tulipeleke tukaunde Kamati iyende ikachunguze hii kadhia nzima.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, katika hizi *lease* nilizozitaja kuna watu wamechukua ardhi nusu ya Zanzibar hizi ni familia, huu ni ukoo, hawa ndiyo marafiki wa Waziri mmoja aliyekuwepo. Hili linatuuma kwa hali ya juu sana na nazungumza hapa kwa hisia kubwa sauti yangu tu ndogo, ingekuwa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano nadhani *microphone* leo ingepasuka, lakini sauti yangu mimi ndogo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nataka kuweka mnasaba na Kamati ya Mawasiliano iliyoyasema pale. Nilishangazwa sana na Kamati imezungumza. Kamati ya kisekta imekwenda kukagua lakini yote yaliyosemwa pale haikuridhika, ujue mtu mzima akilia pana jambo kubwa. Nina niya ya kuweka Kamati Teule kutumia kifungu 111. Lakini nina niya nyengine ya kuzuia fungu nataka nitangaze niya yangu hadharani kabisa, nina niya kabisa ya kuunda Kamati Teule. Tunaangalia vigezo vingi sana ambavyo vipo.

Mhe. Mwenyekiti, chengine cha kushangaza mambo haya haya ya ardhi kuna Msitu wa Ngezi nimekuja kikamilifu sana leo nimekuja mpaka na ramani. Msitu wa Ngezi baada ya kuwa mali ya serikali tamaa zetu zinatupeleka katika mahali pabaya sana. Hii ni hifadhi ya wananchi wa Zanzibar, hii ni hifadhi ya wanyonge wa Zanzibar, leo tunakwenda kwa sababu tuna *beach* nzuri tunakwenda kuikata viwanja ilimradi tuone viwanja gani humu. Nimesoma sana *decree* ile aliyokuwa Hassan Nassor Moyo kaiweka lakini nikaiyona ile barua ya Mhe. Mohamed Aboud na ninazo hapa nataka niseme. Anachokataza kwa kile tulichokisema kwa nini wale watu kama wamepata tusiwape katika mashamba ya heka ya karafuu kule tunawapa kwenye huu msitu. Kwa nini tukate viwanja hapa wakati Msitu huu ni hifadhi. Hii inatuumiza sana.(*Makofi*).

Mheshimiwa sitopitisha hata kidogo, tena naomba nionyeshe hisia zangu kuwa sitopitisha hata kwa asilimia moja bajeti hii ya Wizara hii. Mheshimiwa niondoke nadhani mmeshanifahamu kwenye ardhi na nimeonyesha jinsi gani ardhi ya wanyonge wa Zanzibar ilivyochukuliwa nusu na familia, nusu na Mhe. Waziri aliyekuwepo na marafiki zake.

Mhe. Mwenyekiti, niende sasa leo sitozungumza sana kwa sababu nina uchungu mkubwa sana kidogo kidogo tu kwa nia njema tu. Nataka kuzungumza kwenye *ZECO*, nataka kuzungumza *ZECO* kwa sababu nisije nikalia. Kwanza niwapongeze sana kwa hatua yao nzuri na wanafanya kazi nzuri. Mhe. Abdalla Maulid Diwani kasema watendaji wa chini na mimi nataka nikiri kwamba watendaji wa chini Mkurugenzi awatizame kwa jicho la huruma ndiyo wanaofanya kazi sio kuliko kukaa kwenye ma-*AC* nawapongeza sana kwa hatua zao wanazokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, jambo moja ambalo la kushangaza tunapoweka miji katika *site* mbali mbali tunatarajiwa kupata miundombinu imara. Tumeweka mji mkuu wetu wa pili kule Tunguu, miuondombinu ile ya maji, umeme inapaswa sasa ikawekwe na *ZECO*, lakini na Mamlaka ya Maji iwekwe mbinu sahihi kwa sababu tumeshachelea kuweka katika sehemu nyengine ambazo hazikupimwa kama Mtopepo na kwengineko lakini hata hivyo na wao wanapata maji ya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, lakini *fee* inakuwa kubwa na *fee* hii *ZECO* wanasema inaitwa *ZECO fee*. Kwa nini mipango imara isipangwe na nchi yetu kuelekeza kuwawekea miundombinu wananchi pale wanapokata viwanja au wanapoona mji ule upo. Tungeomba sana kwa sababu hizi pesa ni kubwa sana mtu pakulipia laki nne na elfu hamsini (450,000) anaweza akafikia laki tisa (900,000) au anafikia 1.6 *billions* tungesema tu Mhe. Waziri utuhurumie kwa

hili, sisi ndiyo wananchi wako tunakuomba sana utuangalie kwa jicho la huruma sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Mamlaka ya Maji (*ZAWA*). Niliwahi kusema kwenye ripoti iliyopita sijawahi kuipongeza Mamlaka ya Maji tangu niingie Barazani humu, mara ile lakini niliwahi. Mara hii niliipongeza kwa dhati sana kwa sababu kumbe kelele zetu Mhe. Waziri anazisikia alifanya ugatuzi mawilayani, akaenda kuwapitia wanyonge kule asikilize shida zao, baada ya yale mambo yote ya ku-*centralize* pale akasema mimi napeleka kule Wilayani. Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri nikupongezeni sana kwa hatua yenu kubwa ya kuongoza.(*Makofi*).
Mhe. Mwenyekiti, hakuna binaadamu asiyekosa kasoro, lakini niwaombe kasoro ziko nyingi sana kwenye mambo ya maji, tujitahidi, tuwapelekee wananchi maji, bila ya maji hakuna uhai na bila ya uhai hakuna maji.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Idara ya Mazingira. Idara hii niipongeze sana lakini nimpongeze sana Mkurugenzi wa Idara hii. Mhe. Waziri kwa kushirikiana na mimi bega kwa bega katika eneo la Shehia yangu ya Kilimani imefanya kazi kubwa tumeanza kupanda mikoko lakini nadhani na ule ukuta hauko mbali pengine akija atanambia ukuta, Mhe. Waziri ukija unambie ukuta pengine keshokutwa tayari utajengwa hili ndilo ninalolitegemea sana.

Mhe. Mwenyekiti, nirudi kwenye Wizara ya Ardhi kuna kitu kimoja kidogo sana nilikisahau. Kuna nyumba ambayo inauzwa inaitwa *Mashariki Palace*, nyumba hiyo ilikuwa inunuliwe na Kampuni moja ambayo ya MULDIVE nyumba hiyo ina namba hizi nataka nitaje taratibu mzisikie H/N289A ya Mjimkongwe niwaombe sana suala hili tumeshalisikia.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunisaidia nafasi hii. Ahsante.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mohamed Said Mohamed kwa mchango wako sasa namwita Mhe. Ali Khamis Bakari kama alivyoomba dakika tano lakini hazitimii vizuri na baadaye Mhe. Panya atafuatia.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nami kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira katika bajeti yake ya kitabu hiki ambacho amekiandaa na kukuwasilisha mbele yetu ambacho tunaendelea kukijadili.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Wizara na Watendaji wake wote kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya siku hadi siku kuhakikisha kwamba malalamiko hayo na kero hizi za wananchi zinapungua.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa suala la umeme. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee kuipongeza Wizara kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya yakuhakikishia kwamba zile kero ambazo zinawakabili wananchi wanazichukulia hatua siku hadi siku. Lakini vile vile niendelee kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhakikisha na yeye vile vile wananchi wake kawapelekea umeme kwenye miji, kwenye vijiji na jana tuu nilikuwa nafungua redio kuna wananchi wa Kisiwani Pemba Mkoani wanampongeza sana Mhe. Rais kwa kuona kwamba suala la umeme na kwao kwenye kijiji chao limefikia.

Kwa hiyo hapa nimuombe Waziri kwamba Rais pale kachukuwa ahadi kwa wananchi na akawapelekea umeme jambo ambalo kawaona wanyonge nimeuliza nikaambiwa kwamba wanyonge wale Mkoani wamepewa kama fursa nzuri na Rais ya kuona kwamba wanalipia pesa ya mapato ya umeme yaani kwa asilimia

ndogo sana mpaka kipindi cha karafuu maana ni wanyonge wamepewa *offer* maalum wao, walipie umeme ule kwa kiwango kidogo mpaka karafuu zitakapokuja nasikia kwa kweli ni suala zuri nampongeza sana Rais kwa kuliona hili wananchi wanakuwa wanyonge lakini ni vile vile anawatatulia matatizo yao.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi hapa nimuombe Mhe. Waziri kwa nini hachukuwi juhudi za makusudi kwa wale wananchi ambao umeme umewapitia mbali wanahitaji labda nguzo mbili, nguzo moja akachukua na yeye juhudi hii kuona kwamba anawapelekea umeme katika yake maeneo yao husika ili kuondokana na ile kadhia ambayo baadhi ya wananchi wanapotaka kuunga umeme wanalazimishwa kulipia nguzo mbili ama moja jambo ambalo linakuwa ni mtihani na pesa hizo wanakuwa hawana, kwasababu tumeona kwamba kiwango kidogo cha sasa hivi cha kuunga umeme ambao wenyewe kiutalamu wanaita *roof pole* yaani guzo liko chini ya nyumba yako ni laki tano kiwango kidogo cha sasa hivi.

Lakini kuna wengine wanatakikana walipe umeme pengine nguzo zimewapitia mbali pengine wengine wanahitaji nguzo mbili na hatujui bei ya nguzo sasa hivi maana yake kipindi kilichopita Mhe. Nadir alisema ni 150,000 lakini mimi namwambia kwamba siyo 150,000. Nguzo inazidi hapo lakini atakapokuja Mhe. Waziri namuomba sana akija aniambie kwanini atachukuwa juhudi gani kuhakikisha kwamba wananchi hawa ambao umeme umewapitia mbali kuweza kulifanikisha hili tatizo kuliondoa angalau waweze kupelekewa umeme wa karibu waweze kuunga na wao wajisikie *comfortable* katika nchi yao na kuona yale matatizo yameipukika.

Kwasababu Mhe. Mwenyekiti baadhi ya wananchi wetu ni wanyonge lakini vile vile na wao wanataka kudiriki kuweza kupata haya mambo mazuri, wengine maskini ya Mungu pengine mtu amepata nyama yake, amepata samaki wake anataka kufanya

angalau vibiashara ya malai na mambo mengine lakini hali kwa kusema ukweli ni mnyonge na hali kwa kweli imembana maana anataka na yeye anangalau mwake muwake taa na hamu ya kufanya hivyo lakini limekuwa kubwa jamba amabalo kuona umeme umepita mbali, nimuombe sana Mhe. Waziri na hili nalo aliangalie kwa macho mawili ili kuwaondoshea wananchi mzigo huu ambao kidogo umekuwa mkubwa kwao.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti katika kipindi kilichopita nilisimama hapa nikachangia nikamuomba sana Mhe. Waziri kwamba katika Wilaya yetu ya Micheweni tuna tatizo na tatizo hili lishakuwa endelevu Wilaya nzima ukiacha Chake na Wete hakuna sehemu maalum ya kuuzia umeme, vile vile hatuna sehemu ambayo katuwekea fundi labda likitokezea tatizo *shot* za umeme tunaona maguzo yanaanguka ovyo tunaona baadhi ya siku nyengine sehemu zinaweza zikatokezea *shot* tu za kawaida anaweza akaingia komba katika *transformer* lakini vile vile katika kipindi kama hiki cha mvua nyingi za masika basi tunaona kama mabarabara yanakatika maeneo kupitika inakuwa shida lakini kama kutakuwa na fundi pale na sehemu maalum aloiweka katika Wilaya ya Micheweni basi wananchi wanaweza kuipata huduma ile kwa haraka sana na kuona matatizo yale yanaondoka.

Kwa hiyo namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hivyo hivyo na mimi aniambie kwamba ni lini sasa atatuwekea fundi pale katika Wilaya ya Micheweni na kibanda kwa ajili ya kuuzia huu umeme kwasababu ni kweli amesema kwamba katika majibu yake ya maswali na majibu nilimsikia hapa akisema kwamba wameirejesha ile *process* ya kutumia umeme kwa kutumia njia ya simu, lakini ni kweli Mhe. Mwenyekiti lakini tunaangalia kwamba mambo ya mawasiliano *sometime* unakwenda pale unahitaji umeme unalipa pesa unakaa masaa ishirini nane waambiwa huduma haijatumika inakuwa kwa kweli ni usumbufu.

Sasa mimi niumuombe sana Mhe. Waziri haya maswala ya *electronic sometimes* yanakuwa yanazingua nimuombe sana atuangalie na sisi watu wa Wilaya ya Micheweni kuna watu wanatoka Kiuyu Maziwa Ng'ombe, kuna watu wanatoka Msuka, kuna watu wanatoka Makangale shida na kila ukielekea katika vijiji basi mawasiliano ya simu yanazidi kuwa hatarishi yaani hayapatikani. Kwa hiyo nimuombe sana angalau angefanya *process* yakuweza kutuweka Wilaya ya Micheweni kijisehemu ndogo cha Ofisi...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali muda wako umemaliza

Mhe. Ali Khamis Bakar: Mheshimiwa niongeze dakika tatu maana yake daa!...

Mhe. Mwenyekiti: Umeomba dakika tano mimi nishakupa na ziada malizia

Mhe. Ali Khamis Bakar: Mhe. Mwenyekiti, ahsante nakushukuru sana vile vile Mhe. Waziri nikuombe sana kuhusiana na maswali ya migogoro ya ardhi tuna sehemu zetu muhimu kwa mfano skuli sehemu za Wizara ya Afya, Vituo vya Afya wengi wao wanalalamika kukosa hati miliki tumeona migogoro ni juzi tu katika uchangiaji wangu wa Wizara ya Elimu nililisema hili katika Skuli ya Sizini pale watu wanahainga kwa kuona kwamba hawana hati miliki wananchi waweza kujenga majumba karibu lakini vile vile wamelichuka lile eneo kwa ajili ya kuanza masuala ya vilimo.

Nimuombe sana Mhe. Waziri kwa hikma zake na busara hizi taasisi zilizomo ndani ya zilizomo ndani ya Serikali hebu kwa haraka sana azipe hati miliki tuondokana na kero hizi, kwasababu imekuwa ni tatizo kwa sekta zetu siku hadi siku watu wanashindwa kufanya majukumu yao kwa ufanisi kutokana na

hizi kero juzi si tu tumetoka katika Kamati yetu ya Katiba na Sheria kutembelea baadhi ya taasisi zetu ambazo zimo katika Kamati yetu kwa mfano kama wenzetu hawa Vikosi vya SMZ nao vile vile wanahangaika wanakwenda pale Mheshimiwa sisi hapa hatuna hati miliki inakuwa wananchi wanatuvamia...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa malizia nimekwambia malizia

Mhe. Ali Khamis Bakar: Mheshimiwa baada ya machache namuomba sana Mhe. Waziri atungalie katika hoja zangu mbili hizo ambazo nimempa nampongeza sana kwa juhudi kubwa ambazo amezifanya siku hadi siku lakini asichoke kututatulia matatizo yetu naunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sasa naomba nimwite Mhe. Panya na baadaye Mhe. Abdalla Ali Kombo ajitayarishe na Mhe. Miraji Khamis pia ajitayarishe.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipatia fursa hii kuweza kuzungumza machache katika Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuanza na mchango wangu napenda nianze kumpongeza kwa dhati Mhe. Waziri kwa jitihada kubwa alizozionyesha katika Wizara hii pia nimpongeze Mhe. Naibu Waziri katika jitihada kubwa na watendaji wao wote lakini kwanini nasema pongezi za dhati kabisa kwa Mhe. Waziri kuna kipindi alipita kila Wilaya ya Zanzibar na kuongea na Viongozi mbali mbali wa Wilaya wa Majimbo wa Shehia kutaka kujua changamoto zinazopatikana katika Wizara yake.

Kwanza nimpongeze sana kwasababu kuweza kujua tatizo lako ndiko kuweza kutatuwa matatizo yanayotukabili. Mheshimiwa hongera sana tunakupongeza kwa dhati na tunasema tuko bega

kwa bega na wewe katika kuhakikisha unafanikiwa kutatuwa changamoto hizi ambazo zinakukabili katika sekta yako.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, pia nianze katika mchango wangu ambao mchango wangu utaanza katika Ofisi ya Mrajis ambayo iko katika ukurasa wa 14 katika aya hii ya 33 *bullet* ya kwanza ambayo inaonyesha jumla ya Shehiya tatu za Mpendea, Matarumbeta, Chukwani zimo katika hatua za utambuzi kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba Shehia ya Limbani imesajiliwa na Shehia ya Tamza.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hapa nilikuwa nataka kueleza nini hapa nilikuwa nataka kusema utekelezaji huu unaonekana ni mdogo sana haurithishi na nasema kwa hatua hii labda inaweza kufika miaka kumi bado hatujafika popote. Kwa hiyo Mheshimiwa mimi nilitaka kujua ninachoitaka kujua makakati gani wizara katika mwaka wa fedha ujao ambao umeweza kujipangia katika eneo hili la usajili wa ardhi.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika *bullet* hii ya sita ambayo inaonyesha katika jitihada za kuongeza uwelewa kwa wafanyakazi wa Afisi ya Mrajis wa Ardhi Afisi imetowa mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi wa Afisi ya Pemba. Nilitaka kujua katika dhamira hii ya uwelewa vipi kwenye Ofisi ya Unguja kwa mwaka ujao wa fedha kwa sababu hapa imeonekana ni kwa upande wa Pemba tuu nilitaka kujua katika ofisi ya Unguja mmejipanga vipi.

Pia Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na na mchangu wangu huu niendelee katika ukurusa wa 16 ambao unaeleza Usimamizi wa Shughuli za Upimaji wa Ardhi katika kifungu cha 36.

Mhe. Mwenyekiti, naomba ninukuu katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 katika Idara ya Upimaji na Ramani imefanikiwa

kupima jumla ya viwanja 259 kwa matumzi mbali mbali ikiwa ni pamoja na miradi mikubwa ya kitaifa na uwekezaji. Mheshimiwa nilitaka kujua Mhe. Waziri anakapokuja hapa basi na mimi aweze kunipatia maelezo kwa sababu hapa kiujumla tunaliona hili jadweli namba moja na mimi ndio ninalotaka kulizungumzia.

Mheshimiwa nilitaka kujuwa kwanza viwanja hivi vilivyopimwa kwa ajili ya maakazi vimeshatolewa kwa wananchi au bado na kama bado ni utaratibu gani ambao utatumika ili walengwa wakwezi na wakulima wafaidike katika mgao huu.

Lakini pili Mhe. Mwenyekiti, nataka kujua viwanja 54 vilivyoainishwa kuwa ni huduma mbali mbali ni huduma gani ningeomba Mhe. Waziri azitaje huduma hizo kwa faida ya wananchi ambao wanaisikiliza bajeti yao hii. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, kuna viwanja vya Vitega Uchumi nilitaka kujua miradi gani ya kitaifa iliyopewa viwanja hivi ambayo imeshapewa lakini na kama bado ni utaratibu gani utakaotumika mpaka kuweza kupata viwanja hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka kujua Wizara ina mkakati gani wa kufanya mapitio ya maeneo ya ardhi yaliyopipwa na kutolewa viwanja kinyume na sheria hasa wale waliopewa viwanja zaidi ya viwili kwa sababu sheria inataka mtu asimiliki kiwanja zaidi ya viwili na sisi tunaelewa kuna watu wamemiliki viwanja zaidi ya kumi, ishirini kwa hiyo tunataka kujua Mheshimiwa utakapokuja hapa naomba utueleze.

Pia niendelee na mchango wangu huu katika ukurasa wa 20 aya ya 40 katika *bullet* ya 2. Mhe. Mwenyekiti, hapa Idara imelipanga upya eneo la Saateni ili kuwawezesha wafanya biashara wa eneo la Michenzani kuhamia eneo hilo ili kuliwezesha eneo la Michenzani liendelezwe kuwa eneo la kibiashara.

Mhe. Mwenyekiti, pia mimi hapa nataka kujua kwasababu huwa mara nyingi kunajitokeza malalamiko wale wanaohamishwa katika eneo kupelekwa lile eneo ambalo lililopangwa mara nyengine hukosa wakapata wengine wapya ambao hawakuwemo kati mpango nilitaka kujua kama kuna utaratibu uliotumika mzuri ili wale walohamishwa katika eneo la Michenzani basi kuhakikisha ndio ambao wameweza kupatiwa eneo la kujiendeleza kibiashara.

Mhe. Mwenyekiti, pia nikiendelea katika *bullet* hii ya tatu ambayo nataka nisome kwa hapa nianze hapa kati ambayo Serikali imefanya maamuzi ya kujenga kituo kipya cha mabasi katika eneo la Kijangwani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara hii imeeleza kwamba imeshirikiana na Baraza hili la Manispaa la mjini, nilitaka kujua hatua gani za utekelezaji ambazo zimefikiwa katika eneo hili la Kituo hiki cha mabasi. Mheshimiwa utakapokuja hebu tueleze ili wananchi wetu waweze kuelewa.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na mchango wangu katika *bullet* ya tano ambayo pia nayo nitaisoma hapa kati ili kujali muda wako ili na wenzetu wengine waweze kuchangia "Kamisheni kwa kushirikiana na Mradi Huduma za Mji (*ZUSP*) zimefanikiwa kusimamia zabuni za kumpata mshauri elekezi wa kutengeneza mpango wa uendelezaji wa eneo jipya la kibiashara". Mheshimiwa mimi hapa kwasababu Mhe. Waziri hakulitaja lile eneo lenyewe moja kwa moja niilitaja kujua ni eneo gani hilo ambao tayari ndio limepangiwa kufanyiwa huo mradi na pia niseme nitowe halafu pia imeeleza hapa kama katika kutafuta wazabuni hawa inaonekana Makampuni arubaini haya yaliomba lakini sita ndiyo yaliyofanikiwa katika kuendeleza huo mchakato wa awamu ya pili.

Sasa ushauri wangu Kampuni hizi sita ambazo zimefanikiwa kuingia katika huu mchakato niombe sana sana Serikali kwasababu tumekuwa tukiona jinsi ya miradi ambayo kama hatukiwa makini basi tunaweze kuingizia Serikali hasara kubwa. Sasa nilitaka kujua tuu Serikali iweze kuzifanyanyia *do diligent* kwa ajili ya kuangalia uwezo wake ili isije ikawa hasara kubwa kwa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu kwa hivi sasa ni huo au hapana ngoja kuna nini kidogo nimesahau.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika ukurasa wa 47 kuna *operation* ya kusimamia marufuku ya mifuko ya *plastic* kwanza nipongeze sana sana Mhe. Waziri kwa kazi kubwa na nzuri lakini pia Wizara na Watendaji wake wote kwa kazi kubwa kabisa ambayo wameweza kuonyesha kufanikiwa katika zoezi hili la *operation* ya kuzuwiya mifuko hii ya *plastic*, lakini hata wenzetu kutoka Tanzania Bara wamekuja kusoma kwetu kwa jinsi ambavyo tumeweza kufikia mafanikio mazuri.(*Makofi*).

Lakini Mhe. Mwenyekiti katika kikosi kazi hichi kina wafanyakazi ambao wanafanya kazi kubwa na nzito na inayohatarisha usalama wao kwa baadhi ya nyakati. Mhe. Mwenyekiti, ombi langu na posho wanazopata inaonekana ni ndogo kulingana na ule ugumu wa ile kazi yao lakini pia posho hizi huwa zinatimiya miezi mitatu bila ya wao kuzipata.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu mcheza kwao hutunzwa na hawa wenzetu wamefanya kazi kubwa na nzuri ni lazima tuweze kuwafikiria ili waweze kupata posho inayostahiki lakini pia kuipata kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nachukua fursa hii kumpongeza tena sana Mhe. Waziri kwa juhudi yako kubwa

unayoifanya sisi wananchi wote wanakuona kwa muda mfupi ambao kulikuwa na malimbikizo makubwa ya upataji hati miliki umeweza kushughulikia matatizo haya kwa kiasi kikubwa na tunaelewa kwamba juhudi zako zitaendelea kumpatia kila mwananchi haki yake ya kumiliki ardhi katika usimamizi wako mzuri, baada ya hayo naiunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii na namtakia duwa za kheri Mhe. Waziri Mwenyezi Mungu aweze kuendelea na majukumu yake.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe kwa mchango wako sasa ninamwita Mhe. Abdalla Ali Kombo na kwa vile Mhe. Miraji hayupo anafuata Mhe. Rashid Makame Shamsi na Mhe. Hussein Ibrahim ajitayarishe. Mhe. Abdalla karibu sana

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Kwa heshima yako Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana nianze kwenye mchango wangu wa Wizara hii kwanza siungi mkono mia kwa mia katika Wizara hii hata kama atapitishwa siungi mkono.

Mhe. Mwenyekiti, wanasema watu maisha ni sawa sawa na gwaride, mnakwenda mbele nyuma twende, twende ukisikia nyuma geuka wewe wa mbele unakuwa wa mwisho, na kama hutaki uwe wa mwisho utaharibu mfumo mzima wa gwaride. Sasa kuna watu hawataki hili gwaride liwepo maisha wanataka wawe wa mbele, hii ni hatari.

Mhe. Mwenyekiti, nitaanza kuchangia katika maeneo ya Nungwi Mnarani, labda nitangaze tu kwamba nilikuwemo kwenye hii Kamati ya Ardhi na Mawasiliano. Mheshimiwa nimekwenda mwenyewe Nungwi na kamati pamoja na wataalamu au Maafisa wa Ardhi, ni Maafisa wa Ardhi lakini pia ni wataalamu wa ardhi. Mhe. Mwenyekiti, chakusikitisha sana kuna eneo la mwekezaji

analipa kila kinachotakiwa katika nchi hii, lakini kwa bahati mbaya sana mle mle kwenye eneo lake amepewa mtu mwengine.

Tunawauliza wataalamu nimefunga na walikuwepo inakuwaje mnafanya hivi? Aah! unajua hii kampuni ya FM, haya FM maana yake nini? Hii ni ya mama hii, nikawaambia sikilizeni hapa tuko kazini kwa watu, hapa hapana mama kila mtu mama yake kamuacha kwao. Sasa nilisikitika sana kwamba tuna Wizara nzima ya Utawala Bora, tuna wizara ambayo inasimamia uwekezaji lakini kwa aibu na kashfa katika ardhi ambayo sisi wenyewe tumempa *investor* anatokea mtu anapewa tunasema hii ya mama hii, na akitoka hapa basi akafanyiwe kwengine. Hivi wataalamu wa ardhi juzi nilikwambieni hatima hii itatufikisha pabaya, wengi wao huko nje wanakwenda upande upande kwa hatma. Sasa hili ni aibu kubwa kwa taifa lakini ni aibu kwa hii wizara.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii sijui inakuwaje kila waziri anayewekwa akifika pahala lazima aingie sherehe na watu wake, Kaskazi husema Kusini, Kusini maana yanakwa mashaka tu aibu. Nilimtania safari moja ingawaje haturuhusiwi Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira akasema hawa rasta rasta hawa mashaka, nikamwambia hawa wanaovaa kofia kama watu ndio watu hatari. Ilikuwa siku ya Ijumaa ile, usije ukaona mtu kavaa kofia ya kiua ukadhania mtu, maofisa wako wote ndio wanaovaa kofia kubwa kuliko mtu yeyote.

Kwa hivyo kitu hiki kwa kweli kinasikitisha na baya zaidi eneo la watu limechukuliwa ukiangalia takwimu ya Wizara ya Fedha kuna *investors* karibu 36 au kuna upungufu wa *investors* kwa mambo kama haya. Matokeo yake taifa sasa uchumi unaanguka, Waziri wa Fedha anatwambia unapanda lakini tulimuuliza kama hawa *investors* sijui kama 16 au wangapi wameondoka maana

yake tumeshakosa ajira, tumeshakosa pesa unapanda pandaje lakini wanaondoka kwa upuuzi kama huu.

Nchi hii ina Wizara ya Utawala Bora lakini mbaya zaidi anachukua *information* kwenda kusambaza nchi nyengine, hii ni aibu. Hii nchi nasema siku zote inatuuma kwa hili kwa kweli limeniuma sana na sitaunga mkono hata kama watu wote watapiga kura nikapigia peke yangu hili simo, hii ni aibu. Nawauliza mnafanya hivi vipi maana yake wizara, wizara halafu tukimtoa hapa basi tutampa kwengine.

Kwa hiyo jamani serikali inauma mtamuumiza mzee Dkt. Ali Mohamed Shein, mtamuumiza ndugu zangu, mfahamu mnafanya kazi kwa kumsaidia yeye. Kwa hivyo, kwa hili kwa kweli sifurahi waziri ukija hapa nataka uniambie lile eneo la watu na huyu mnayempa hii ni taratibu kutoka sheria ipi? Nasema tena ukisikia nyumaz geuka muda wako wa kukaa mbele umekwisha. Maana yake anaambiwa sawa sasa *75 percent* utachukua wewe mwekezaji umempa *document* yote halafu analipa kila mwaka unampa risiti, *75 percent* sasa unamnyanganya nini. Nataka waziri ukija utwambie lile eneo limekwendaje, umempa mwenyewe *100 percent* ama limebakia *70 percent* ananyukuliwa kwamba atoke, nataka jibu ukija.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili hapa nina masikitiko sana. Mheshimiwa tulifanya kikao wakati huo tuko kwenye kamati ilikuwa kesi ya *Hakachi Resort*. Nilikuwepo na ndio siku tulioambiwa hawa rasta wana mashaka, na mimi huwa navaa kofia yangu hii nikasema aah! bora hii kofia yangu ya hivi kuliko za viua, maana za viua hizi ukivaa unaonekana mtu lakini nikivaa hii najua aah! huyu mshenzi tu huyu, lakini mtu imani. Mheshimiwa mbele yetu baada ya mambo mengi, mashaka mengi na mbele ya Mkuu wa Wilaya wa Kusini ukakiri kwamba hili nalifuta. Jana nasoma soma ma-*information* yale ngoma iko pale

pale, mimi sina tatizo ungetuita ama ungemwita mwenyekiti jamani ile sikuifuta kwa sababu wataalamu wangu wameniambia kadhaa, kadhaa, kadhaa, lakini iko pale pale hakuna maelezo.

Mimi huwa nashindwa lugha ya kuzungumza kwa sababu natoka shamba, sasa nisije nikazungumza lugha nikaambiwa ushatukana Baraza, lakini hiyo ni kutuvunjia heshima maana yake kamati ni za Baraza. Ni kwamba Baraza halina maana hii kamati yake lakini hata sisi watu wazima tena maana hatuna na wengine walivaa hizo kofia. Sasa sijui kwa nini ukatwambia unafuta na iko pale pale, ungetwambia haikufutika wana sheria wangu wamekuja pale basi tungeridhika. Lakini tunakuja kukumbana uwanjani sasa, si vizuri hayo mengine huko kauziwa nani, kachukua mzungu gani mimi huko simo, lakini na kile kitendo cha kwamba unafuta unatwambia mbele yetu, lakini iko mle mle ile naona si barabara.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja tena unajua dhamana ni kitu kingine lakini sote nyinyi na sisi tumepewa dhamana. Sisi dhamana yetu wananchi wanatutizama, nyinyi mna majukumu haya mmepewa dhamana ya serikali lakini mkubali na mkubali kwamba nyinyi ni wawakilishi mnadhamana hii. Tumepewa wizara hizi siku zote huwa nazungumza hapa utasikia watu huwa wanacheka, tunapewa wizara hizi wengine tunazifanya ni wizara zetu. Yaani maamuzi yanatoka kichwani kwako, haya si ya BLM wala si ya Baraza la Wawakilishi. Kwa mfano, gazeti ninalo hili hapa kuna mnada wa hadhara.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nisome naruhusiwa kwa ruhusa yako.

Mhe. Mwenyekiti: Soma kwa ufupi.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Shirika la Umeme Zanzibar linawatangazia wananchi wote kuwa litafanya mnada wa hadhara wa kuuza mafuta ya *IDO* utaofanyika siku ya Jumamosi tarehe

07/01/2017 saa 5:00 asubuhi katika Ofisi ya Shirika la Umeme Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, mnada umefanyika na wanunuzi wakatokea katika masharti wakaambiwa unatoa nusu kama kawaida ya minada chengine baada ya muda utakitoa, baada ya muda hawakutoa. Maana yake mkataba umeuvunja lakini kilichofanyika sasa, baada ya mkataba kuvunjika sasa simu za upande upande zikawa zinaanza kwenda, wale watu wahalalishwe na anayetaka kuna baadhi ya simu ambazo zilipigwa. Kuna ya tarehe 18/04/2017 ziko kama saba hizi kuhalalisha wale watu wapewe tena.

Ndio niliposema jamaa wenzetu huko mmepewa jukumu la serikali na mmepewa jukumu la wananchi tunayofanya mengi sio, watu hawa baada ya mazungumzo ya simu mbili sitaki kutaja, huku na huku wameruhusiwa na kamisheni inayohusika imeshatoa barua watu hawa walipwe, wale waliovunja mkataba baada ya mazungumzo na mazungumzo. Jamani tutaiua nchi *serious* kabisa tufikeni pahala ukija huku nyumba imechukuliwa, ukija Uwanja wa Ndege kumeingia maji ilimradi mashaka. Mhe. Mwenyekiti, hii ni hatari nazungumza leo shirika na Mzee Jaku lakini nalia kwa uchungu tunakwenda siko katika nchi hii tumeumia wengine, wengine mmekuja juzi vijana wadogo, si mdogo kiasi hicho tumehangaika. Nimesomeshwa na nchi hii, napokea mshahara kwa nchi hii tunakwenda siko msifanye nchi wenu wengine, nchi ya watu wote.(*Makofi*).

Kama tunafika pahala tunagawana mali basi ipigwe mafungu, kila jimbo ipewe mali yake iwe ngoma imekwisha katika nchi hii. Wewe wa Donge lako hili, Makunduchi lako hili chukua nini, wewe Ungujaukuu chukua zako yawe yamekwisha, lakini haiwezekani wengine kazi yao kuchukua mali tu ya nchi hii ikawa sisi tunaambizana amani na utulivu. Chukueni vitabu vyote hivi

mwisho mnaandika amani na utulivu, amani na utulivu uko wapi. Hatwendi wanaume namna hii mnafika pahala si vibaya wanasema mambo yanaanza mtu kwao, lakini zile kampuni nyengine ofisini una *supply* za ndugu yako baba mmoja, za baba yako, wanaume ile kibafte ndio hii. Unanitaja kibafte hapa unachukua nchi na mali za nchi kwa kusema kibafte mbili nifute tena ndio ushapata, sasa hii hatari, hii yote iko chini ya Wizara ya Ardhi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko sana ardhi lazima kubadilishwe, kushabadilishwa sana na siwafichi hata wale Maofisa wa Ardhi wengine hawaridhishi wanachoka, maana wengine zile kofia wanavaa kofia kwamba za watu. Si kofia za ku-*pretend* kwamba leo Ijumaa, leo kuna ile siku anayokwenda Rais nini ile, utakuta kila mtu katia kanzu na kila mtu ana lake, ifike wakati wizara hii tubadilike. Mhe. Mwenyekiti, usije ukashangaa ukaja ukaona mkubwa wa wizara hii anakwenda kuuza viwanja usiku, usije ukashangaa. Kweli kabisa nazungumza kwa uchungu kabisa wanatoa viwanja vinakwenda nchi za nje, unakuta ratiba iko hivi anakwambia mtu unataka kiwanja kipi unachokitaka, nje ya nchi mihuri aliyokuwa nayo ya Wizara ya Ardhi. Mbele ya Mzee Karume yakhe sharii! sharii! ndio haya *wallahi* inauma, tunachoka na nchi hii tunategemea kura 2020 mnawaumiza watu halafu mtu ana kibanda chake kidogo anauza sigareti, hii si sheria vunja, tunafanya nini.(*Makofi*).

Unakuta mtu ana viwanja 14 Mhe. Jaku alisema nataja Mnyamwezi na mimi nataja Wahindi wanavyo hivi 14 mtu anavyo peke yake. Mimi nazungumza kama unatoka Kiboje nitakwambia wewe Mruguru shemeji yangu 14 peke yake mtu katika sehemu moja, wizara hii inatufanya nini. Kwa hivyo, wizara hii naomba ijirekebishe wananchi wanachoka kila mtu anataka kula, kila mtu anataka kujisaidia lakini ukimuona anajisaidia barabarani mgonjwa. Kwa hiyo, tujirekebishe

wakubwa wa wizara hii tunamchosha Rais anajitahidi sana, kenda kule fukwe zimeuzwa kama njugu, anakwambia hii yangu.

Kwa hivyo, nasema kwa uchungu kabisa kama tunagawana mali Zanzibar, basi Mhe. Mwenyekiti, lipigwe tangazo Waheshimiwa Wawakilishi kila jimbo lake zigaiwe mali iwe mpira umekwisha. Ukienda Uwanja wa Ndege, ukienda sijui baada ya visiwa vya Bawe, ukienda wapi kila mtu kachukua wenyewe wanakwambia mama huyo, mama huyo, mama vyakuzaa eeh!(Makofi).

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuna matatizo katika sehemu ya Magereza, hili ningemuomba waziri maana wamekuja wananchi sina uhakika wanasema umefukia lakini pameuzwa hili ningemuomba waziri tukakutana na wale wananchi na yeye tukajua ukweli wa mambo uko wapi. Kwa sababu sina uhakika hili tutalisemea ningemuomba tu waziri atakatafuta muda tukakaa na wale wananchi wa hapa kwetu Magereza tukakaa pamoja tukajua ukweli uko wapi, wao na sisi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nawashukuru sana *ZECO* na *ZAWA* ningewaomba tu *ZECO* hapa kwenye soko la Mwanakwerekwe Kivulini nawakumbushia kwa sababu huu ni kama mwezi wa tatu kuna nguzo imelala la umeme tuepukane na Mhe. Mohammed Aboud Mohammed kuja kutizama maafa, maana sasa yeye kamanda wa kutizama maafa. Kwa hivyo watu wa *ZECO* nawaomba waende Mwanakwerekwe Kivulini watizame ile nguzo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nakuja tena kwenye *investor* hawa tuna *indigenous investor* anaitwa Khamis Kipara sijui kampuni yake inaitwaje. Tulikwenda kule Mangapwani ambapo huko huko Wizara ya Ardhi imepima unasikia huyu kapewa leo, hapa palikuwepo na *ZURA* hayo mtayajua wenyewe, lakini analalamika sasa ukweli sijui uko wapi. Kwa hiyo, nakuomba Mhe. Waziri na

ukuta wako mpana tukae labda kwa nini hajapewa hiki kibali ana kosa gani lakini tujitahidi hawa *indigenous* uwasaidie na wao wapate rizki yao lakini pia wachangie kwenye nchi.

Mhe. Mwenyekiti, pale pana miradi nimeiona kwa macho yangu kama nakosea Mwenyekiti nisamehe kuna weupe, kuna weusi, weupe wengi wameshafanikiwa tayari kwa kupata *lease*. Nazungumza si kwamba naona furaha lakini nazungumza kwamba weupe wengi pale wamefanikiwa ni wa Zanzibari lakini weupe, mimi Mzanzibari lakini mweusi. Sasa na huyu naye naomba watu wakae kitako tujue kuna shida gani na kuna nini ile kazi anayoifanya nimeiona. Shimo lile nimeliona anavyohangaika nimeona tukae kitako tujue kuna nini, kama kuna kitu cha kumsaidia tumekwama basi tumsaidie na yeye aendeshe maisha yake.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa hayo nina mengi lakini naona roho haitaki kwa wizara hii, nakuomba mwenyekiti kama kuna chochote cha kufanyisha wizara hii kama haiwezekani wakawa pamoja basi tukae nao lakini kwa kweli hali ni mbaya, ni mbaya. Tunasema kuna diplomasia ya uchumi siku hizi kwa mabalozi wetu, sasa diplomasia ya Zanzibar kupitia wizara hii huko nje ni mbaya sana na bahati mbaya kuna wengine walionyanganywa viwanja ni ma-*pilot*. Kwa hivyo, kila anapotua Zanzibar iko hivi, Zanzibar iko hivi keshakwenda na maji dola zake sijui Kandwi au wapi huko zishachukuliwa. Kwa hiyo, naiomba wizara hii, hii haihitaji dhumari maana yake hata ukipiga bure hapandi shetani maisha, zishakaa wizara tano kila waziri anayekaa ukipiga dhumari hukutizama hivi, hata ukimpiga masikioni hapandi shetani wizara hii. Kama ni marogo yapo hapa katika wizara za serikali hawana dhumari wazungu hawawezi hawa hapandi maisha.

Kwa hivyo, mimi nimemaliza mheshimiwa ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Abdalla Ali Kombo nakushukuru sana umechangia kwa hisia kali sana lakini ndio hali. Sasa naomba nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi na baadae atafuatia Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na Mhe. Miraji Khamis Mussa ajitayarishe.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Awali nimshukuru sana Mhe. Waziri, Naibu Wake na watendaji wote katika wizara hii. Lakini vile vile nichukue fursa hii ya kuipongeza kamati inayohusika na wizara hii kwa uwasilishaji wao na kwa maelezo yao ya kina.

Nimshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, niwashukuru vile vile Wajumbe wenzangu ambao wamenitangulia. Lakini nimshukuru sana Mjumbe aliyetangulia hivi punde Mhe. Abdalla Ali Kombo Mwakilishi makini wa Jimbo la Mwanakwerekwe.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mengi yamechangiwa mimi nilikuwa sitaki kusema sana katika hotuba hii lakini nichukuwe fursa hii kwanza kuwapa pole watendaji na hususan Waziri na Naibu Waziri. Nawapa pole kwa sababu wizara hii ni nzito inawagusa watu wengi ina mambo matatu muhimu sana.

Kwanza ni ardhi; ardhi hivi sasa ndio kimbilio la kila mtu, ndio *asset* iliyobakia katika visiwa hivi. Sasa pana kazi sana katika ardhi. Lakini maji ndio uhai wetu yanamgusa kila mtu na kila kiumbe ambacho kipo katika ardhi hii. Lakini la tatu ni Nishati ya Umeme ambayo nishati hii ndio chanzo cha maendeleo ya mwanaadamu lakini vile vile uchumi katika nchi zote duniani.

Kwa hiyo, niwape pole kwa sababu wana kazi nzito na misingi ambayo imetandikwa hapo nyuma ndani ya hii wizara ndiyo ambayo hivi sasa sisi tunawapelekea madongo. Niwape pole sana kila Mjumbe alietangulia kusema hapa wengi wamezungumzia kwa hisia kubwa sana. Hii inaonesha kwamba kuna malalamiko mengi, kuna dhulma nyingi lakini wananchi wanapata matatizo mengi katika upatikanaji wakati mwengine wa huduma hizi. Kwa hiyo, niwape moyo watendaji, niwape moyo sana wayapokee na yale ambayo wanahisi yamo ndani ya uwezo wao basi tuisaidie serikali hii ili kuweza kuona kwamba wananchi wetu wanaishi salama bila ya matatizo yoyote. Niwaombe sana wasivunjike moyo na huo ndio ukubwa kwa sababu ukubwa ni jaa.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu mimi leo kwanza nije katika Jimbo langu la Magomeni. Wananchi wamenichagua na nawashukuru sana lakini wananchi wangu wana matatizo ya maji sehemu za Meya kuna tatizo, sehemu za Sogea kuna tatizo. Mhe. Mwenyekiti, kuna mradi unaitwa SEMUSO ambao huu kwa makusudi ulikuwa una lengo la kufanya wananchi wa Sogea wananchi wa Sebleni na Muungano waweze kupata maji vizuri. Lakini hivi sasa mradi ule umezidiwa kiasi ya kwamba wananchi wangu wa Sogea hawapati maji vizuri na kwa sababu bomba lile kubwa limeungwa katika hali ambayo hivi sasa naweza kusema ndio ambayo inachangia kuweza kukosekana kwa maji kwa ufanisi katika maeneo hayo, limeungwa kinyume na utaratibu. Ningeomba sana mamlaka inayohusika kuweza kufuatilia laini ile ya maji ya SEMUSO ili kuweza kuwabaini wale waliounga maji kinyume ya taratibu na wengine wanamahozi makubwa na visima vikubwa kwa hiyo wanawanyimamaji wengine.

Ningeiomba sana mamlaka inayohusika kufatilia bomba lile la SEMUSO ili kuona tunapata maji kwa yale mategemeo ya mradi ule. Mheshimiwa kuna kisima hichi ambacho kiko kwa Bint

Amrani. Nimshukuru sana Mhe. Mbunge wa Jimbo la Mpendae Mhe. Turky ambaye alikichimba kisima kile. Hivi sasa tunaingizwa katika mawio sana hata juzi siku tatu tu tumeingizwa kwenye mawio wananchi wangu hawapati maji sehemu za Meya na hiyo ni kutokana na kisima hichi. Kisima hichi kimekabidhiwa Mamlaka ya Maji *ZAWA* na *pump* yake imeungua karibu wiki tatu. Lakini inashanganza sana ndani ya mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani wananchi wanapata shida ya maji kutokana na kutorejeshwa kwa *pump* ile.

Nimeona katika kitabu cha bajeti humu kuna utaratibu wa kubadilisha kutengeneza *pump* lakini lazima tufukirie huu ni mwezi mtukufu wa Ramadhani. Niiombe sana Mamlaka ya *ZAWA* irejeshe haraka sana ile *pump* ili wananchi wetu waweze kupata maji kwa ufanisi na kuwapunguzia adha ya maji na hususan eneo lile hata haya magari ya maji basi huwa hayafiki mara nyingi huwa yanafika katika sehemu mbali mbali.

Nimuombe sana Mhe. Waziri na namuamini sana katika hili basi aifanye huduma hii ya maji katika Jjimbo langu katika *line* hizi mbili basi tuweze kuona kwamba wananchi hawaturushi katika mawio ili wapate maji kwa ufasaha kabisa na sisi tuweze kupata neema ambayo iliyotarajiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo katika utetezi wa huduma ya maji katika jimbo langu nije sasa katika suala zima la ukusanyaji wa mapato. Mapato yanahusiana na maji, kwanza niwapongeze sana mamlaka kwa kuweza kufuatilia na kusimamia upatikanaji wa mapato yahusianayo na huduma ya maji.

Mhe. Waziri katika hotuba yake alisema kwamba wizara haikufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato haya ya maji na tatizo kubwa sana ambalo ameeleza ilikuwa ni muitiko mdogo wa walipaji wa maji. Mimi niseme tu kwamba Mhe. Mwenyekiti,

inawezekana tukachukuwa miaka mingi sana tukawa hatufikii malengo ya makusanyo katika huduma hii ya maji, na kwa nini nasema hivyo. Tatizo kubwa sana Mhe. Waziri dadaangu Salama Aboud Talib kufikiwa au kutofikiwa kwa malengo katika ukusanyaji wa maji ni huduma yenyewe.

Huduma hii ya maji kama haitokuwa endelevu tusitarajie kwamba tunaweza tukafikia malengo ya ukusanyaji wa mapato. Ni ukweli usiofichika kwamba huduma ya maji yanayotolewa na *ZAWA* sio endelevu, unaweza ukayapata miezi miwili, miezi mitatu huyapati umeyapata mwezi mmoja mwezi wa pili huyapati, kwa tafsiri hii hatuwezi kufikia malengo. Wananchi sio kama wagumu katika kulipa malipo ya maji na hususan mijini, sote tunahitaji maji. Lakini endelevu wa maji haupo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe ninanunua maji au nalipa huduma ya maji ya shilingi elfu kumi na moja katika eneo langu kutoka katika kisima cha mtu binafsi wakati *ZAWA* ningekuwa nayapata pengine ningelipa shilingi elfu nne au elfu tano. Sasa tazama tafauti iliopo na kila ukifika mwisho wa mwezi nalipa shilingi elfu kumi na moja na maji hayo nayapata kutoka saa kumi za jioni mpaka saa moja za asubuhi lakini nayapata kwa uhakika mpaka mfreji wa juu nakoga. Lakini huduma zetu za *ZAWA* sio endelevu. Kwa tafsiri hiyo Mhe. Mwenyekiti hatuwezi kufikia malengo. Hata wananchi wa kawaida katika visima tunavyochimba sisi Waheshimiwa ambavyo wanavichangia kwa huduma ya maji wakifanya mahesabu kwa mwezi basi anatumia kati ya elfu kumi na elfu kumi na tano. Lakini maji yangepatikana kwa uhakika ya *ZAWA* basi angetumia elfu nne au elfu tano.

Kwa hiyo, niiombe tu serikali kupitia wizara yake na Mamlaka basi najua matatizo yanajulikana basi hizi fedha ambazo tunazipata za misaada basi tuanze sasa kuweza kurekebisha hii miundo mbinu ya maji ili kuona kwamba wananchi wetu Zanzibar

wanapata maji kwa asilimia kubwa ili kuweza kuondosha adha hii ambayo inawafanya wasishiriki vizuri katika shughuli nyengine za kimaendeleo na za kujiletea kipato.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije sasa katika suala zima la ukaguzi wa maeneo yaliyohitaji kutayarishiwa mikataba ya uwekezaji na maeneo ya kilimo au ya eka tatu. Kwanza niwapongeze sana wizara katika ripoti yao wameeleza kwamba wamefanya ukaguzi wa maeneo 73 yaliyotayarishiwa mikataba ya ukodishaji. Lakini vile vile zoezi kama hili wamelielekeza katika sehemu ya eka tatu kwa kuweza kupitia maeneo 108 yaliyofanyiwa ukaguzi. Niwapongeze sana kwa juhudi zao na nina imani kwamba wanaelewa majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa kuna tatizo sana katika suala hili la eka tatu, lazima wizara na serikali ikubali kwamba kuna matatizo. Hivi sasa wenzetu sijui kama wamefanya utafiti na wanaweza kuja kutueleza wamebaini ni eka ngapi zimeshauzwa na mikataba yake au nyaraka zake zimebadilishwa kwamba eka zile ni mashamba akija Mhe. Waziri atueleze katika pita pita yao wamebaini hilo na zaidi haya yako katika Wilaya ya Kati. Wilaya ya Kati maeka mengi yameuzwa na nyaraka zake zimegeuzwa kuwa sasa ni mashamba na sio eka.

Mhe. Mwenyekiti, mzee wetu Abeid Aman Karume alikuwa na nia nzuri sana ya kuweza kutupa hizi eka tatu kwa sababu alikuwa anamini kwamba eka tatu hizi wananchi watazitumia kwa kilimo na kilimo ndio uti wa mgongo wazee wetu walibahatika wakachukuliwa maeneo ambayo yalikuwa yanaishia mawe wakaja wakapewa maeneo ya eka tatu. Lakini leo hii eka tatu hizi zimekuwa wajanja ndio kimbilio lao kama nilivyosema tatizo la ardhi. Maeka haya yanauzwa Mhe. Mwenyekiti, na viongozi wetu ngazi ya Masheha, ngazi ya Madiwani, Wakuu wa Wilaya, Mikoa wote hao kama tutachunguza basi tutaona kwamba wanahusika

kwa njia moja au nyengine. Baya zaidi baadhi ya maeka sasa yanazungushiwa makuta. Sasa hujui ndani ya kuta lile mnafanywa shughuli gani.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri dadaangu nampenda sana nimsaidie katika hili kuweza kuchunguza maswala haya na inawezekana hata ndani ya wizara yake mna wajanja ambao wametayarisha hizi nyaraka. Nimuombe sana vyenginevyo tutakuwa hatuna ardhi ya kilimo. Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza katika hotuba ya Wizara ya Kilimo washirikiane sana katika kuona kwamba maeneo yetu ya kilimo yanabakia ili kuweza kuona kwamba tunapiga hatua katika kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie tulikuwa na Mwakilishi au Mjumbe wa Zanzibar katika Bodi ya Wakurugenzi wa *TANESCO* katika kipindi cha nyuma. Hivi sasa ningeomba Mhe. Mwenyekiti, waziri aje atueleze kama tunae Mjumbe katika *TANESCO* katika Bodi ya Wakurugenzi na kama hatuna ni sababu gani ambazo zimepelekea hivi sasa tusiwe na Mjumbe kwa sababu *TANESCO* ndio wenzetu ndiko tunakopata umeme. Sasa iwapo hatuna Mwakilishi katika Bodi hii ni hatari. Ningemuomba sana Mhe. Waziri akija atueleze sababu gani au kama Mjumbe huyo tunae au hatuna ni sababu gani.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na mimi niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia. Lakini Mhe. Waziri atakapokuja na kunihakikishia juu ya upatikanaji wa maji katika jimbo langu namuongeza na asilimia kumi. Ahsante sana nashukuru. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Rashid Makame kwa mchangia wako na sasa naomba nimwite Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na baadae anafuatiwa na Mhe. Miraji Khamis kwaza ajitayarishe.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu awali ya yote kufika mchana huu kuchangia bajeti hii muhimu sana ya serikali yetu.

Lakini pia nikushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kuchangia pia katika hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa kweli nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa kazi kubwa anayoifanya. Lakini pia niipongeze wizara, Katibu Mkuu nimpongeze sana kwa juhudi zake kubwa japo wizara hii kubwa lakini kwa kweli mchango wake tunauona na anajitahidi sana hasa suala hili la maji na mambo mengine katika nchi yetu.

Lakini pia nimpongeze sana ndugu yangu Mhe. Nassor Salum Ali (Jazira) ni Mjumbe wa Bodi kwa kazi yake kubwa anayoifanya hata jana nilimuona kwenye *ZBC* anazungukia maeneo mbali mbali kuangalia maendeleo yanayofanyika.

Mhe. Mwenyekiti, nianze katika ukurasa wa 33 kifungu namba 75. Kwanza niishukuru sana serikali kwa kazi kubwa inayofanya katika sekta hii ya nishati. Ukiangalia katika kitabu cha Mhe. Waziri hapa mimi nimpongeze kaweka nyuma picha hapa kuna picha na Wajumbe wamekaa viongozi mbali mbali wa nchi yetu kuhusu suala hili la mafuta na gesi. Kwa kweli namshukuru sana na picha hii hapa iliyorushwa ndege ya kufanya utafiti hapa imeshamaliza kazi. Kwa kweli imani yetu kubwa na wananchi wetu kwa mafuta sasa yataweza kuchimbwa.

Lakini mimi niseme katika utafiti wetu Mheshimiwa wa hii *oil and Gas* sasa hivi imeshachukuwa miaka kumi kwa kweli muda mrefu na wananchi wana imani kubwa kwamba haya mafuta wachimbwe ili tupate maendeleo hasa katika upande wa ajira kwa vijana wetu. Kwa kweli mimi naomba sana serikali ijitahidi sana muda umeshakuwa mkubwa hasa tujipange ili tuweze kuchimba

mafuta haya ili vijana wapate ajira japo mafuta itachukuwa muda mrefu kupata lakini ile ajira itatusaidia sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya wizara hii ya Ardhi na Mawasiliano kwa muda wa miaka mitatu, nilikuwa naijua sana wizara hii na nimefanya kazi kubwa katika kipindi cha miaka mitatu ya nyumba. Kwa hivyo nafahamu sana hii sekta ya nishati kama tutaweza kuichimba basi tutaweza kufanikiwa sana katika nchi yetu. Mimi nitoe mfano nilipokuwa Mjumbe wa Kamati niliwahi kufika Songosongo kwenda kuangalia mradi wetu kule Mtwara wanaochimba ndugu zetu gesi. Kwa kweli wananchi wanafaidika kwa mradi huu hasa ukitizama wananchi wa pale wanasoma bure watoto wao ukitizama afya bure wanapatiwa, ukitizama kwenda Dar- es Salaam na kurudi wanapata usafiri bure kwa ajili ya mradi huu.

Kwa hiyo, mimi naomba sana Mheshimiwa tukifanikiwa kuchimba haya mafuta tutafanikiwa kuwasaidia wananchi wetu ajira na mambo mengine maendeleo katika nchi yetu. Kwa hivyo, mimi naomba itolewe taaluma sana kwenye TV wananchi wetu wana hamu kubwa na hili suala limechanganyika na mambo ya kisiasa. Kwa hivyo, naomba Serikali yangu ya Mapinduzi kila inapofikia basi itoe taaluma kwenye TV na Vyombo vya Habari tunapokwenda kwenye mchakato huu wa uchimbaji wa mafuta, *oil and Gas*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende kwenye Ripoti ya kamati. Niipongeze sana kwanza kamati yangu hii ya Mhe. Hamza Hassasn Juma Mwenyekiti kwa kazi kubwa sana waliyoifanya na jana nimesoma ripoti yao hapa nilipata na nina bahati na Wajumbe wawili Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa pia ni Mjumbe wa kamati na Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira) ni Mjumbe wa kamati. Jana nilipata kidogo kwenye ripoti ya kamati uharibifu wa

mazingira umejitokeza katika Jimbo la Mtoni zaidi ya nyumba 80 sasa zinaingia maji.

Mhe. Mwenyekiti, hili suala mimi mwenyewe nimeshaenda kuliona na nakwenda kuona nyumba baadhi juzi mwezi kuandama maji wanaingia katika nyumba za watu wananchi wetu. Kwa hiyo, mimi niombe sana serikali iangalie ufumbuzi gani wa kuwafidia hawa wananchi au kufanya miundo mbinu yoyote haya maji yasiweze kufika au itakuwa hatari baada ya muda mfupi Jimbo la Mtoni eneo la ukanda wa pwani lote litakuwa limo kwenye maji. Kwa hiyo, mimi naomba sana na juzi juzi Mhe. Balozi Seif Ali Idd pia alikwenda nilimuona kwenye vyombo vya habari alikwenda kukagua maeneo yale. Kwa hivyo, mimi naomba serikali na kupitia kwa wananchi wangu Mheshimiwa sasa hivi ni kilio kikubwa kwa wananchi wangu wa Jimbo la Mtoni haya maji yanasogea kwa kasi sana. Kwa hiyo, naomba suala hili Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwenyekiti wa kamati ulifuatilie kama ulivyokwenda kwenye ripoti yako basi ulijuwe ili tuweze kuwasidia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nije kwenye ukurasa wa 57, lakini kwanza niipongeze sana serikali na mimi nilikuwa Mjumbe wa kamati hii Mheshimiwa ukiangali hii ripoti ya Mhe. Waziri katika kifungu 57 mradi huu Ras al Khaimah visima 50. Kwa kweli mimi naipongeza sana serikali kwa juhudi kubwa sana. Mimi nilipokuwa Mjumbe wa Kamati mradi huu ndio kwanza unaaza wanaanza kuchimba na wanaanza kujenga hawa Ras Al Khaimah visima hivi 50. Lakini sasa nashukuru katika ripoti ya Mhe. Waziri kaandika kama mradi huu tayari umekamilika. Kwa hiyo, mimi nawashukuru sana kwa serikali kwa juhudi zake kubwa kwa Ras al Khaymah kutusaidia ili kupata upatikanaji wa maji kuongezeka.

Lakini pia nije kwenye Serikali ya China tumeona hapa matanki mawili maeneo ya Chaani na Donge na mabomba yenye urefu wa kilimita 7.2 Donge, lakini kilimota 3.8 umekamilika. Mimi niipongeze serikali sana kwa juhudi zake kwa sababu hili suala lilikuwa sisi tunakwenda nalo mbio ili kuweza kuona suala hili la maji safi na salama yanapatikana kwa vizuri sana. Kwa hivyo, juhudu ya serikali yetu imejitahidi sana kwa suala hilo.

Lakini nije kwenye ukurasa wa 25 kifungu 53 Mamlaka ya Maji kupiti mradi wa *ADFI2* imefanikiwa kuchimba visima 9 pia Mheshimiwa. Jambo la kujipa hongera sana kwa serikali yetu kuona kazi kama hizi zinafanyika, ukiangalia hata maeneo hapa aliyoandika Mhe. Waziri Bumbwini, Bubwisudi visima sita, Machui kimoja, kuna maeneo mengi tu visima karibu 9 vimechimbwa mimi nampongeza Mhe. Waziri na kazi hii imefanyika kwa muda mfupi na tumeona mazuri yake. Vile vile na matengenezo pia ya visima 23, ukitizama Mbweni, Mombasa, Kaburikikombe, Kianga, Mwembe Mchomeke, Chumbuni vimefanyiwa matengenezo kwa kweli visima hivi 23 ambapo haya yote yalikuwa kwa kipindi kile mimi mjumbe wa kamati kulikuwa kuna shida kubwa, lakini sasa hivi nashukuru sana Mhe. Waziri kuona mambo haya yanakwenda vizuri na wajumbe wa kamati kwa kufanya kazi zao vizuri. Kwa hivyo, nashukuru sana hata Welezo pia kwenye chanzio cha maji awamu ya pili umekamilika sasa Mradi wa *JAICA*. Mimi nashukuru sana kuona mambo mazuri kama haya kwa kweli inasaidia kwenye nchi yetu.

Pia Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kuna matengenezo pia wamefanya kwenye hizi chemba 26 na *valve* 36 kwa kweli nashukuru na napongeza sana. Kwa hivyo, mambo mazuri sana Mhe. Waziri umeyaandika kwenye kitabu chako na tumeona *improvement* ambayo tutaipata baadae kwenye maji muda sio mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze Mamlaka ya Maji *ZAWA* kwenye kifugu 63 ukurasa wa 28 imefanikiwa kufanya matengenezo mabomba Mwembeladu, Michenzani Saateni, Kijichi, Kihinani, Dole, Dimani, Mfenesini kwa kweli mimi nawapongeza sana *ZAWA* mmefanyakazi kubwa na tunaona mazuri mnayofanya. Lakini mimi niseme tu Mhe. Mwenyekiti, haya mabomba kurekebisha yalikuwa kidogo tujitahidi, kwa sababu siku zile mimi ni mjumbe wa kamati nilikuwa nakwenda kutembelea kwenye mabomba miundombinu hii ilikuwa chakavu sana, lakini ukitizama pia mabomba haya yanapokuwa mabovu Mhe. Mwenyekiti, basi na haya maradhi pia ya mripuko ya kipindupindu yanakuwa maji yanachanganyika baina ya maji safi na yale maji machafu mvua zinapokuja yanachanganywa kwenye mabomba wananchi wanakwenda kutumia maji hayo inakuwa mara nyingi wanapata maradhi.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana serikali yangu na hasa kupitia *ZAWA* tujitahidi sana kuyaangalia mabomba na hasa kabla hiki kipindi cha mvua muwe mnayapitia mabomba na kama kuna matatizo muweze kuyarekebisha. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia sasa hivi matangazo kila wakati unakuta kwenye vyombo vya habari TV zetu zinatangaza Zanzibar kuna cholera. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana tuangalie kwa sababu sasa hivi tunategemea utalii pia hapa Zanzibar na wananchi wa nchi za nje wakisikia mambo kama haya wanashindwa kuja kwenye utalii, na sisi tunategemea utalii mwezi wa 6, 7 na 8 wageni wetu kuwapokea hapa. Sasa tukiangalia nchi za wenzetu ukitizama India hii cholera haiishi maisha yote ukenda utaambiwa lazima uchanjwe, ukenda Hong Kong China lazima uchanjwe cholera haiishi. Sasa haya maradhi tujikinge mapema sisi, lakini suala la kutangaza kila wakati kwenye vyombo vya habari, kwa kweli mimi sifurahi suala kama hili ni kama tunajiumbua wenyewe kuonesha tuna maradhi, haya maradhi yanatibika, tujipange na

hasa kwenye usafi mazingira yetu maeneo yetu yawe masafi hasa maji safi, mabomba haya mnayotengeneza.

Kwa hivyo, mimi nawaomba sana *ZAWA* muyatengeneze kila wakati mabomba, linapoharibika tu basi mkatengeneza msisubiri mpaka maji na mvua ije yachanganyike wanachi wetu wapate kunywa maji machafu wapate maradhi. Mimi nawapongeza pia *ZAWA* wametengeneza pampu zaidi ya nne katika maeneo mbali mbali. Pia katika masuala ya umeme Unguja na Pemba wametengeneza 27 vianzio vya umeme, jambo hili ni zuri sana. Kipindi cha nyuma ilikuwa kisima kinashindwa kujiendesha kwa sababu ya umeme au pampu imeharibika, lakini sasa hivi tunaona marekebisho mengi mmefanya. Kwa hivyo, mimi naomba sana msisubiri mpaka mambo yaharibike zaidi muwe mnapitia vile vianzio vya maji ili kuangalia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme wajumbe wengi wamezungumza hapa. Maji ni kitu muhimu sana kwenye nchi yetu hasa kwa binadamu huwezi kuishi bila ya maji. Mimi sijawahi kumuona mtu anaishi bila ya maji. Mimi nasema sasa hivi maji ni biashara, tena biashara ya maji haitaki hata matangazo pakijulikana pana maji tu basi mtu atafanya kila njia apate maji. Kwa hivyo, mimi nawaomba *ZAWA* hapa mmeandika kwenye kitabu chenu kwamba mmefunga mita 4,000, ukitizama mita 4,000 Mhe. Mwenyekiti, ni kidogo hazitoshi kwa Zanzibar, hata ukisema mtu alipe shilingi 2,800/- au shilingi 3,000/- kwa mwezi pia ni fedha kidogo na watu wako tayari kulipa hii huduma, sio kwamba wanakataa kulipa.

Ukiangalia Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa mjumbe wa kamati, tulikwenda Arusha sisi *ZAWA* walitupeleka kuangalia wenzetu wa Arusha wamefanikiwa suala la maji, tena wamefanikiwa kwa asilimia mia kwa mia. Hata juzi mimi nilikwenda na kamati ya bunge Arusha, kila ninapouliza maji yapo naambiwa yapo, wananchi wanalipa maji sio tatizo wanalipa na maji yalikuwa

yanafika kwa wakati kabisa. Kwa hivyo, hata sisi Zanzibar kama wananchi wanapata maji, mimi sidhani kama watakataa kulipa. Utafiti nilioufanya katika jimbo langu mtu mmoja anatumia maji kwa siku ndo 10 na familia yake, apate ndo 10 kwa siku lazima au bila ya hivyo hawezi kujitosheleza kwa mahitaji yake. Kwa mwezi apate ndo 300 yule mtu nyumba moja tu. Sasa mtu ukimwambia alipe shilingi 5,000/-, hata umwambie *flat rate* usimwekee hata mita, Mhe. Waziri angalia hata kama mtu hana mita basi mwekee *flat rate* alipe zile fedha ili *ZAWA* ipate kujiendesha pia. Lakini leo kwanza unafunga mita 4,000 ni kidogo sana Mhe. Waziri, wananchi sio kama wanakataa kulipa wanataka huduma wapate watalipa maji, kwa sababu huduma ya maji sasa hivi kuipata wananchi wetu ni ngumu sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kwenye ripoti ya kitabu hiki cha Mhe. Waziri kifungu cha 79 Mamlaka ya Maji Zanzibar 2016/2017 ilijipangia kukusanya bilioni 5.1, sio pesa kidogo lakini tizama kitabu hiki cha waziri kinasema katika muda wa hadi kufikia Machi 2017 jumla iliyokusanywa ni bilioni 2.045 tu karibu nusu nzima haijakusanywa ya fedha. Sasa sio kama wananchi wanakataa kulipa maji, wananchi wako tayari. Sasa mimi naomba hata kama hizo mita hazipo za maji na maji kama yanafika kwenye nyumba basi mpangie yule mlipaji alipe japo *flat rate* tu kwa mwezi kiasi kadhaa alipe, kwa sababu lazima serikali ipate maji na *ZAWA* wajiendeshe, sasa usisubiri mpaka upate mita Mhe. Waziri, hizi mita zitakuja lini kwa Zanzibar nzima itachukua muda.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kama kule Arusha kuna nyumba hazina mita, lakini ni *flat rate* wanapewa kwa mwezi shilingi 20,000 au 30,000 alipe, na mtu analipa hakatai kwa sababu anapata huduma ile ya maji. Kwa hivyo, naomba sana iangaliwe hiyo *flat rate* na nini kwa sababu ya kuweza. Lakini nikiiangalia ripoti ya kamati ya mwaka 2013/2014 mimi nilikuwa

mjumbe wa kamati, ripoti ya kamati ilikuwa inasema *ZAWA* wameweza kukusanya mpaka bilioni 11 kwa kipindi hicho. Lakini mwaka 2016/2017 *ZAWA* wanakusanya bilioni 2, wamezidi bilioni moja tu. Sasa mimi naona tuko nyuma sana Mhe. Waziri, wananchi sio hawataki kulipa, wananchi wanataka kulipa lakini hizi mita zinachelewa sana na inakuwa usumbufu kwa wananchi wetu. Kwa hivyo, mimi naomba sana uangalie.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ripoti ya kamati ambayo ni nzuri, hasa ripoti yetu ya kamati hii inasema kama Mwanyanya taarifa ya wataalamu ndio msitu unaohifadhi kiasi kikubwa cha maji. Mhe. Mwenyekiti, msitu huu ni wa historia sana na kwa kweli ukiangalia juzi mimi nilikwenda Mwanyanya nilikwenda kuangalia chemchem ina maji na maji yanakuja kwa wingi hapo, sasa mimi sifahamu kama ni mvua tu au, lakini maji mengi mazuri na safi ya chemchem, hii ni *national resource*. Mimi nasema haya maji ya Mwanyanya ni mazuri sana na ukitizama ni msitu ambao una chemchem kubwa sana kwa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika ripoti hii ya kamati imesema, mimi niseme tatizo la maji ni tatizo kubwa katika Mkoa wa Mjini Magharibi, hili tatizo lipo kubwa. Sasa mimi nimesema mafanikio tumepata mazuri huku nyuma, tulitia Ras al Khaimah visima 50, mabomba wametandika kuna mradi wa China ule visima wamesaidia Serikali ya China, lakini bado tatizo liko pale pale la maji mheshimiwa kwa nini. Miaka mitatu ya nyuma ukiisoma ripoti yangu hii hapa nimekuja nayo ripoti ya kamati na ya leo ukitizama haina tofauti,tofauti ni kidogo sana kwa nini inakuwa hivi hebu tujiulize kuna kidudu mtu gani hapa, maendeleo yanatakiwa yapatikane kwa asilimia 80 sasa hivi katika nchi yetu ya Zanzibar maji yapatikane, lakini leo unakuta bado ni ghali.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nimekwenda kwenye jimbo langu nimezunguka jimbo zima kila kona nimekwenda, nimezunguka

kila pahali nimekaa na wananchi kuongea mambo mengi, lakini jambo kubwa nilopata shida kwenye Jimbo langu la Mtoni Mhe. Mwenyekiti, maji shida. Kila ninapokwenda shida ya maji, sasa mimi najiuliza tunayo chemchem hapa ya Mwanyanya maji yanatoka hapa yanapelekwa Saateni, hawa wananchi maskini ya Mungu wanyonge hawana haki ya kutumia maji haya. Sasa Mhe. Waziri nakuomba na wewe pia ni mdau wetu unatokea kule Mkoa wa Magharibi, kwa hivyo naomba sana uangalie Mtoni, chemchem tumeizunguka tunaiangalia tu lakini maji hatupati, maji yanakwenda.

Mhe. Mwenyekiti, juzi kuna mwananchi mmoja alisema mimi bomba nitakuja kulikata, haya maji yote tuyapate sisi hapa. Nikamwambia usifanye usilikate hili bomba kwa sababu yanakwenda sehemu husika halafu yatakuja huku. Sasa mimi naomba Mhe. Waziri hebu tupe upendeleo basi haya maji ya chemchem ya Mwanyanya wapate wananchi wa Jimbo la Mtoni kwanza, watolewe japo *pipe* iweze kwenda majumbani mwao waweze kufaidika na chemchem hii.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, niseme kwa miaka mitano sasa hivi kipindi changu cha pili kuongoza katika nafasi yangu hii ya uwakilishi, lakini nimeweza kuweka matenki 40 kwenye jimbo langu la Mtoni, matenki ya lita 5,000, visima mbali mbali nimeweka kisima pale Kibweni Mshelishelini nimechimba kisima, nimeweka mnara na nimeweka matenki mawili tu ya lita 5,000 ambayo ndio yanawasaidia wananchi wa Kibweni Mshelishelini pale maji, na maji yale kama yatakata siku moja inakuwa hatari kubwa. Nimeweka pale, nimeweka juu kule Mwanyanya Kiboko yao matenki mengine mawili na kisima. Kwa kweli yanasaidia sana. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana mimi mradi wangu ni mdogo, huu mradi hauna uhakika. Leo unaamka asubuhi pampu imeshaungua tayari, unakwenda kesho umeme ukiambiwa haupo inakuwa shida.

Kwa hivyo, mimi nawaomba sana *ZAWA* tuangalie turejeshe maji kwa wananchi hawa. Kwa sababu huu mzigo nikiuchukua mimi. Wajumbe wamesema sisi hatuna uwezo, kweli uwakilishi wa kusema asilimia mia kwa mia jimbo langu litakuwa na maji mimi nitalifanyia sina uwezo huo tunajitahidi. Napiga siasa kwa wananchi wetu watuone kama tuna imani nao, lakini kwa kweli wakati mwengine inakuwa shida. Sasa naomba sana serikali yangu sikivu na Mhe. Waziri tusaidie suala la maji katika Jimbo la Mtoni. Mhe. Panya Ali alisema hapa zamani ulikuwa unafanya ziara kweli unakuja, unakaa na sisi na unatuuliza shida yenu nini maji, lakini sasa hivi umekata Mhe. Waziri hebu fanya hiyo ziara, hata ukiniambia kesho au keshokutwa tukayatembelee maeneo, tutakaa na wajumbe wa kamati ya siasa wenzetu viongozi watatusaidia suala hili, watatuambia shida ya maji ikoje katika jimbo hili. Mimi nakuambia Mhe. Mwenyekiti, lakini katika wizara zao kuna matatizo ndani yake, sasa sijui lakini Mwenyezi Mungu anajua, kama kuna tatizo basi ndio maana wananchi wetu hawapati maji, naomba ulifuatilie kwa kina kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi juzi katika ziara yangu kwenye jimbo langu nilikwenda mpaka skuli ya Mtoni pale mwisho Shehia ya Mtoni nilipofika kuna skuli pale ya primary skuli, mwalimu wa skuli akaniita Mhe. Mwakilishi umekuja imekuwa vizuri hebu nikuambie, shida yetu maji. Mimi niliwapa *tank* la lita 5,000 moja ili kusaidia maji, lakini matokeo yake maji hayafiki hakuna, sasa yanafika maji ya *ZAWA* lakini kidogo sana, yaani kwa wiki labda mara moja. Kwa hivyo, akaniambia unawaona hawa wanafunzi wa primary wakitaka kujisaidia wanakwenda kwenye nyumba za raia kujisaidia na watoto wari kabisa watoto wetu. Sasa kwenye nyumba ya raia hujui yule mwenye nyumba yake anapokwenda msalani yule mwanamke hujui ana nia gani, akija kumbaka yule mwanamke je. Sasa tizama hasara tutakayoipata hapa mtu kenda kuomba kwenda msalani anakuja kubakwa na mtu, kila mtu na

imani yake. Sasa tutapata hasara mtoto yule kuharibika maisha yake yote, huku tunakuwa tunakimbia huu udhalilishaji, lakini unakuta huku watoto wanabakwa ndani ya nyumba wakienda kujisaidia, pale Mtoni juzi Mwalimu Mkuu aliniambia

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana tuliangalie hili suala la maji ni suala ambalo muhimu sana wananchi wapate kulipata, mimi nasema maji hayataki hata matangazo Mhe. Waziri, ukimwambia mtu maji yapo atakulipa, watu wananunua maji sasa hivi. Kwa hivyo, mimi naomba sana uangalie sana Mhe. Waziri nakuomba kwa heshima zote tuangalie.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika hii idara yetu ya umeme *ZECO*. Mimi niwapongeze sana *ZECO* kwa jinsi wanavyojitahidi. Lakini pia niseme *ZECO* wenzetu wanadaiwa karibu bilioni 61...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, una dakika mbili.

Mhe. Hussein Ibrahim (Bhaa): Haya ahsante, namalizia Mhe. Mwenyekiti. Sasa hivi katika ripoti ya kamati imesema *ZECO* wanadaiwa karibu bilioni 61 deni halisi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nishukuru sana Muungano wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, deni hili ni kubwa sana, hakuna mdau yeyote anayedaiwa fedha hizi katika *TANESCO* na mimi nilikuwa mjumbe wa kamati siku hiyo nilikwenda Tanzania Bara *TANESCO* pale Ubungo, yule meneja akasema Mkurugenzi hebu huu mtambo mmoja chukuweni nyinyi tieni mafuta tu halafu basi. Kwa kweli sisi tujivunie huu Muungano wetu tuone kama wenzetu wanatustahamilia na Rais wetu anajitahidi sana kwenye suala hili. Kwa sababu umeme ni kitu muhimu sana katika maisha ya binadamu, maji na umeme lakini vitu vyote vinakwenda pamoja, ukikosa umeme utakosa maji na ukikosa

maji utakosa umeme. Kwa hivyo, mimi nasema maji na umeme ni vitu muhimu sana.

Kwa hivyo, mimi nampongeza Rais alikwenda Dar es Salaam akazungumza na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wameelewana ni jambo la kujivunia sana. Nawaomba wananchi wajuwe bila ya Muungano huu sisi tusingekuwa na umeme sasa hivi hapa, huu umeme ungekuwa umeshakatwa tuko kizani sasa hivi. Kama Muungano huu ungekuwa sisi na Kenya au Uganda basi umeme zamani ungeshakatwa. Kwa hivyo, mimi niwaambie wananchi tuwashukuru hawa viongozi wetu kwa hekimakubwa waliyokuwanayo.

Mhe. Mwenyekiti, pia niwapongeze sana *ZECO* kwa kupeleka umeme vijini kwa asilimia 80. Mimi nawapongeza sana jamani hawa Mhe. Mwenyekiti, wanafanyakazi vizuri sana, ukimtizama Meneja wa Shirika la Umeme ni mtu makini sana na ana busara sana, Meneja Hassan na ukimtizama Thabiti msaidizi ni mtu makini na ni mzuri sana anajua kuongea na wateja wake wa umeme hata kama una deni atakwambia hapa fanya moja, mbili na tatu, hukatiwi umeme lakini atakuwekea mikataba ili wewe ulipe, anajua kuwaweka wateja wake vizuri Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu wateja wa umeme wengi ni wafanyabiashara, kwa hivyo na wao wanafanyakazi kwa makini mimi nakupongeza Mhe. Waziri huyo ni Meneja mzuri sana na msaidizi wake ni watu wazuri sana watu wa umeme wanajitahidi kuweka ile misingi mizuri ya kushirikiana na wananchi wao katika suala hili la umeme.

Hata ukiangalia kwenye ripoti yao kwenye ukurasa wa 39 hapa wamesema wamekusanya bilioni 107, lakini matumizi yao ukitizama shirika kazi za kawaida bilioni 73. Kwa hivyo, mimi nasema hivi fedha nyingi zinakwenda kwenye mambo ya kuendesha hili shirika

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, muda wako umemaliza.

Mhe. Hussein Ibrahim (Bhaa): Ahsante. Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia bajeti hii na naomba sana wajumbe wenzangu tusipige mabuti kwa sababu naamini mambo mazuri yapo kwenye kitabu hiki na Mhe. Waziri mwenyewe kaandika. Kwa hivyo naamini mwakani tukija hapa naamini tutakuwa na mambo mazuri kabisa, hasa katika masuala ya maji. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hussein Ibrahim. Sasa namwite Mhe. Miraji Khamis Kwaza na baadae atafuatiwa na Mhe. Hassan Khamis Diaspora, na Mhe. Said Omar ajitayarishe.

Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwaza): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa wizara hii kwa kuweza kutoa jitihada zao na mchango wao mkubwa kwa kutufikisha pale ambapo azma ya serikali inataka kuelekea.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba kwa namna ya pekee nimpongeze pia Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano kwa ripoti yake na mengi wameyaeleza na kuyagundua ambayo sehemu kubwa ya serikali wakishirikiana kamati na serikali, namaanisha wizara wanaweza wakafika pahala pazuri na mambo yale yasiweze kuripotiwa tena huko mbele twendako. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti kama alivyoibua basi pia na miono yake washirikiane na Mhe. Waziri au viongozi wa wizara ili kusogeza mbele wizara hii lakini kusogeza mbele jitihada za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, maeneo mengi yameshachangiwa, naomba mimi niwapongeze wenzangu kwa hatua njema ya yale maeneo waliochangia, mimi nitakwenda moja kwa moja katika maeneo ambayo nahisi hayajaguswa na wachangiaji wengi. Eneo ambalo nakwenda mimi ni aya ya 77 utekelezaji wa nishati mbadala. Kwa mara nyengine naomba sana nipongeze azma njema ya serikali ya kutaka kutuondoa pale ambapo tupo sasa na kutuelekeza katika eneo jengine. Wameeleza humu katika kitabu kuna tafiti zinafanywa, lakini pia wametueleza na kampuni ambayo inatusaidia kutufadhili katika eneo hili. Kwa hivyo mimi naomba sana mashirikiano yawepo, lakini na tuangalie zaidi muda muafaka ambao zile tafiti zikamilike, lakini na kile ambacho wamekiona serikali iweze kukifanya. Kwenye eneo hili tutalisaidia sana Shirika la Umeme, tutawasaidia sana wananchi wa Zanzibar, tutawasaidia sana wakwezi na wakulima kama ambavyo Mhe. Hassan Khamis anavyosema.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka kujua katika eneo hili hawa wafadhili wetu katika nia njema tu ya kuweka sawa bajeti yetu na kutekeleza ile ilani ya CCM ni gharama za kiasi gani ambazo wametusaidia katika eneo hili, ili wenzetu waone basi yale matumizi ya fedha zinavyotumika na jitihada ya serikali. Kwa hivyo kwenye eneo hili nilikuwa naomba kwa kuweka sawa tu ule utaratibu mzima wa jitihada za serikali katika kufanikisha mambo mema kama haya ya kimaendeleo.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili lili tunajua sera tuliyonayo sasa ni sera ambayo inatulazimu sisi tununuwe umeme *TANESCO*. Sasa pia nataka nimuombe Mhe. Waziri lakini tujuwe tu ile azma ya serikali ya mapitio ya sera na kuibadilisha sera hii ili tuone inakuja kwenda sambamba na ile azma ya hiyo *study* inayofanyika huko tunakokwenda. Kwa hivyo tusije tukawa tunakamilisha kule, huku sasa tunasema tunapoteza miaka

mingine mitano ya sera tafiti zitatupeleka tu, kunako *sollar* kwenye ile *Installation* yoyote ya kuwa *power generation* tutaambiwa tu tuelekee wapi, lakini kabla ya kutuelekeza huko sasa hivi tuna sera ambayo inatuelekeza sisi kununua umeme *TANESCO.* Sasa haya mapitio ya sera sijui tuone Wizara kwa ujumla wake wameanza kuikalia ili tuone jitihada zile haya mambo yaende sambamba ili kupunguza muda tuna kiu sana ya kuwasogezea wananchi wetu maendeleo katika sekta hii muhimu sana. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri kunako eneo hili basi aje atupeleke vizuri.

Lakini pia naomba niende aya 76 ya kuwapa elimu wananchi wa masuala ya mafuta na gesi kwa mara nyengine naomba niipongeze Serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa adhma njema ile ya kukuza uchumi wa nchi yetu huko mbele tuendako, najua hii ni adhima njema tulilitewa sheria tumeipitisha na jitihada najua za Serikali na Wizara zinakwenda vizuri, lakini ndani ya Sheria ile tumesikia kutangazwa kwa Mkurugenzi Mkuu, Naibu Mkurugenzi wa *ZPRA* kwa kuanza ile shughuli ya kuratibu kwa kufuata sheria tuliyokuwa nayo. Lakini sheria inatwambia uwepo wa kampuni ambayo itasaidia ile ku-*regulate* masuala haya ya mafuta na gesi sijui kampuni ile imefikia wapi kwa niaba ya Serikali ambayo inakuja ku-*support* kazi hii.

Kwa hivyo naomba pia hapa Mhe. Waziri anipe majibu lakini katika sura ile ile ya kufanikisha ili kuona basi bajeti hii wenzetu ambao wanatusikilia zile jitihada njema za Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar za katika kuwatoa katika uchumi huu kwenda katika uchumi wa kati na baadae uchumi ule ambao tunautegemea vizuri zaidi, kwa hivyo naomba sana Mhe. Waziri katika eneo hili aje kunambia.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili hili niombe tu kwa hatua za mbele huko tunakokwenda kwa sababu adhma sasa ndio

kwanza tunaanza kuratibu na ishaalla Mwenyezi Mungu atatujaalia tufike katika hatua ya uchimbaji wa mafuta na gesi, lakini katika tatizo kubwa la uendelezaji wa uchumi wa eneo hili lazima tufike pahala tukishayagundua basi ule mpango mkuu wa serikali uelekezwe katika kuplani kutengeneza ile *refinal* ambayo tutasafisha wenyewe mafuta yetu, mpango ule wa kuuza *crude oil* baadae wakasafisha na nchi yetu ikaja ikauziwa tena si mpango rafiki maana sisi tutanunua tu hiyo *Demand* itakuwepo kwa sababu tunanunua vyombo tunaendelea kuafiri, vyombo vya usafiri vipo tunaendelea kusafiri. Sasa jitihada hii njema sasa tupo katika utaratibu wa huo uvumbuzi wenyewe lakini huko tunakokwenda nasema mpango mkuu uje uelekeze basi kwa kutafuta hiyo *refinal* ili tuone ina-*support* zile jitihada za moja kwa moja za kubakisha uchumi wetu kwenye nchi yetu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, pia katika eneo hili sina uhakika mzuri wa wenzetu wamefikia wapi katika suala la utengenezaji wa *data* kwa sababu lazima huko tunakokwenda lazima tuna *data room* ambayo inaweza ikaja ika-*support* masuala mazima ya uendeshaji wa maeneo haya ya mafuta na gesi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende eneo jengine la Shirika la Umeme kwenye aya ya 87 nimpongeze Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme kwa jitihada yake kubwa na kazi kubwa anayoifanya ya kusambaza umeme vijijini, juzi tumeona hata Pemba kule kuna jitihada za usambazaji wa umeme maeneo mengi yamewekwa umeme kwa hivyo katika hatua hii lazima tumpongeze Meneja Mkuu, tupongeze na viongozi wa Wizara pia katika ku-*support* eneo hili.

Pia naomba tu nitoe rai kwa sababu Shirika katika kazi kubwa wanazozifanya lakini fedha zile za kuwahudumia wananchi ile kuchangia tu katika sekta ya umeme zinabaki mikononi mwa wananchi wenyewe hasa kwa ufuatiliaji wa zile mita za zamani.

Sasa nilikuwa niombe tu waongeze jitihada ya kubadilisha mita zote za Unguja na Pemba kutoka katika matumizi ya umeme wa nitumie kwanza halafu ndio nilie wabadilishe mita mtu hataki huduma ya umeme akachangie maana kulipa umeme ule kwa asilimia mia moja kama ambavyo inatakiwa hatuwezi, lakini ile kuchangia basi akachangie ile asilimia ambayo tunajua Serikali inabeba sasa ile aina tu ya jitihada ya Shirika la Umeme basi waelekee huko, waelekeze nguvu zao huko wabadilishe mita, mita zote ziwe *pre paid* watu walipe wakatumie tutaweza ku-*control* lakini pia tutapunguza ile namba ya wafanyakazi ambao tunawaajiri katika huduma ile ya kata umeme huku, leo kakate huku sasa wale wafanyakai wanaondoka kwa sababu umeme ukimalia katika matumizi yako unakatika wenyewe, mteja mwenyewe atakwenda kuufuata umeme na sio sasa tunaendelea kukimbizana na wateja sugu ambao wakati fulani hawaitakii mema hata jitihada za kuwepo hilo Shirika la umeme lenyewe.

Lakini sasa naomba nielekeze katika eneo la aya ya 107 kunako uhifadhi wa mazingira. Mhe. Mwenyekiti, katika eneo ambalo tunatakiwa tujitahidi sana ni eneo hili la uhifadhi wa mazingira kuna idara kule ya mazingira katika Wizara hii, tumeona maeneo mengi tunaruhusu kuchimbwa ikiwa katika kupitia uchimbaji wa mchanga lakini kupitia na kazi zetu nyengine za kimaendeleo. Lakini jitihada za urudishaji wa maeneo haupo sasa yanatokezea mengi katika utaratibu huu wa uhifadhi wa mazingira, ukichukua hilo eneo la mchanga tu lenyewe linatoa ada ya urejeshaji wa ardhi ile hatuoni ardhi zile kurejeshwa.

Sasa fedha hizi zinatumika wapi sasa tuone jitihada za pamoja Wizara ya Kilimo inapofika pahala kwenda kutoa eneo la kuchimba mchanga ada ile ambayo inatakiwa irudi katika urejeshaji wa ardhi basi iende Mazingira *direct*, pesa zao tuwape wafanye kazi ya kwenda kurejesha ardhi ile, mimi naamini tukichimba ardhi ikirudushwa katika mfumo ule ule wa

kimazingira tutafikia katika hatua salama ambayo nchi yetu haiwezi kukumbwa na majanga ambayo tunaweza tukayaepuka.

Lakini pia naomba niungane na wenzangu hapa tu nitaungana na wenzangu ambao wametangulia tumeona ujenzi ambao una nia nzuri, lakini nia ambayo sasa inaanza kutugharimu katika eneo la Mtoni. Mhe. Hussein Ibarahim Makungu (Baa) hapa kazungumza mimi jirani yangu akitoka jimboni kwake anaingia kwangu nikitoka kwangu mimi naingia jimboni kwake, lazima unapata taarifa zote za utekelezaji wa mazingira yale. Eneo lile linalofukiwa sasa litazidisha pia matumizi ya ardhi kuelekea katika bahari yetu maji haya kweli yatapanda athari ya mwanzo lakini Serikali imeplani vipi katika kuja ku-*control* ule uhalifu kwa sababu tuna *Depot* pale na hatuna *Depot* nyengine, sisi tukiruhusu tu mazingira ya kulinda ile *Depot* yetu yako wapi sasa tuone tu mazingira ya uwekezaji ni ya nia njema, lakini mazingira pia ya kulinda vile vianzio muhimu vya nchi pia ni nia ya pili.

Sasa ilikuwa tuone tu katika mazingira yale tukiendelea kuruhusu tu ardhi ile kutumika na ile *Depot* yetu tutalilindaje sasa mazingira hayo ndio ninayoyazungumzia mimi, wananchi Mhe. Hussein Ibarahim Makungu (Baa) kawazungumzia na washasikia na naamini kura zao watampa tu, lakini eneo ambalo nalizungumza mimi ni miundombinu ya Serikali ambayo itakuja kuathirika katika mazingira ambayo si rafiki kukaribisha ule uwekezaji ambao utakuwa unakaribia miundombinu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kwa sababu nimeshasema maeneo mengi yalishachangiwa na mimi sitaki kurejea yale ambayo wamechangia wenzangu kwa sababu wote wana nia njema ya kuishauri Wizara hii, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia, lakini pia niendelee kuwapongeza viongozi wa Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wanakabiliana nayo Mwenyezi Mungu atawafikisha pale ambapo panastahiki inshaallah.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Miraji sasa niniamuita Mhe. Hassan Khamis Hafidh (Diaspora) na baadae atafuatiwa na Mhe. Said Omar Said ajitayarishe.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii ya kukushukuru kwa kunipa muda huu wa kuongea ikiwa ni saa 7.30 kwa saa za Afrika ya Mashariki, leo nitaongea lakini kwanza kabisa naomba kumpongeza sana dada yangu na Naibu Wake Mhe. Muwakilishi wa Kijini wanafanya kazi nzuri sana, ingawaje Wizara hii ni miongoni mwa Wizara ngumu katika nchi hii ngumu sana na hasa ukiangalia Wizara hii Masikini ya Mungu kaachiwa majuju na majuju chungu nzima kaachiwa Mhe. Waziri na Naibu wake, lakini kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana, na mimi muwakilishi wa wananchi jimbo la Welezo nachukua fursa hii kumshukuru sana miongoni mwa watu walionisaidia mpaka maji yameanza kuchuruzuka japo kidogo kidogo hayatoki yanavyotakiwa, lakini japo kuchuruzika japo kidogo kule Welezo amenisaidia hayatoki kama yanavyotakiwa lakini yameanza kuchuruzika.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo matatu makuu ambayo yanawagusa moja kwa moja wananchi wetu katika nchi hii, kwanza tulilizungumza hapa kikiri kikiri ilikuwa kubwa hapa ilikuwa Mnazi Mmoja, lakini mbili ardhi lakini tatu maji haya mambo matatu makuu Mhe. Mwenyekiti, ndio yanayoifanya Serikali yetu isemwe na wananchi na isemwe vibaya. Kwa bahati mbaya sana haya mambo mawili yote japo kunako wizara anayaiongoza dada yangu Mhe. Salama Abdull Talib ambayo ni maji na ardhi, kwa bahati mbaya sana mawili makubwa yote anayo yeye.

Mhe. Mwenyekiti, sasa baada ya pongezi hizo naona imefika wakati wa kuaza kuchangia hotuba hii iliyoletwa hapa ya bajeti

ina program ya usimamizi, upangaji wa matumizi ya ardhi. Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu Zanzibar ni kisiwa tena kisiwa chenyewe kidogo sana kimeweka Wizara ya Ardhi ambayo kazi yake kama sikosei ni kusimamia matumizi mazima ya ardhi ndani ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nasoma hichi kitabu ndani ya Wizara hii kuna idara ya Ardhi, Hatimiliki, Haki za matumizi ya Ardhi, Ofisi ya Mrajis wa Ardhi, Idara ya Upimaji, Idara ya Mipango miji na vijiji, Kutatua migogoro ya Ardhi yote ardhi ardhi ardhi. Miongoni mwa rasilimali ya mwananchi rasilimali ya nchi, rasilimali ya mtu au watu ni ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, si siri sote mashahidi kuna mambo manne au matatu makuu yanayoifanya Zanzibar iwe mdomoni sana kuhusu suali la ardhi namtaka Mhe. Waziri anisikilize kwa umakini hapa, imekuwa ni tabia ya watu Zanzibar bila ya kimeme kuchukua ardhi za watu mtu akishakujiona yeye ana mbavu kidogo na huyu mnyonge kidogo basi anaipiga pute ardhi yake Mhe. Mwenyekiti kumekuwa na malalamiko mengi nchini mengi hasa jamaa zangu huko shamba utaambiwa mtu fulani ameshachukua ardhi yetu, mengi mpaka unatia huruma na ardhi ndio rasilimali ya mwananchi wa Zanzibar ndivyo Mzee Karume alivyotwambiya ardhi yetu hii, mali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya Mapinduzi asilimia 13 ya watu wanaoishi Zanzibar ndio waliokuwa wanamiliki ardhi asilimia 13 tu, yaani ardhi ya Zanzibar ilikuwa inamilikiwa si zaidi ya watu 300 waliokuwa wanamiliki ardhi katika watu laki tatu watu walikuwa wengi lakini ardhi ilikuwa ukiitaka lazima uende kwa bwannyenye tena kazi yako ni kulima tu, bwannyenye akukatie kidogo ulime ukamlipe. Namshukuru sana Mzee Karume katuletea Mapinduzi na baada ya Mapinduzi akasema ardhi ni mali ya wananchi akatugawia eka tatu tatu kwa wenzetu ziko nchi bado mambo hayo yako, lakini sisi alhamdullillahi leo kwetu hayapo hata mie bibi yangu kanirithisha ardhi shamba kanirithisha

zamani ilikuwa hilipati mtu kama mie nitalipata wapi hilo shamba, ilikuwa ardhi yote wanayo watu wachache.

Mhe. Mwenyekiti, sasa watu wamechukua ardhi za watu hilo la kwanza, lakini la pili kuna watu ndani ya nchi hii wana maeneo hayaa mwisho mtu mmoja ana maeneo ishirini anatega bei, mtu mmoja ana eneo utaambiwa hapa mpaka kuleeee kule hukujui, pale Uroa kuna pahali unakwenda kuna pahali unaendesha gari mpaka uchoke bado unaambiwa eneo la mtu mmoja hee aloona bibi yangu umezaa! Inakuwaje eneo hilo lote ukalichukue wewe wewe ndio nani ebwana hii nchi ya watu hivyo ya wananchi, lakini cha tatu ujenzi holela, mimi nimezaliwa pale Amani napata umri wangu wa utu wa akili naijua nchi Zanzibar mwisho barabara ya Amani huku kunakoitwa Magogoni, kunakoitwa sijui wapi huku kote huku mimi namjua mtu mmoja tu alikuwa akikaa akiitwa Kankuni peke yake ndio akikaa na kijumba cha roshani, lakini leo Mhe. Mwenyekiti kumejaa watu hawana mwisho. Kujaa watu sio tatizo lakini kinachosikitisha Mhe. Mwenyekiti kwamba hata baiskeli ukipata kupitisha pia haipiti hii ni aibu.

Mhe. Mwenyekiti, Mji wa Kwahani, Mji wa Makadara, ni mzuri uliojengwa ukoloni kuliko mji wa leo uliojengwa miaka 25 nyuma huko Kwerekwe sijui wapi hakupiti hata baiskeli Mhe. Mwenyekiti na Wizara ya Ardhi ipo, lakini chengine kinachosikitisha mtu anaamka asubuhi ashapata pencheni au ashazipata pesa alikozipata anakokujua yeye anakamata kamba yake anasema anaanza kujenga hajaenda kwa Sheha, hajenga popote anajenga mpaka nyumba inafika juu hivyo hii nchi haina sheria, hivyo hii nchi haina taratibu, hivyo hii nchi haina weyewe ukajenga tu bila ya kupata hata kibali kwa sababu umeshapata pesa. Haiwezekani Mhe. Mwenyekiti nchi hiyo Duniani hichi ni kisiwa kitakwisha, kuna taasisi moja ilifanya *Research* katika nchi za visiwa ikasema Zanzibar Ardhi yake ni *Soft Touch* yaani kila mtu bila ya kujali anafanya anavyotaka.

Mhe. Mwenyekiti haya yameshatutosha hasa hii Unguja itakwisha mwisho pa kuzikiwa itakuwa hakuna hivyo tutakwenda kuzikwa wapi, mkeshakumaliza Uroa, Marumbi, Mchangani, Dunga, Uzini, Mitakawani tutakwenda kuzikwa wapi lazima mtu akitaka kujenga afuate taratibu apimiwe asiyefuata taratibu lazima Serikali ichukue hatua basi itakuwa kila siku tunatunga sheria tu sie hazitumiki. Mhe. Mwenyekiti, Fuoni humo mote mmejengwa juzi ardhi yake ni ya rutba lakini mmejengwa kiholela sasa hivi hata pa kupitisha baiskeli huna na watu wanaendelea kujenga na tunawatizama tu wanaendelea kujenga hawafuati sheria wala taratibu halafu tuje kusema wameshaharibu tuwabomolee.

Mhe. Mwenyekiti, wahenga wamesema usipoziba ufa utajenga ukuta naomba sana uniambie Mhe. Waziri una mkakati gani wa kuzuia haya majenzi kiholela la kwanza kwa sababu tumeshachoka nayo la kwanza yanatutia aibu, yanatutia hasara kwa sababu ardhi inatumika ovyo yanaifanya Zanzibar isiwe nchi ya utalii kwa sababu unamchukua mtalii unasema leo hebu tukatembee huko ndani ndani pakupita huna kila mtu kajenga anavyotaka na wasi wasi wetu mkubwa tutakuja kuchomwa hapa kwa sababu wa kuzikiwa itakuwa hapana tena tutakuja kuchomwa. Huko kwa kina Mhe. Issa Gavu kote kushajengwa inakuwaje haiwezekani? jambo jengine Mhe. Mwenyekiti lazima tufuate mambo kwa taratibu, sasa uje uniambie Mhe. Waziri una mkakati gani wa kumzuia mtu asiye na kibali asiiguse ardhi hatua gani utazichukua maana mapesa ndio tunakupitishia haya kila siku mwaka jana niliyasema haya haya ikesha tukapitisha sijaona hatua yoyote iliyochukuliwa watu wanajenga ovyo ovyo hii Unguja itakwisha na tushachoka sasa uje kunijibu.

Lakini la pili hawa watu hawa wenye maardhi hayana mwisho mtu mmoja ana ardhi ishirini mtu mmoja ana ardhi hee oya wee kuliko Rais wa nchi fulani haina mwisho yote yake inakuwaje,

yeye nani haiwezekani ardhi ni mali ya watu wote, ardhi ni mali ya Serikali uje unambie una mkakati gani Mhe. Waziri wa hawa watu wenye kumiliki ardhi yoote wamejichukulia wao tumechoka wanategа bei hatuwezi. Mhe. Mwenyekiti ukienda huko hasa shamba za fukwe Uroa, Marumbi, Michamvi kote unaikuta ardhi kila mtu achanganganyia kama kuku anolalia haiwezekani, lini utazichukua ulitangaza kuzichukua hapa Mhe. Mwenyekiti watu wenye viwanja hapa Tunguu mimi nakupongeza ndo anavyotakiwa mtu kusema ndo waziri ati, lakini hawa wenye maardhi yasomwisho utazichukua lini, usizichukue za panya mpunga tu aaaa na hawa manyangumi maana mtu ana ardhi hizi ardhi za nyangumi utazichukuwa lini. Lazima unijibu Mhe. Waziri lini utazichukuwa hizi ardhi utugaiye na siye wanyonge na sisi tunataka tukapate upepo baharini ati. *(Makofi)*

Utambie lini ukazichukuwe utugaiye sisi wananchi ardhi mtu ana ardhi hana mwisho, akenda mwekezaji kutaka kununua ardhi anabei hata pesa kuzitaja sizijui kaiweka tu haitumii, haikodishi, hampi mtu anategа bei alaa anategа bei mpaka lini. Muwekezaji Mheshimiwa nataka kupitisha sera ya nchi hii, ardhi yoyote ambayo ipo na muwekezaji kaja nchi hii anataka na yuko muwekezaji *serious* si mbababishaji apewe, kuna maardhi yamekaa huko wawekezaji wanatafuta ardhi hawapewi imekuwa kama wale maji moto wananganganiа embe kuila hawezi. Mhe. Mwenyekiti uje unambie hawa manyangumi wenye maardhi huko, mtu mmoja anaardhi za hoteli za viwanja vya hoteli 20 utavichukua lini. Vyama wafanya mpunga ulitangaza utachukuwa februari tunashukuru hujachukuwa vya hawa manyangumi utavichukua lini.

Mhe. Mwenyekiti chengine utawasaidiaje hawa ndugu zetu Mhe. Mwenyekiti Uroa, Marumbi, Michamvi, Paje, Jambiani walitoa ardhi zao bila ya kujua wakawapa wawekezaji leo hii babu yangu mnyonge wa Mungu hakuingia ubia masikini kulikuwa hakuna

hiyo sera, lakini tajiri anatajirika kwa ardhi ya babu yangu kazi ya Serikali ni kusaidia wananchi pale wanapoteleza na wanapo kosea. Mhe. Mwenyekiti nataka unambie zile hoteli zilizochukuliwa kihilba za mahoteli za wazee wetu zimechukuliwa kihilba leo, shamba kama Paje, Jambiani kwa kuzikiwa kuchakuwa hakuna mtu anazikwa lazima lichongwe jiwe halafu ndo unatiwa mtu.

Unazikwa kunako kiwanja cha mpira kwa sababu zimechukuliwa ardhi zote zinafanywa hoteli, lini utakuja na utaratibu wa kutaka kuwasaidia na kuwaokowa hawa watu wetu Mhe. Mwenyekiti ndo ardhi ishachukuliwa na wazungu, na watu wengine wajanja. Mhe. Mwenyekiti naomba sana uje kunijibu haya ili nipitishe bajeti haya kama si hivyo Mhe. Mwenyekiti kama hujanijibu haya utakuwa vigumu leo dada yangu tena nampenda sana hasa Waziri na Naibu wake wote marafiki zangu lakini aaaa, kwa jinsi ardhi hii inavyojengwa kiholela, kwa jinsi manyangumi haya yanavyo ardhi kubwa, leo nitaweka msuli mkubwa Mhe. Mwenyekiti aipiti bila ya kujibiwa mambo hayo.

Mhe. Mwenyekiti nikitoka hapo nnakwenda kunako ZAWA. Mhe. Mwenyekiti nawapongeza sana watu wa ZAWA wanajukumu la kutupa maji tunywe na kukoga, lakini nataka taifa litambuwe nataka na wewe Mhe. Waziri utambuwe na kila mtu atambuwe kwamba maji, visima viko Welezo. Maji wanaokoga watu wa mjini wakanukia wakangara yako kwetu ngambu Welezo na hapo ukoloni ilikuwa inaitwa *Welzon* maana yake eneo la visima kwa wale wasiojua, naomba nitowe darasa kule Welezo mkoloni kulikuwa na *Welzon* eneo la visima. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti umenisaidia kidogo maji yanachuruzika kule Welezo lakini miye ndo nnovisima vyingi vya maji wanaokunywa watu wa mjini wanaokoga watu wa mjini, nashukuru kwangu yanachuruzika hayatoki kama yanavyotoka mjini, yanachuruzika lakini nina tangi kubwa lile la maji lipo kwangu, ninalowapa watu

wote wa mjini hee, juzi wananchi wangu wakanita wakasema Mheshimiwa ndo tulokuchaguwa Uwakilishi nikawambia kweli walikuwa 10 hao, mkanichagua mimi.

Mhe. Mwenyekiti namwambia Mhe. Waziri lile tangi lina paipu kubwa nimepita limekwenda mjini kwangu maji yanachuruzika lakini hivyo visima mara paipu zimeharibika, mara mambo chungu nzima lini atantobolea awambie watu wake wa ZAWA antobolee lile tangi kubwa Mhe. Waziri nakwambia unisikilize, unitobolee lile tangi kubwa lilopeleka mjini ili watu wangu wapate washakuwa wanachukiwa mara imeharibika mara kumefanywa hivi, na lile tangi haliharibiki hata siku moja. Yalikuwa Welezo masingi Mungu watu wangu hawapati lini utanitobolea, unitolee kimpira kidogo tu, wallahi watapata watu wangu wote na hii shida ya maji Welezo itaondoka na halafu ingalau watajisikia wale watu wa Welezo kama maji yapo kwetu na sisi tutafaidika.

Lakini Mhe. Mwenyekiti umenisaidia lakini watu wa Welezo mara yamefungwa mara yameharibika mara yamekatika na maji ya *permanent* yako kwao Mheshimiwa haiwezekani, paipu lile la chuma maana washafika kunambia wananchi bora tuchukuwe sururu tukalipige kwa sururu nikawambia mimi aaa Waziri wa Maji, mtu muungwana sana dada yangu najua nikimwambia hakatai na nitakwenda kumwambia naitakuwa kwa hiyo sina wasi wasi kwa hilo Mhe. Mwenyekiti sina wasi wasi kwa hilo kwa Mhe. Waziri na Naibu wake na Katibu wake Al Khalil Mirza naamini wazi kwa walivyo makini watakwenda kuntobolea lile tangi kubwa linalowapelekea maji watu wa mjini ambayo watu wa Welezo hawayapati na nataka nimuhakikishie watu wa Welezo wakitobolewa tangi lile shida ya maji itakuwa imekwisha, itakuwa imekwisha.*(Makofi)*

Lakini chengine nataka niwaombe watu wa maji Welezo ndiko kwenye paipu nyingi lakini pia kuna vidimbwi vingi vya maji, kuna paipu nyingi na vidimbwi vingi sijui ulikuwa hata hujawa Waziri, lakini inaonesha hawa walionunua mabomba mwanzo walinunua mabomba feki si siri, nasema tena Mwakilishi nafikiri ulikuwa hujawa Waziri, Naibu Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika nne.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Eee sasa Mhe. naomba sana yale mabomba kule kuna vidimbwi vya maji wanapopigiwa ZAWA yamepasuka wafike haraka wakanyatengeneze ni hatari umenifahamu. Mheshimiwa naomba kuchukua fursa hii pia kumpongeza Meneja wa Shirika la Umeme anafanya kazi nzuri kaka Hassan somo yangu Hassan kazi anafanya lakini achukuwe tahadhari na ajitahidi na watu wanaom-*supplier* vitu wangine wanampiga changa la macho masikini ya Mungu bila ya yeye mwenyewe kujua wajanja wengi ndo wanaomtia mashakani humu, kuna Waheshimiwa wengine hasa Abdalla Diwani akaja akasema mengi kuhusu Shirika la Umeme. Kwa hiyo naomba kukuomba Mhe. Mkurugenzi achukuwe tahadhari na wale watu wanao-*supplier* vitu wanaompelekea Shirika la Umeme ndo watu wa humo humo Shirikani wanaofichua karatasi wakampa waheshimiwa hasa Mhe. Abdalla Diwani tena akapata kuja kumsema humu lakini anafanya kazi nzuri Mheshimiwa nimefahamika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti nikitoka hapo nakwenda kwenye Mazingira Idara hii ipo kwako Mheshimiwa kuna mambo ya aibu nna *document* hii kule Pemba msitu wa ngezi 1968, alikuwa Waziri wa Kilimo anaitwa mtu mmoja anaitwa Mzee Hassan Nassor Moyo alifanya *declaration* kwamba msingi wa ngezi ni Msitu wa Hifadhi ya Taifa, na tarehe 06 Agosti, 2004 alikuwa Waziri wa Kilimo anaitwa Mohamed Aboud Mohamed ambaye tunaye hapa

alikuwa ndo Waziri wa Kilimo alitia saini *document* hii hapa, akasema huu ni msitu wa Hifadhi ili kuzifuta *declaration* mbili hizi za Mohamed Aboud Mohamed na Mhe. Hassan Nassor Moyo inahitaji Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa mujibu wa sheria ndo aifute tena kwa kupoteza sifa ule Msitu sio Msitu wa Hifadhi, lazima uwe kuna sifa umepoteza halafu Mhe. Rais atowe tangazo kunako ndo Msitu umefutwa ili kufanyike jambo jengine *document* nnayo hii. Lakini leo tumeletewa nnayo makaratasi mengi tangu ya kesi mna kambi mle kama sikosei ya JKU. Pia haithamini kwa sababu kuna fukwe wajanja tayari wameshamenyeza menyeza rupia huko kushakatwa viwanja lile eneo.

Hii si sahihi hakuna *document* iliyoletwa kusema lile eneo limepoteza sifa sasa linaweza kukatwa viwanja, hii si sahihi kwanza si sahihi kwa mambo mawili, kwa kizungu kuna kitu kina *sub-sibiliting environment* endelevu. Mheshimiwa neno sitaendelevu maan yake tutumie siye na kitumie kizazi kijacho leo hii kama kila kitu tutatumia siye tumekaa janyoka tutakuwaje mbona sisi tumevirisi kutoka kwa wazee watu nataka Mhe. Waziri anambie atamke leo hapa vile viwanja vilivyokatwa kule Pemba Ngezi kunako Msitu wa Hifadhi uliokuwa *declare* na Mawaziri wawili atangaze leo hapa kama si hivyo nitazuia fungu. Namjua dada yangu ni makini, ni mahiri na anaweza kulifanya hili nataka avae mkaja atangaze leo, kwamba vile viwanja vyote vilivyokatwa Ngezi kunako Msitu wa Hifadhi ni batili. Namtaka atangaze leo namjua anaweza na uwezo huo anao kapewa kisheria na kikatiba na Mhe. Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa niko mwisho kabisa usipate shida.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. muda wako umemaliza umalizie lakini muda umekwisha.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. nakushukuru sana mwisho nawasifu sana watu wa ZURA wanafanya kazi nzuri waendelee kufanya wanavyofanya kazi, lakini Mheshimiwa la mwisho kabisa namuomba sana Mhe. Waziri kuna hii kadhia ya Pakachi japo ni mzungu na nchi yetu inaendeshwa na utalii, tunawataka watalii waje ili tuweze kuimarika kupata pesa za kununua madawa hasa pale Mnazi Mmoja ambapo Serikali inatowa pesa nyingi bado huduma si nzuri. Pakachi kuna muwekezaji tayari wajanja fulani wazalendo wa nchi hii kwa kushirikiana na watu wengine wanataka kumdhulumu muwekezaji yule hii si sahihi, wawekezaji tunawataka sisi tumeishi nchi hii na wengine wahajadhulumiwa na hakuna haja ya kuwadhulumu. Namuomba Mhe. Waziri afanye anavyofanya haki ya pale Pakashi itendeke yule mzungu apewe aendeleze biashara ya utalii awe balozi wetu mzuri kwa kutangaza nim-Scotland yule Uingereza na Scoth na dunia nzima kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti baada hayo machache namuomba sana Mhe. Waziri aje kunijibu nachangia asilimia thamanini na tano, kumi na tano asilimia nina *reserve* Mhe. Mwenyekiti ndio nitakapokuja kuunga mkono hoja, Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja asilimia thamanini na tano, kumi na tano ya *reserve* ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, Waheshimiwa kwanza kabla ya kuendelea na kuchangia naomba nitowe tangazo hili hapa. Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wanaomba baada ya kikao kuakhirika kikao hichi cha muda huu wafike katika kikao kitachofanyika cha wana CCM, Wajumbe wa CCM katika ukumbi wa juu, mara baada ya kuakhirika kikao hichi ahsanteni. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea namwita Mhe. Said Omar Said na baadae akifuatiwa na Mhe. Suleiman Sarahan ajitayarishe.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwanza kabisa nimshukuru Mwenye ezi Mungu mwingi wa rehema alojaalia mzima na kuniwezesha kuwepo katika kikao hichi cha leo.

Nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii ya kutowa mchango wangu japo dakika mbili, tatu kuhusu Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Sitokuwa na mchango mkubwa na wala sitotumia dakika ambazo nina kawaida kuzitumia maana yake nitatumia dakika chache tu.

Basi nianze kumpongeza Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa jinsi alivyowasilisha Hotuba hii, lakini nimpongeze Mhe. Naibu Waziri nimpongeze Katibu Mkuu niwapongeze na Watendaji wao kwa kazi kubwa wanayoikabiliyana nayo kwa kila siku kwa kuweza kuchupa matuta na kuhepa hepa silaha za kila wakati.

Mhe. Mwenyekiti nataka nianze ukurasa wa 40 unaoeleza usambazaji wa umeme vijijni, hapa nataka kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kufanya ziara katika jimbo langu na hususan katika shehia ya sizini, na pia nakumbuka kwamba alipokuja Mhe. Waziri katika jimbo hilo, nakumbuka kumtambulisha maeneo ambayo bado hayajafanikisha kwa masuala ya umeme, nilimtambulisha maeneo matatu katika eneo la Sizini ikiwemo Mliyani ambao iko eneo la Sizini, Mnazi Mmoja ambayo iko eneo la Sizini na Chaguani pia iko katika eneo la Sizini kwa hivyo hapa nazidi kumkumbusha Mhe. Waziri kama alivyowambia wawe wananchi aliowakuta pale, sababu walipojua kwamba anakuja Waziri wakawa wana hamu nawe waje wamuone waziri wao. Wakaja pale wakamsubiri na wakaonana naye na wakamsikia kwamba awahidi kuwa umeme katika mji mitatu hii, au vijiji vitatu hivi utapatikana kwa muda mchache tu. *(Makofi)*

Kwa hivyo Mhe. Waziri nazidi kukumbusha kwamba katika bajeti hii, iwe ni miongoni mwa vijiji ambavyo vitafaidika kwa masuala ya umeme, lakini sambamba na hilo pia ningependa nichukuwe nafasi hii ya kukuunga mkono maelezo yako yaliyomo kwenye katika kitabu, nimeona katika kiambatisho D maelezo ya sehemu ambazo zimefaidika na *transformer* moja ni Kinazini nimeiona humu kwamba Kinazini ni sehemu moja ambayo au ni kijiji ambacho kimeekewa *transformer*.

Mhe. Mwenyekiti, Kinazini ni kijiji ambacho kipo baina ya Wingwi na Finya apo katikati apo ambao kijiji hicho kiko katika jimbo la Wingwi. Mhe. Mwenyekiti mimi nina masikitiko makubwa hapo kwa Mhe. Waziri kwa sababu taarifa hii anayoitia humu *transformer* iliyowekwa toka mwaka jana karibu, sasa imo humu kuwa Kinazini ipo *transformer* hasa sasa basi itakaa *transformer* tu hiyo hiyo yataka ibakie hiyo hiyo *transformer* ya Kinazini Mhe. Mwenyekiti na mwakani tuje tusome hivi hivi Kinazini iko *transformer* akaa. Mheshimiwa nakuomba sana kwamba katika bajeti hii hiyo *transformer* ambayo ishafungwa basi itumie, na wananchi wa Kinazini wapate faida ya Mapinduzi yao ya Zanzibar, kama wanavyofaidika watu wengine.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika programu ndogo ya Utawala wa Ardhi, hapa ningemuomba sana Mhe. Waziri alifafanulie haya nitakayomuleza haya masuala wakati wote huwa napambana nayo jimboni, sina jibu isipokuwa jibu nitalipata kwako. Mhe. Mwenyekiti ninalolitaka nifafanulie ni kuhusu eneo au ardhi ya wananchi wa Wingwi ambayo wameimiliki kwa kipindi kirefu kwa muda zaidi ya miaka 20 na wakaanza kupanda miti ya kudumu na imo, ambayo miti ya kudumu nisehemu ya waraka kwa sababu ikiwa mtu eneo hilo si lake na akapanda miti ya kudumu ikafika miaka 20 hajatokea mtu halaani eneo hilo kwa hivyo ile miti ya kudumu ambavyo inazaidi ya miaka 20 ni sehemu ya waraka.

Mhe. Mwenyekiti, eneo hilo walikuwa wananchi hao wanalitumia kwa ushirika wa kilimo na eneo hilo lipo karibu na kuingia Msitu wa Micheweni kabla ya kufika Msitu wa Micheweni upande wa kulia upo uwanda ndiyo eneo hilo walilokuwa wakilitua wazee hao au wananchi hao kwa ajili ya kilimo cha ushirika.

Mhe. Mwenyekiti, siku miongoni mwa siku wakatokea watu wa Kilimo wakawambia hii sehemu yenu tunataka mtugaiye sehemu ndogo tunataka kufanya utafiti, watu wa Kilimo wanawaleza wenye shamba. Wakawagaiya sehemu ikawa wale maafisa wa kilimo anakuja siku walikuwa wanafanya utafiti gani. Lakini baadaye ukaeleweka kumbe utafiti wenyewe ni huu wa kuwanyang'anya. Hawakutoa taarifa kwamba tunafanya utafiti wa kitu fulani, tumegundua kitu fulani, ndiyo maana ya utafiti. Eneo lile ni lao wao watu wa Wingwi lakini walilokuja kuliona wakahamishwa pale wakaambiwa kwa taarifa yenu kuanzia leo eneo hili muondoke eneo hili limeshapewa muwekezaji rasmi. Wakauliza muwekezaji yupi, wakaambiwa huwo ni uwamuzi wa serikali na serikali huwa haihojiwi.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi hawa ni wananchi ambao wenye kuipenda sana serikali yao ni wananchi ambao ni wenye kuiheshimu sana serikali yao, hilo tu ndilo lilowafanya wakaondoka. Lakini wanaloomba baada ya kuambiwa kuwa ni serikali ndiyo inayowanyang'anya ndiyo pahala ambapo ndipo tulipoka karibu kufahamu mimi hapa nusu ya maisha yetu tumeyapata hapa, leo serikali ndiyo imetunyang'anya haya. Lakini kwa kuwa kuna miti yetu humu yakudumu tunahitaji angalau tupate fidia. Sasa hii fidia tutaipata wapi, wakaanza kwenda huku na huku, wakenda Kilimo wanaambiwa sisi shamba lile halituhusu. Wakienda Wizara ya Ardhi wanasema sisi hatuna habari hiyo wala hatulijui shamba hilo. Ikawa wanapigwa dana dana hawajui kama wako juu au wapo chini wapo tu wanayumba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo wamenituma kuja kuwaulizia kwako, kunyang'anywa wameshanyang'anywa sawa, ni serikali yao wanaiheshimu lakini kama siyo serkali yao ingekuwa hapatoshi. Wamenambia kwamba tuulizie kwa Mhe. Waziri hii fidia yetu tutaipata watu na tutaipata lini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Said, sasa namwita Mhe. Suleiman Sarahan na baadaye akifuatiwa na Mhe. Hidaya Ali Makame.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia machache ya Wizara ya Ardhi.

Awali ya yote baada ya kuungana na nanyi kumshukuru Mwenyezi Mungu pia nimpongeze sana Dkt. Ali Mohamed Shein Katika jitihada zake za makusudi za Wizara zote lakini hata hii Wizara ya Ardhi katika kuisaidia kwa hali na mali katika mambo tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, pia niwashukuru Wajumbe wangu au wapiga kura wangu wa Jimbo la Chakechake kwa kunipa nguvu ya kuwa kila siku Mwenyezi Mungu amenijaali kufika hapa na kutoa mawazo yangu. Mimi leo sitokuwa na mengi sana mpaka ukafika kunizuia muda lakini nataka kidogo na mimi nichangie.

Kwanza nataka nimpe pongeze Waziri wa Ardhi, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wote wa Wizara hii kwa ushirikiano wao mzuri na kutoa kila nafasi katika jitihada zao za kuendeleza wizara hii. Pia nataka niunge mkono Kamati ya Ardhi

na Mawasiliano ambayo imewasilisha ripoti yake hapa na mimi naunga mkono kwa yale yote waliyoyasema.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka Waziri atakapokuja aweze kuchambua kidogo kwamba ni lini atakuwa amefanya upembuzi yakinifu katika sehemu ya Fumba ambayo ni sehemu ya Uwekezaji aweze kuwa ameshaibagua baina ya sehemu itakayotumika kwa uwekezaji na wananchi wapate sehemu yao isiwe kila siku mtu akijengwa siku ya pili anaondoshwa. Ningeomba pahali penye wakubwa na wadodo wadogo wapo. Baada ya kupima na kule Fumba akawekea maeneo ambayo kwamba hapa sasa ni ruhusa kwa wananchi wanaotaka kuishi maeneo ya kule au wanaotaka kuhamia kule hatutohusiana tena na mazingira mengine. Isiwe kila siku wananchi wanavunjiwa wakilipwa inakuwa kama tunaitia hasara serikali ambapo tunakuwa kama hatujaweza kuiweka mipango mizuri au mipango endelevu.

Ningeomba Waziri atakapokuja anambie mpaka lini atakuwa ameshawafafanulia watu ili mtu anaponunua na kuweka mipango yake iwe tayari maeneo yanajulika. Chengine atakapokuja Waziri hapa mimi nataka anielezee kuhusu habari ya Forodhani ya Chakechake. Nilimwambia Waziri kwamba sehemu ya Tibirinzi ambayo ina *opposite* na *Archipelago* au Hifadhi Hoteli *opposite* ni sehemu ya serikali ni sehemu ya ufukwe. Sehemu ile Mhe. Waziri wewe ulishakaa Chakechake na ulilelewa pale, umecheza Chakechake na uliwahi kuogelea ogelea maeneo yale.

Sehemu ile tokea zamani ni sehemu ya kujidai watu jioni. Chakechake tunashukuru sana serikali namshukuru Rais kwa kuupandisha mji ule kuwa ni mji wa pili nambari mbili na ni mji wa kwanza nambari moja kwa Pemba ambao ni mji mkuu. Pia nimpongeze na Mhe. Haji Omar Kheri, kwa kuchangia michango mingi Chakechake anaitizama vizuri sana nimshukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kumwambia Waziri wa Ardhi kwamba sehemu ile ya Chakechake usihadaliwe na ile mikoko kwa sheria yako mwenyewe au kwa sheria ya nchi hii kutoka barabara kuu mpaka kufika katika eneo la barabara la kuifika barabara ni mita 15, kutoka mita 15 mpaka kuifika bahari hapazidi mita ishirini au mita 10. Eneo lile linakuwa na utata sana hata katika sehemu ya mambo mengi ambayo maeneo yale ni maeneo karibu na Ikulu. Maeneo yale hayaruhusiwi sana kujenga magorofa yanayovuka ili kuiyona ikulu ndani au kuona maeneo ya Ikulu.

Lakini pia Chakechake kama Mji Mkuu hatuna sehemu ya watoto ya kujidaii zaidi ya kiwanja cha watoto ambacho kipo *profession* na sisi tunataka eneo la kuchoma moto wa kawaida, mambo ambayo ya *tradition,* kama mle kiwanda cha watoto hakiruhusiwi. Ningeomba sana Waziri utakapokuja hapa nimeshakuomba nikakwambia ukakague, ukija hapa uje unambie kwamba lile eneo tayari umeshafuta *lease* zinazokuwepo pale na tayari eneo lile umelikabidhi katika Ofisi za Serikali za Mitaa au Manispaa ili waliendeleaze katika kuweka Forodhani katika kuhakikisha watoto wana *enjoy* na mapato ya serikali yanapatikana na pia kuweka mandhani nzuri. Pale ndio kama kiyoo cha Chakechake katika sehemu ya Kibirinzi.

Ningekuomba sana Mhe. Waziri, utakapokuja unambie kwamba Chake Chake lile eneo ambalo lipo pale. Kwa sababu utakapotoa *lees* pale unasababisha kuja kuwapa tabu serikali kuja kuwapa mita zao za barabara ambazo watu wameshazijenga na wewe ni shahidi ukiteremka Tibirinzi hata hatua moja hakuna ya kutoka barabara mpaka kwenye eneo jengine, nyumba zimefungana gari ya pili inapita kwenye barabara ya nyumba sasa na kule mwisho itakuja kuwa ni hatari hata huyo Mhe. Rais atashindwa kupita.

Ningeshauri eneo lile likawekwa wazi na eneo lile ni kwa sababu kama ni nyumba moja ambayo imeshajengwa ya hifadhi ambayo ndiyo *ZSSF* ningeomba kwa eneo la Tibirinzi kutokana na matatizo yanayokuwepo sehemu zile ni sehemu ambazo kiunga uzi. Tumeiyona Wizara ya Fedha imedidimia pale imakatika na bado sehemu ya maji juzi tumepata mitihami mikubwa ya maji na hatujajua mvua za mbele zitakuwaje.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba eneo la Tibirinzi kama ilivyokusudiwa mwanzo liachiwe katika kilimo na sehemu nyengine iliyopo iwekwe sehemu ya wazi na kuweza kujidai, ningeomba sana. Lakini pia utakapokuja ningekuomba unambia kwamba uwanja wa Tibirinzi ule wa mpira unamilikiwa na nani kisheria, kwa sababu watu wanajenga tu hivi sasa na watu wengine tunakwenda tukiwavua maji na mtu anasema mimi najenga sijui wanapewa na nani na wakati uwanja ule uko kwenye mamlaka ya serikali. Kama ni wa serikali basi serikail ianze kuchukua hatua za dharura kuuliza uwanja ule ambao ndiyo kioo cha Chake Chake.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja Shirika la Umeme, Shirika la umeme limejitahidi na limepiga mwendo wa kasi kweli kweli katika hatua zake. Nilishukuru Shirika la Umeme sote ni mashahidi Zanzibar watu wanatwambia kwamba huku kwenu umeme kama utakatika zaidi ya dakika tano unarudi *other wise* iwe main *power* huko ambayo ndiyo inamatatizo, lakini kama Zanzibar basi hauchukuwi muda mrefu. Niwashukuru sana *ZECO* wanafanya jitihada kubwa na *full emergence* wanazimaliza haraka iwezekanavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikwambie katika jitihada wa kuongeza nikwambie kwamba waongezewe vijana vyombo vya maringi mawili kati ya mapikipiki au vespa kunakuwa na muda wa dharura ambapo unapiga simu sio lazima litoke gari zima na mafundi, kuna mambo mengine madogo madogo ambao wengine

wapesi wanaweza kwenda wakafutatilia wakaweza kwenda kukata kitu cha kwenye nguzo au *emergence* ya haraka haraka ningeomba kama itawezekana mfuko watafutiwe mapikipiki ili kuweza kuboresha zaidi na kuweza kuokoa maisha ya watu panapotokea matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja katika hoja ambayo Kamati ilisema hapa. Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ilitoa hoja ya kusema kwamba inataka kuunda Kamati ya kuweza kushughulikia suala la ardhi. Mimi hili suala naliunga mkono sana ni maneno mengi yameshasemwa hayajulikani ukweli wala haujulikani uwongo. Suala hili litakapokua limefanyiwa hitimisho litakuwa limemaliza na mdomo mdomo utakwisha. Ninachosema ingekuwa vizuri Kamati hii ikafanyika kwa sababu mwenye haki akajulikana na aliyekuwa hana haki akajulikana.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ina uwezo wa kumwita kila mtu ikamuhoji, Kamati inauwezo wa kumwisha mtu ikawapatanisha na wakajua kitu gani ambacho kitaendelea. Lakini Wizara kama Wizara kuna watu humu wanahangaikia kwenda Mahakamani hawapati haki zao. Kuna watu ambao kama hana uwezo wa kwenda Mahakamani anamuachia Mwenyezi Mungu, sifikirii kama serikali ina niya mbaya na wananchi wake. Ina nia njema na mimi nitaishukuru sana Kamati hii isijeikamuona tajiri ana viwanja 10 kile cha 11 isimpitikie kwa sababu ana viwanja vingi, kama ni haki yake apewe ndiyo Mungu alivyomuandikia. Kama mtu hana kiwanja lakini kile ndio kiwanja chake basi ile haki impe isimuonee mtu yeyote katika kuhakikisha kwamba inatenda haki.

Mhe. Mwenyekiti, ningeishauri Kamati, ningeishauri Wizara ikakubaliana na Kamati kwa kujua kwamba hili neno limekuwa tatizo na bora liende likamalizikie. Mimi ushauri wangu naseme kwamba ukimficha mgonjwa basi kilio kitakufichua. Ukisema

kamba hapana sijui hivi na hivi, basi kilio kitakufichua maana itakuwa migogoro haishi na utaongeza Mahakama nyengine mpaka itakuwa Mahakama ya Dunia ya Ardhi kwa sababu hizo nyengine zilikuwa zimepanda Mahakama ya Mwanzo, Mwahakama ya Wilaya, Mahakama ya Mkoa, Mahakama Kuu, sasa Mahakama zinakwenda kwa kupanda kutokana na sababu mambo yamekuwa mazito. Ningeomba kamati tukalimaliza hili ili likawa basi, hakuna mdomo tena, watu wakaendelea na shughuli nyengine na mambo madogo madogo yakaweza kufnywa maneno yamekuwa mengi, mengine yanaukweli mengine hayana kwa hivyo ningeishauri sana serikali ikakubaliana na hili.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna sheria zinakingika katika suala la haki natake useme kwamba sheria haitendi haki, sheria inatoa kama sheria haki itabakisha kuwa haki. Mtu akiweza kushindwa kutoa vielelezo vya kisheria mtu huyo hana haki hata kama ile haki ni ya kwake. Nina uhakika kuna masuala ambayo kibinaadamu unajua kama kitu hiki ni cha kwake na baadhi ya majaji ambao wametii kwa Mungu na wamekula kiapo kwa Mungu wanawatafutia watu haki zao hata kama hana haki na anajua kama kitu hiki ni cha kwako. Lakini kuna majaji kwa wenyewe wana *interest* zao akikuuliza huna cha kumueleza hata kama anajua kama ni cha kwako atampa mwenye haki.

Mhe. Mwenyekiti, haya mambo ni mambo makubwa sana na ardhi itakwenda kushtaki na itakubana kwa Dini yetu ya Kiislamu na Ramadhani hii. Ningeomba sana tusiichezee ardhi. Unachezea maji utaoga sana lakini ardhi itakubana mwenyewe, ningeomba sana suala hili likatizamwa sana ili kupunguza matatizo ambayo yanaweza yakatutokezea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakwambia tena naunga mkono hoja kwa kifungu cha 111 cha Baraza hili kwamba ipo haja ya kuunda Kamati ilipo bado uwelewa haujatimia. Ningemuomba na

utakapokuja katika majumuisho nataka hili awaulize Wajumbe kama wanalikubali au hawalikubali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Waziri atakapokuja hapa anieleze nimemwambia mara nyingi Chanjamjawiri ina eneo kubwa sana, ina kisima, ina pampu ya maji lakini kila mwenzi inaharibika na matatizo yake inakuwa hayaishi, ukosefu hasa ni tenki la *reserve*, hebu atakapokuja anambie ana mpango gani wa kuweza kuweka *reserve* ili kuipumzisha *pump* na wananchi muda wote waweze kupata maji ili wananchi waweze kufanyia shughuli zao. Nikisema hivyo nafikiri Waziri atakuwa ananielewa. Sitaki nimkwaze sana Waziri wangu, lakini lazima tu kwa sababu anawahudumikia wananchi ni lazima nimwambie.

Mhe. Waziri hivi juzi mimi nilitea sehemu, unajua unapotembea watu wanapokuona kwenye mapicha hapa watu wanakwita. Hivi karibuni nilikwenda kununua baadhi ya vitu katika barabara ya Fuoni. Siyo jimbo langu lakini nitaifa langu. Pale nilipofika kuna mtu mmoja akanambia sisi ni raia wema lakini ninachotaka kukwambia tuliipisha miundo mbinu ya barabara ili barabara na sisi tunaihitaji, tukaahidiwa miundombinu ya maji itakatwa mtapata tabu lakini baadaye itarudishwa. Akanambia kafanye *reaserch* kama unaweza, haijarudishwa baadhi ya Miundombinu watu wanapata shida ya maji, *other wise* wale wenye visima ndio wanaopata maji. Kwa hivyo ningeshauri kwa sababu ni maendeleo na tunahitaji na wakanambia sisi si Mbunge wala kitu gani lakini tunakuomba na wewe tupigie debe nikamwambia tena kwa nanihi niandikie mesaji ili iwe ushahidi wangu ameniandikia na mesaji na ukitaka nitakupa.

Mheshimiwa mimi niendelee kidogo katika mazingira ni kwamba nataka nikwambie kwasababu unapowahudumia watu basi ni Serikali na Mheshimiwa mimi nataka nikwambie sitaki kumtuhumu mtu lakini nataka nikwambie kwa ushahidi wangu

sijui Unguja lakini Pemba mpaka sasa hivi kuna watu bado hawajaridhika na matokeo ya Serikali kuongeza nchi, bado wanatumia *interest* zao za kuharibu ama za kufanya vitendo ambavyo wananchi wachukie katika maeneo fulani ili mradi Serikali isemwe hata kama Serikali imeweka miundo mbinu mizuri bado wataharibu na baadhi ya watu wengine pia ni Watendaji anaweza kwenda pale mtu akamjibu maneno ya kijeuri ili atoke huko hii si Serikali au hawa watu wa hivi ningeomba Maofisa wako walioko Pemba wakajaribu katika vituo katika maeneo yao kupitia wakikagua kagua na kutafuta maoni.

Mheshimiwa mnafanya kazi kubwa sana na Pemba wanajitahidi kwenye Shirika la Umeme, Maji na kila kitu lakini *still* Pemba ni *hundred percent* maji sasa hivi nataka nikwambie kuliko hata Zanzibar lakini anaweze mtu anafunga ile *pump* wiki nzima anaenda kwa mke mwengine anakwambia hayupo, haya muyatizame vizuri kwasababu hatuna tatizo la maji Pemba hilo nalishukuru sana.

Jengine Mheshimiwa...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika mbili

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante Mheshimiwa nataka nizungumzie mazingira. Mheshimiwa neno la mazingira tunalichukua kama mazingira kama sijui jirani yako, kama upeni, kama asumini, sijui na kiluwa ndivyo tunavyofikiri mazingira lakini Mheshimiwa mazingira ni upeo mkubwa sana sana hiyo unayosikia mabadiliki ya tabia ya nchi yote mazingira, nimeshapata funzo kwa Pemba sasa hivi kujuwa mazingira nini mheshimiwa katika jumla ya maumbile ya ardhi katika jumla ya mambo ambayo tunayo mito, milima, maziwa, mabonde yote ni jumla ya maumbile ya Mwenyezi Mungu katiki kupamba ardhi yake tunahitaji milima iwepo na ndiyo inayotusaidia Pemba mvua

yote iliyonyesha hii kama si milima tungekuwa hatupo tena na mabonde, sasa tunayahitaji yale milima ambayo iko mjini mjini tunaona nchi za wenzetu inapambwa kwa ujenzi ambao inayopendeza wala haimong'onyoki tena zaidi ya kupendeze na kuona nini. Ningeomba sana basi tutafute mafungu ambayo na wafadhili kutusaidia mji kama wa Chake Chake *total hundred percent* ni mji ambao una milima una mabonde umekaa vizuri katika mapambo yake hauko sawa ni mji wa milima milima.

Ningeshauri ukapambwa kama ulivyo kuwa mji mkuu ukaweza kupambwa ili ule mji ukapendeza sio yapukutike madongo yaanguke miti ikawa kitu gani ile miti Mheshimiwa mti mmoja ukianguka miaka kumi, kumi na tano hatuupandi tena ule hauko katika nchi yetu lazima mazingira tuyakubali na tuyaweke katika mazingira mazuri sana.

Jengine Mheshimiwa nataka ufanye utafiti wa kina kuhusu eneo la *Qatar* utafute watu usichukuwe maneno ya kawaida ya binadamu kwamba ahaa ndio mazowea ndo kitu gani, Mheshimiwa eneo la *Qatar* kutoka kwa Makamo wa Pili wa Rais mpaka kuja banda la kahawa ambalo Mhe. Haji Omar Kheir anajenga soko pale la *Qatar* lile eneo linakaa uchafu, lile eneo linajazika kwani tusilijaze lile eneo tukatengeneza mazingira mazuri ambayo yatatupatia faida ya kodi ya kuweka kila aina...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa malizia muda wako umemaliza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti na ahsante sana lakini kidogo tuu namalizia kwani hebu kaa utafakari na wataalamu wako kwanini tusijaze tukapata sisi shida yetu ardhi kuliko bahari kwa hivyo ningetaka Mheshimiwa hebu jaribu kuangalia na wataalamu zaidi tuweze kuangalia ili kujaza.

Lakini Mheshimiwa la mwisho tumekwenda tena kwenye nchi za wenzetu Mheshimiwa watu wana heshimi sheria za ardhi. Mheshimiwa tumekwenda Kenya tumeenda maeneo mengine umeambaiwa mita thelathini ni maeneo ambayo ya *public* usichezee na bahari lakini kwanini tunamuona Muwekezaji au mtu wa ardhi anajenga chini ya ufukwe mita thelathini ziko wapi mwisho unamkuta mtu sasa akitaka kupita akitaka kwenda hoteli ya pili akazunguke tena akapite huko aje hoteli ya pili kutokana na mazingira ya sheria ya Serikali yakumruhusu mwananchi tumeziba tumempa uhuru yule...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umemaliza

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru naunga hoja Mheshimiwa mpaka atakapokuja Waziri kunipa haya nitaunga hoja sasa hivi kwanza nakaa *standby*. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa kwa mchangio nilimwita Mhe. Hidaya kwa vile hayupo mbele ya macho hapa namwita Mhe. Ahmada Yahya na baadaye atafuatia Mhe. Nassor Ali Jazira kwa dakika tano.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, namimi kuniona ili niweze kutoa mchango wangu katika wizara hii ambayo nina uzoefu nayo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimefanya kazi wizara hii karibu miaka kumi na sita kabla ya kustaafu mwenyewe napenda nimpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kumuona ndugu yangu Bi. Salama kwamba anaweza na anatosha kabisa kufanya kazi kwenye Wizara hii kama ni Waziri.

Hapo hapo napenda kuwapongeza Watendaji wote wa Wizara hii Katibu Mkuu Ndugu Ali Halil Hassan Mirza, Wakurugenzi wake

wote na Manaibu Waziri, mchango wangu mimi utajikita katika *angel* mbili. Zanzibar inaendelea katika nyanja mbali mbali na haki ya mwananchi na raia kupumzika baada ya kazi ngumu kwa kipindi cha miaka mingi nchi yetu ina sehemu moja tuu ya kupumzikia ambayo ni *Forodhani Park* wananchi wote wa Zanzibar wamekuwa na mwitikio mzuri wa kwenda kupumzika kupata hewa na kupata vyakula vya kitamaduni katika sehemu ile.

Mhe. Waziri, wakati umefika nakushauri kwamba eneo la Ng'ambo nalo linahitaji ipate huduma kama ile ukiangalia na kufanya *survey* hata leo nenda idadi ya watu wanaokuja Forodhani sasa hizi imekuwa imezidi zaidi ya kiwango cha uwanja wenyewe, katika miaka ya nyuma ilikuwa imeingia *consent* kwa nini sasa hivi eneo la uwanja wa Amani panachongwa magogo magogo ni eneo zuri la kujenga *park* kwa ajili ya watu tunaoishi Ng'ambo tuweze kupumzika pamoja na watoto wetu. *(Makofi)*

Eneo hilo linatosha na nimelipima kwa macho ndani ya miezi mitatu nyuma kwamba baada ya njia ya kwenda nyuma Uwanja wa Amani ukija mpaka huku ukija huku basi inatosha pale kupewa Mwekezaji ya aina yoyote au hata wizara iweze kujenga tupunguze mzigo wa Forodhani isiwe Forodhani tuu tunataka mji ubadilike na hii imo ndani ya kitabu chako cha bajeti ukurasa wa 17 kuhusu Upangaji wa Mipango ya Miji Midogo Midogo.

Kwa hiyo Mhe. Waziri si hiyo tuu hata hii eneo la Kiembesamaki pale panatosha bustani kadhalika kufanya kadhalika viwanja vidogo vya kupumzikia watoto, sisi tumebahatika kusafiri hili si jambo la ajabu kwamba kila *District* basi kuna viwanja vya watoto wanakwenda kupumzika na watu wazima, mle mle inapatikana ajira kwa sababu tukitaka tusitake utamaduni wa vyakula vyetu vidogo vidogo urojo, chipsi na kadhalika basi ajira itapatikiana nakuumba sana Mheshimiwa wakati utakapopanga

Master Plan mji jambo hilo uli *consider* hata kama bajeti ijao, kiuwezo napenda mimi kuchokoza chokoza katika mambo ya *Building Society* wala hahitaji gharama kubwa, ukiangalia pale *Forodhani Park* hakuna utaalamu mkubwa uliotumika lakini mjenzi aliposhirikiana na Serikali kapanga sehemu vizuri sana katumia zile *pavement* na *interlock* na kagawa hapa pawe hivi hapahitaji hata gharama kubwa ni gharama nafuu ili na sisi huku Ng'ambo tupate pahala pakupumzikia.

Nchi imeendelea sasa katika ushauri ninaokupa ndani ya Uwanja wa Amani inatosha kidogo kumega sehemu kidogo alau magari yakaingia kule kwa hiyo Mheshimiwa hiyo ni *angel* ya kwanza huo ni ushauri.

Angel ya pili ni kwamba mnafanya kazi mnafanya kazi nzuri hasa Shirika la Umeme. Shirika la Umeme ninalolijua mimi kwasababu mimi ni mchokozi chokozi katika mambo ya kujenga jenga Shirika la Umeme la miaka kumi na tano nyuma sio Shirika la Umeme la sasa, sasa limejikweza katika kuwahudumia watu na ukiangalia lina dhana za kutosha lakini sifa ambayo sasa hivi ya pekee kwamba Shirika sasa linaongozwa na Wataalamu Wazalendo wa hapa hapa, tena wala hawaringi alianzia Hassan Mbarouk alikuwa *engineer* kabla ya hapo alikuwa *main engineer* leo ni Meneja kwa hiyo hii ni sifa kubwa kwamba nchi yetu imejitahidi kwa kiwango kikubwa sasa kusomesha wazalendo na sasa wanashika nafasi kuendesha nchi yao.

Kwa hayo machache Mheshimiwa mimi sina tatizo Wizara ninaijuwa nimefanya kazi jengo lile mimi kwa muda wa miaka kumi na tatu mzee wako alikuwa Waziri wangu leo hii mia chini mia naunga mkono bajeti hii ipite bila ya pingamizi yoyote. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Ahmada Yahya sasa anafatia Mhe. Nassor Ali Jazira na baadaye Mhe. Suleiman Makame ajitayarishe.

Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira): Ahsante Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi kidogo ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mheshimiwa kwanza nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini la pili nichichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wetu wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein pamoja na Serikali yake lakini nimpongeze sana sana Waziri wetu Dada yangu Mhe. Salama Aboud pamoja na Naibu wake Mhe. Makungu na Katibu Mkuu ndugu yangu ndugu Mirza, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mkurugenzi Mkuu wa *ZAWA* lakini vile vile Mkurugenzi wa *ZURA* halikadhalika Mkurugenzi wa *ZECO*.

Mheshimiwa kwa kweli Wakurugenzi wetu hawa wanafanya kazi kizalendo na wanastahiki kupewa pongezi na Ishaallah Mwenyezi Mungu awape imani lakini yote haya ni kutokana na Uongozi mzuri wa Waziri wetu.

Mheshimiwa nije katika kazi kawaida za Mamlaka ya Maji *ZAWA.* Mheshimiwa nichukuwe fursa hii kwasababu wananchi wangu wa Jimbo la Kikwajuni katika maeneo ya Mwembeladu wamenituma ili nitowe pongezi zangu hizi kwa Mamlaka ya Maji *ZAWA* baada ya kutokea maharibiko katika wakati wa mvua kwa kupasuka bomba la maji pale Mwembeladu.

Mheshimiwa baada ya kuwapa taarifa *ZAWA* siku ya pili walikuja kufanyia kazi bomba lile na kwa kweli siku ile wananchi wote wa

maeneo yale ya Mwembeladu walipata faraja na kutowa pongezi zao kwa *ZAWA* kwa kutengeza bomba lile kwa hiyo, hongereni sana *ZAWA*.

Mheshimiwa ndugu yangu Mwakilishi wa Jimbo la Mtoni Mhe. Bhaa kazungumza neno ambalo kwa kweli mimi nimpe pongezi nina imani kwamba Waziri atakapokuja pia atampa pongezi kwa hotuba yake ua kwa machango wake ambao ameutowa.

Mheshimiwa katika kutoa elimu kwa watumiaji wa maji *ZAWA* bila ya kusaidia sisi tukiwa kama viongozi, tukiwa kama wananchi kwa kuweza kuchangia katika kutoa huduma za maji Mamlaka ya *ZAWA* haitofika mahali kwa hivyo wajibu wetu kama viongozi kuwashajihisha wananchi wetu na Mhe. Bhaa kasema hapa haba na haba hujaza kibaba hata kama shilingi elfu tano, elfu sita basi ni wajibu wetu sisi kuwashajihisha wananchi wetu ili waweze kuichangia *ZAWA* ili kusonga mbele katika kutowa huduma zaidi katika kutowa maji kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa katika kitabu chake Mheshimiwa amesema kwamba wanachama au wateja waliounganishwa na kuwekewa mita ni takribani 1,582, lakini watumiaji wa maji Zanzibar hivi sasa takribani asilimia thamanini wanapata maji na katika Zanzibar tuna watu takrbani 1,500. Sasa niombe *ZAWA* kuhakikisha kwamba tunafanya bidii zaidi ili kuongeza wateja kuwaunganisha mita ili *ZAWA* iweze kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa nikija katika mradi wa uchimbaji visima wa Ras al Khaimah nishukuru sana Serikali na nimshukuru sana mtawala wa Ras al Khaimah kwa kuweza kutusaidia kuchimba visima hivyo. Lakini Mheshimiwa kuna msemo mmoja ambao unaosema na Mhe. Kibano msema huo anaujua zaidi kwa sababu siku moja Mhe. Mwenyekiti, kamati yako ya Baraza la Wawakilishi tulifanya ziara kule katika Jimbo la Mtambwe na baada kufika

kule kuna mwananchi mmoja alisema neno alisema hivi "maji yatekwayo ndiyo yavaayo" maji yatekwayo ndiyo yavaayo maana yake ni kwamba yale maji yanayochimbwa katika visima vile baada ya kutumika ndiyo yanayofaa kwa hiyo vile visima ambavyo vilivyochimbwa.

Mimi nimshukuru sana na kumpongeza Mhe. Mwakilishi wa Jimba la Mtambile Mhe. Mgaza, kwa kuweza kuchangia fedha taslim ili kisima chake ambacho kilichimbwa na mfadhili huyu wa Ras al Khaimah katika maeneo ya Kengeja Mjiweni ili kumalizia matengenezo ya kisima kile halikadhilika Ndugu yangu Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni Mhe. Shamata ameahidi kuchangia takribani shilingi milioni tano (5,000,000) ili kuhakikisha kwamba visima vile ambavyo vile vinachimbwa vinamalizika ili wananchi wetu waweze kupata huduma ile ya maji. Haya ndiyo maendeleo na sisi kaka viongozi tunatakiwa tuunge mkono juhudi za Serikali yetu na Mamlaka ya Maji *ZAWA*.

Mheshimiwa uchimbaji huu wa visima hususan katika maeneo ya vijijini *ZAWA* imefanya kazi kubwa chini ya Uongozi Waziri wetu lakini vile vile Serikali yetu imekuwa ikifanya kazi kubwa sana kutafuta wafadhili mbali mbali ili kuondoa tatizo kubwa la maji linalowakabili wananchi wetu, katika maeneo ambayo yalikuwa na tatizo kubwa la maji likiwemo Jimbo la Kikwajuni Mheshimiwa Kikwajuni katika majumba ya Mjerumani mimi nimeingia uwakilishi katika Jimbo la Kikwajuni mwaka 2015 na nilikuta tatizo hili la maji katika maeneo ya Kikwajuni majumba ya Mjerumani.

Lakini leo kutokana na juhudi na maarifa, na mipango ya wafanyakazi wa *ZAWA*, nichukue fursa hii kuwapongeza sana *ZAWA*. Leo majumba ya Mjerumani maji yanatoka, hongera sana Mhe. Waziri. Nilikuwa nikipiga kelele sana kuhusiana na tatizo la

maji katika majumba ya Mjerumani, lakini ule ushauri niliokuwa nikiutoa umefanyiwa kazi na leo majumba ya Mjerumani maji yanatoka. Lakini bado katika maeneo mengine nina imani kwamba *ZAWA* italifanyia kazi ili kuhakikisha maeneo yale yote yanapata maji.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mengi ambayo yamesemwa kwa wachangiaji wenzetu humu ndani kuhusiana na mgogoro wa matatizo ya ardhi. Mwenyekiti wangu Mhe. Hamza Hassan Juma katika ripoti yetu ya kamati ametoa mapendekezo na maelekezo Mhe. Mwenyekiti kwa uongozi wako ulionao chini ya Spika wetu nina imani hili kwa uelewa wa Mhe. Waziri, suala hili nina imani litakwisha na Mwenyekiti wetu wa Kamati chini ya uongozi wake tutalisimamia ili kuhakikisha migogoro hii ya ardhi inakwisha na inamalizika kabisa kwa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili limetajwa na viongozi mbali mbali waliokuwepo huko nyuma, lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa uelewa na ufahamu mkubwa wa Mhe. Waziri amekuwa akitupa ushirikiano mkubwa sana kamati yetu ambayo inaongozwa na Mhe. Hamza. Mimi nina imani kwa uongozi wako Mhe. Mwenyekiti, chini ya Spika wetu haya matatizo tutayafanyia kazi na ninaomba mtuamini wakati tutakapokuja kwenye kikao kitakachokuja, basi ripoti hii tutaileta na itakuwa tumelifanyia kazi kulimaliza na kutoa ripoti ambayo itakuwa na manufaa kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba wawakilishi wenzangu tuiunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, hotuba hii ni mafanikio ya serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. Hotuba hii ni kujenga maendeleo ya wananchi wetu, ni kuijenga nchi yetu, ni kujenga kuleta kutatua matatizo ya wananchi wetu yakiwemo matatizo ya maji, matatizo ya ardhi, matatizo mbali mbali ambayo yanawakumba wananchi wetu. Kwa hivyo, niwaombeni sana

waheshimiwa wenzangu tuiunge mkono, tumpe kazi Mhe. Waziri aende akafanye kazi ili wananchi wetu wapate maendeleo, wananchi wetu wana imani na viongozi wetu, wananchi wetu wana imani na Rais wetu. Kwa hivyo, ni wajibu wetu tukiwa kama viongozi tuwe na imani na mapenzi na nchi yetu, tuwe na imani na mapenzi kwa Rais wetu, tuwe na imani na waziri wetu. Waziri wetu ni mwana mama anafanyakazi vizuri, asubuhi, mchana na usiku mama yuko mabondeni kwenye maji, mama yuko mabondeni kwenye ardhi kila mahali yupo anahangaika usiku na mchana. Mhe. Mwenyekiti, mimi nayaona kwa sababu huko tunakokwenda mabondeni tunayaona kwenye matope, kwenye mvua anahangaika mwanamke huyu, tumpe nguvu, tumuamini afanye kazi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema haya kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati naelewa vizuri sana matatizo ya wizara hii, na ninajua vizuri utendaji wa Mhe. Waziri wetu pamoja na Naibu wake na Katibu Mkuu. Kwa hiyo, mimi naiunga mkono kwa asilimia mia moja na nawaomba waheshimiwa wenzangu tuunge mkono ili waziri wetu akafanye kazi kuleta maendeleo kwa wananchi wetu. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo atakuwa ni Mhe. Suleiman Makame Ali. Karibu sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla ya kuchangia kama kanuni hairuhusi, lakini naomba uniruhusu nimpe pole Kada mwenzangu, rafiki yangu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo ndugu Juma Ali Juma kwa kupata mtihani jana, kwa kuunguliwa nyumba yake na

moto. Nimuombe aendelee kuvuta subra ni mambo ya Mwenyezi Mungu, ni mipango yake mwenyewe kwa hiyo mimi mwenyewe binafsi kwa sababu aliwahi kuwa mgombea wangu wa Jimbo la Ziwani kupitia Chama cha Mapinduzi na mimi nikawa Meneja Kampeni wake nitaweza kumsaidia japo chochote kama mchango wangu.

Mhe. Mwenyekiti, badala pole hiyo niende moja kwa moja kwenye suala la maji. Mhe. Mwenyekiti, hivi juzi nilikuwa nikiangalia Bunge nikamkuta Mbunge mmoja kule Dodoma akasema kwamba bila ya maji huwezi kufanya chochote, hata mtoto anakushinda kama huna maji, yaani kumpata huyo mtoto. Ni kweli naunga mkono kwa suala lile ni kweli kwa sababu bila ya maji huwezi kuoga, huwezi kufua, huwezi kufanya lolote. Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la maji nimpongeze ndugu Juma Bakari Alawi (JB) Afidha Mdhamini wa Maji kule Pemba na ndugu Omar Mshindo Bakari Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji kule Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Ziwani kuna shehia sita. Kuna Shehia ya Ndagoni, Wesha, Michungwani, Ziwani na Mbuzini. Shehia hizi zote tatizo kubwa la maji lilisakili kule Ndagoni, Afisa Mdhamini na Mkurugenzi walishirikiana na mimi kwa hali yoyote, kwa njia yoyote ili kuhakikisha kwamba tatizo la maji Ndagoni linaondoka. Ni kweli tatizo hilo limeondoka Mhe. Mwenyekiti, nataka kukwambia mpaka hivi sasa napigiwa simu kuanzia saa sita za usiku napewa hongera kwa suala la maji kuliondoa Ndagoni. Napewa pongezi kwa tatizo lile la maji tulikuwa na kisima cha Ras-al-Khaimah pale kimetumika nimetoa shilingi milioni 10 za jimbo na mimi mwenyewe nimechangia ili kuhakikisha tatizo hili la maji linaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, mpaka kwenye umeme kule Mkumbuu ilikuwa wana tabu ya maji nadhani Afisa Mdhamini ni shahidi analijua

hilo, walikuwa wanapelekewa maji kwa magari lakini mpaka wale wanaolinda umeme kule Mkumbuu hivi sasa wanatumia maji yale ambayo kwamba nilihakikisha kulisimamia suala lile. Kwanza nawapongeza sana hawa na nawaomba wazidi kushirikiana na mimi na kwa yeyote yule ili kuhakikisha tunaitekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye migogoro ya ardhi. Mhe. Mwenyekiti, kama utakumbuka asubuhi nilimuuliza Mhe. Naibu Waziri hapa kwenye maswali na majibu katika migogoro hii ya ardhi kuna baadhi ya masheha pamoja na watendaji wake wa wizara yake wanasababisha migogoro hii, akanambia kwamba hajui. Kwa hiyo, mimi nataka kumwambia Mhe. Naibu Waziri kama yeye hajui mimi najua kwamba hayo yapo na kama atataka ushahidi wa hili tukimaliza Baraza basi mimi niko tayari kwenda kumpeleka ili ajionee mwenyewe mgogoro ule ulivyosababishwa na watu hao.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye Shirika la Umeme, niwapongeze sana watu wa Shirika la Umeme. Lakini Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu ndio tunayoitekeleza, ukurasa wa 154 inasema hivi.

> “Sekta ya nishati hususan umeme ni nyenzo muhimu katika kukuza uchumi na maendeleo ya jamii. Aidha, matumizi ya nishati ya umeme hurahisisha shughuli nyingi za kiuchumi, kuongeza kasi ya uzalishaji na kuwawezesha wananchi kujiajiri wao wenyewe”.

Mhe. Mwenyekiti, kujiajiri wenyewe kuna wengine wanafanya *juice*, wanaweka samaki wao kwenye mafriji na mambo mengine na mangine mengi. Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti waheshimiwa wengi wamesema hapa kuhusu suala la umeme kuna baadhi ya vijiji, nilithubutu kusema kwamba shehia zote sasa hivi nina imani

kwamba kwa Zanzibar kupitia ilani ya Chama cha Mapinduzi na Chama cha Mapinduzi ndio kinachotekeleza kila kitu na hakuna asiyejua hilo, hakuna hata shehia moja ndani ya Zanzibar hii iliyokuwa haina umeme. Mhe. Mwenyekiti, lakini kila penye faida na kasoro zipo, kwa hiyo kuna baadhi ya maeneo mengine vile vijiji vilivyomo ndani hawajafikiwa na umeme, lakini sasa kama mwakilishi hana uwezo wa kununua nguzo 20, 30 kupeleka umeme. Leo watu wa Shirika la Umeme ukiwauliza wanakwambia tuletee orodha ya majina ya watu wanaohitaji umeme. Orodha ile wanapelekewa lakini hawafanyi lolote.

Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri na nadhani bajeti yake hii haitukuwa na mabuti sana kwa sababu hakuna hata mmoja aliyenyanyuka akamponda Mhe. Waziri isipokuwa ni kumpongeza kwa utendaji kazi. Mimi niungane nao wale wote waliompongeza na hata mimi niseme kwamba sitopiga buti kwenye wizara hii, kwa sababu kwenye suala lile la Ndagoni Mhe. Waziri alinisaidia ilikuwa zinatakikana shilingi milioni 14,031,000, milioni 4,031,000 zimetoka wizarani kwake yeye mwenyewe Mhe. Waziri amezitoa. Kwa hiyo, na mimi Mhe. Waziri wala sina cha kuzuia hapa kusema la ukweli, isipokuwa ni kwamba tukupe meno udhidi kutafuta ufanye kazi ili utekeleze ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende hapo hapo kwenye suala la umeme. Mhe. Mwenyekiti, kama utakumbuka mara nyingi napiga kelele humu kuhusu suala la umeme. Mhe. Mwenyekiti, umeme kule Pemba umetoka Ndagoni lakini ikianguka nguzo ya umeme kule Pemba nzima itakuwa haina umeme hata wewe mwenyewe Mhe. Mwenyekiti utalala kiza kwa sababu unatoka Pemba, utakosa na maji. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri ahakikishe kwamba suala lile la barabara ya Ndagoni ashirikiane na Wizara ya Miundombinu pamoja na Tawala za Mikoa ili kuhakikisha kwamba barabara ile ya Ndagoni kwenye

miundombinu imejengwa kwa kiwango cha lami, kwa sababu inafika mpaka wale walinzi wa umeme wanapata tabu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi sitaki niseme mengi kwa sababu hii wizara kusema la ukweli nadhani haina makosa, kwa sababu hata Mhe. Jaku Hashim Ayoub akikusifu hapa basi sijui tena usifiwe na nani. Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia, isipokuwa namuomba tu dada yangu kwamba azidi kuchapa kazi na sisi tuko nyuma yake tutamsaidia. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, kwanza hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuweza kukaa muda wote hapa na kuweza kuchangia wizara hii kwa upana mkubwa sana. Wajumbe ni wengi ambao wamejitokeza na ni wachache sana watakaobakia kumalizia kesho. Kwa kuwa muda wetu tena hautoshi uliobakia ni mdogo sana nawakumbusha Wajumbe Wawakilishi wote wa CCM kuendelea kwenda kwenye kikao cha Kamati ya CCM katika ukumbi wa juu, mara baada ya kuakhirisha kikao hiki.

Baada ya hayo nachukua fursa hii kuakhirisha kikao hiki mpaka kesho saa 3:00 asubuhi panapo majaaliwa.

(Saa 8:49 mchana Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 07/06/2017 saa 3:00 asubuhi)